**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 25 Machi, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** *Bismilahi Rahman Rahiim.* Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** *Bismilahi Rahman Rahiim*. Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani juu ya Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 31**

**Ujenzi wa Soko Jipya la Wete**

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad (Kny: Mhe. Farida Amour Mohammed)** - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali inayo nia njema katika ujenzi wa soko jipya la Wete na kwa kuwa ni muda mrefu sana ujenzi wa soko hilo umekuwa ukizungumzwa kwa maneno tu bila ya utekelezaji wowote wakati tayari wadhamini (Benki ya Dunia) walishakubali kuanza kwa ujenzi huo tokea mwaka 2011 ambao utakuwa ni wa ghorofa moja na fedha za Kitanzania Shs. 1,400,000,000/- (Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Nne) zilishatolewa.

a. Je, ni lini hasa ujenzi huo utaanza na ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kuchelewa kuanza ujenzi wa soko hilo wakati fedha tayari zilishatolewa.

b. Je, mchoro ambao ulikubaliwa na wadhamini ni ule ule wa ghorofa moja au umebadilika, kama umebadilishwa ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kubadilishwa kwa mchoro huo wakati wadhamini walishakubali mchoro wa mwanzo ambao ni wa ghorofa moja.

c. Je, kucheleweshwa kuanza kwa ujenzi wa soko hilo serikali haioni kuwa ni kuwanyima fursa za kiuchumi wananchi wa Wete na Zanzibar kwa ujumla.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Spika, ukarabati wa soko la Wete utaanza hivi karibuni baada ya Mkandarasi kupatikana. Mradi huu umechelewa kuanza kutokana na taratibu za upatikanaji wa Mkandarasi kwa mujibu wa masharti ya Benki ya Dunia zilizokuwa hazijakamilika, lakini kwa sasa Mkandarasi ameshapatikana na kazi itaanza hivi karibuni. Naomba pia nimfahamishe Mhe. Mjumbe kuwa fedha za Benki ya Dunia huwa haziletwi hapa nchini wanachofanya ni kutoa taratibu za manunuzi na watakaporidhika kuwa kila kitu kimekamilika kama wakiona ni sawa, basi wao humlipa Mkandarasi moja kwa moja na sio kutupa sisi fedha ili tumlipe Mkandarasi.
b. Mhe. Spika, mchoro ambao ulipendekezwa na Madiwani wa Baraza la Mji Wete ulikuwa wa ghorofa tatu na sio ghorofa moja kama Mjumbe alivyosema. Hata hivyo, Benki ya Dunia hawakuukubali ujenzi mpya wa soko la ghorofa tatu kama mchoro ulivyowasilishwa. Sababu zilizowafanya wasikubaliane na mchoro huo ni kuwa ulikuwa unaondosha kabisa haiba ya soko la kihistoria la Wete na pia gharama za kujenga jengo la aina hiyo ni kubwa na Benki ya Dunia huwa hawaendeshi mradi nusunusu kama walivyosema Madiwani kuwa lingemalizwa kwa utaratibu mwengine. Kung'ang'ania ujenzi kwa mchoro huo kungewafanya Benki ya Dunia kukataa kutoa fedha na sisi wenyewe hatuna fedha za kulijenga soko hilo hali ya kuwa sasa soko hilo liko katika hali mbaya.

c. Mhe. Spika, serikali haina nia ya kuwanyima fursa za kiuchumi wananchi wa Wete na Wazanzibari kwa ujumla, bali kinachoendelea sasa ndicho kinachowahakikishia fursa kwa vile ukarabati utaanza hivi karibuni, tungefanya kinyume chake ndio tungewanyima hiyo fursa anayosema Mjumbe, kwani wangezuia fedha na tusingepata hata hicho kinachoendelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri uzoefu unanionesha humu ndani kuwemo serikali iko mbioni matunda yake tu mara tu kwa vile Mwenyezi Mungu kaumba wiki, mwezi, mwaka hebu awahakikishie wananchi lini kazi itaanza wiki ijayo, mwaka ujao au mwezi ujao ni suala dogo tu Mhe. Waziri.
**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, tayari Mkandarasi amesharipoti toka tarehe 20 mwezi huu kwa ajili ya kazi ambazo zimepangwa kutekelezwa kwenye mradi huu. Kwa hiyo, saa yoyote kutoka hapo aliporipoti kwenye *site* ujenzi wa soko hili utaanza.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Pamoja na serikali kuwa na nia njema katika ujenzi wa soko jipya la Wete lakini Mhe. Spika lipo soko la Kangani katika Wilaya ya Mkoani-Pemba hadi hii leo bado limeshindwa kumalizika.

Je, Mhe. Waziri unawaambia nini wananchi kwa kipindi hiki kumalizika au kutokumalizika. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, soko la Kangani halimo katika Mradi huu wa ZUSP, lakini limo katika mpango wa Halmashauri ya Mkoani katika bajeti hii ya mwaka 2015/2016 na saa yoyote kuanzia sasa fedha zitakapopatikana basi mradi huo utaendelea kujengwa. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Unajua mimi ile Mkoani ilikuwa sikuisikia vizuri wala hii sio kuchomekea, kuchomeka haswa, Mhe. Waziri tunakushukuru (*Makofi*)

**Nam. 32**

**Ufungaji wa Mashine za CCTV**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** – Aliuliza:-

Kwa kuwa matukio ya kutumia uhalifu wa kutumia nguvu yamekuwa yakiongezeka katika Miji yetu hususa Mji Mkongwe wa Zanzibar, na kwa kuwa waathirika wakubwa wa matukio hayo ni wageni wa watalii na kwa kuwa serikali kwa muda mrefu imekuwa ikiahidi Baraza hili tukufu kufunga mashine za kielektroniki (*CCTV Camera*) ili kunasa matukio ya uhalifu.

(a) Je, ni lini ahadi hiyo zitatekelezwa.

(b) Kwa kuwa utalii ni nguzo ya uchumi wa Zanzbar kwa nini serikali haiweki ulinzi wa masaa 24 ya doria ili kuhakikisha usalama wa wageni na wananchi wa Zanzibar.

(c) Camera hizo za *CCTV* zinagharimu kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye kifungu (a), (b) na (c) na kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba uhalifu dhidi ya watalii umeongezeka katika maeneo ya Mji Mkongwe, ingawa si katika kiwango cha kutisha ukilinganisha na Miji mingine. Hii ni kutokana na sababu kadhaa ikiwemo hii ya kutokuwepo kwa mfumo wa ulinzi wa kutumia vifaa vya kisanyansi kama vile *CCTV* na ndio maana sasa mkazo unawekwa kuona kwamba mfumo huo wa ulinzi unakuwepo ndani ya Mji wetu.

Mhe. Spika, kuhusu waathirika wakubwa wa matukio ya uhalifu kwa wageni hususan watalii, dhana hiyo haina ukweli. Waathirika wakubwa wa vitendo vya uhalifu katika Mji wa Zanzibar ni wananchi kuliko wageni. Mara kadhaa Jeshi la Polisi limekuwa likikabiliana na kupokea au taarifa za matukio ya kihalifu kama wizi na unyang'anyi wanayofanyiwa wananchi kuliko wanavyofanyiwa wageni.

Tatizo liliopo ni kuwa matukio ya uhalifu wanayofanyiwa wageni huwa yanavuma sana kutokana na kutangazwa na vyombo vya habari vya ndani na nje ya Nchi, wakati ambapo matukio ya aina hiyo hiyo wakifanyiwa wananchi huwa hayasikiki kutokana na kutotangazwa sana na vyombo vya habari vya nje ya nchi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa namjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imeahidi kufunga mashine za kielektroniki za kuwatambua wahalifu katika Mji wa Zanzibar. Kwa hivi sasa wataalamu wanaendelea na kazi ya kuchambua mambo ya kitaalamu ya mradi huo na mara baada ya kukamilika kazi hiyo na kupatikana fedha kazi hiyo itaanza.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia Jeshi la Polisi imeweka ulinzi kwa masaa 24, na wanazunguka maeneo yote ya mji wetu kwa kutumia magari, pikipiki na pia kutembea kwa miguu. Aidha, Polisi Jamii wamekuwa wakishirikiana vizuri na Jeshi la Polisi na wameweza kupunguza matendo au vitendo vya kihalifu yaliyokuwa yanatokea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

(c) Mhe. Spika, hakuna bei maalum ya *camera* za *CCTV*, *CCTV* au bei ya *camera* hizo inategemea aina ya *camera,* ukubwa wa *camera*, ubora wa picha inayohitajika na mifumo mengine

inayoambatana na *camera*. Kama ilivyo kwa vitu kama gari huwezi kusema gari ni kiasi gani hadi uwe na maelezo mengi ndio utakisia bei ya kununulia gari.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwa kuwa suala hili la kuweka *camera* na kusaidia ulinzi limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu, serikali imefikia hatua gani mpaka sasa kutokana na umuhimu wa vifaa hivyo ili kusaidia mradi huo. Hilo la kwanza.

La pili, kwa usalama siku zote unaimarika zaidi pamoja na kuwepo taa lini mtaweka taa katika vichochoro vya Mji Mkongwe ili ule Mji uzidi kung'ara au tunasubiri ule wimbo wa UNESCO uje kutusaidia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** (a) Mhe. Spika, hivi karibu tu serikali itamaliza kukamilisha taratibu zote kwa ajili ya kuweka *camera* za *CCTV* ndani ya Mji wa Zanzibar.

b) Katika mradi huu wa kuweka *camera* za *CCTV* pia ipo component kwa ajili ya kuweka taa za vichochoro vyote ambavyo Mhe. Mwakilishi amevitaja.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikauliza swali dogo la nyonge kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kumsikia Mhe. Waziri aliposema kwamba serikali sasa hivi ipo katika hatua za mwisho za mchakato wa uchambuzi wa utaratibu wa kuweka *CCTV* camera katika Mji wetu. Suala langu ni kwamba huu mradi unaofanyika sasa hivi wa uchambuzi wa uwekaji camera ni mradi maalum wa serikali au kuna kampuni ambazo zimejitokeza wanataka kufunga hizo *CCTV* camera au serikali inaweka utaratibu nini inahitaji halafu baadae itatoa tenda kwa ajili mchakato watu kuomba kuweka hizo *CCTV camera.*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba mradi huu ni mradi wa serikali na mradi huu katika kufanya taratibu na kukamilisha mchakato tumeangalia aina zote hizo ambazo Mhe. Mjumbe ameziulizia. Kwanza sisi wenyewe kuweza kuufanya huu mradi lakini pia aina ya pili ni kuweza kushirikiana na Makampuni mengine kwa makubaliano maalum katika miradi hii ya maridhiano. Kwa hiyo, aina zote ambazo amezitaja ndio serikali ambayo imezitumia.

**Nam. 42**

**Kuongezeka kwa Maradhi Mbali Mbali**

**Mhe. Panya Ali Abdalla -** Aliuliza:-

Tunaipongeza Wizara ya Afya kwa huduma mbali mbali zinazotolewa na madaktari bingwa katika kuwahudumia wagonjwa. Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa kukijitokeza maradhi mengi na ya aina mbali mbali katika nchi yetu.

(a) Je, serikali imeliona tatizo hilo.

(b) Je, madaktari bingwa wamekuwa wakipatiwa mafunzo ya kujifunza kwa wenzao (*short course*) ili kuongeza ujuzi wao na kuweza kukabiliana na changamoto kubwa zinazojitokeza.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-**

Mhe. Spika, ahsante sana kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa tumeamka wazima wa afya na kushiriki katika Baraza lako tukufu katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara imeliona tatizo hilo na magonjwa mbali mbali yasiyo ya kuambukiza yanaonekana hivi sasa kuibuka kwa kasi. Magonjwa hayo ni pamoja na kisukari, sindikizo la damu (*pressure*) na saratani ikiwa pamoja na wimbi kubwa la ongezeko la ajali za barabarani ambazo zinaingia katika kundi hili hili la maradhi yasiyoambukiza.

Mhe. Spika, matatizo haya yanaambatana na mabadiliko ya *style* ya maisha yetu ya sasa kwa kuacha vile vyakula vya asili na pia kuacha kufanya mazoezi na kutumia vipando viendavyo kwa kasi zaidi.

(b) Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina mpango maalum wa kufanya *exchange program* ambayo ni endelevu kati ya hospitali hiyo na Vyuo Vikuu vyengine pamoja na taasisi nyegine mbali mbali ulimwenguni ikiwemo pamoha na Chuo cha *Haukeland University* cha mjini Bergen nchini Norway kwa wafanyakazi wa fani mbali mbali. Madaktari bingwa wa watoto na magonjwa ya kawaida wameshakuwa wakipatiwa mafunzo hayo na hivi sasa jumla ya wafanyakazi 15 wakiwemo madaktari bingwa na kada nyenginezo tayari wameshafaidika na mpango huo endelevu ambao unaendelea.

Kwa sasa wafanyakazi watano wa Wizara ya Afya wako nje masomoni. Aidha, nchi ambazo tuna mikataba nazo na mashirikiano kwa upande wa madaktari bingwa na kada nyenginezo, wanaopata mafunzo ya ziada ni pamoja na China, Egypt, Malawi na Tanzania Bara.

Mhe. Spika, mafunzo hayo ni endelevu na kila panapotokea dharura ya maradhi mengineyo basi pia huombewa nafasi maalum, ili wafanyakazi wetu wapatiwe mafunzo haya. Ahsante sana Mhe, Spika.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa madaktari bingwa wanakabiliwa na changamoto hizi za kupatikana wagonjwa hawa wa maradhi mbali mbali ambayo yanawatokea na wizara imeseme imejipanga katika kuwapatia madaktari hawa taaluma.

Mimi nilitaka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri je, kuna taratibu zozote ambazo pale pale ndani ya hospitali ambazo madaktari hawa wanajipangia inapotokea kesi ya mgonjwa kuwa ile kesi imekuwa ngumu, ili madaktari hawa wakaweza kukaa *as a group* na kubadilishana mawazo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kuna taratibu aina mbili ambazo zimepangwa katika hospitali pale panapotokea mgonjwa ambaye matatizo yake ni makubwa na yanashindikana. Kwanza hukaa kama *departmient* wale madaktari na pale Mnazi Mmoja kuna *department* kadhaa, nadhani tisa kama sijakosea.

Kuna *depertment* ya *surgery*, *ENT*, maradhi mbali mbali wana *departments* zao. Wapasuaji wana kitengo chao, masikio, koo na pua wana kitengo chao, upande wa *laboratory* nao pia wana kitengo chao, maradhi ya watoto wana kitengo chao, maradhi ya macho wana kitengo chao.

Sasa panapokuwa panatokea tatizo ndani ya kitengo basi madaktari bingwa pamoja na wahusika wakuu wa kitengo kile huwa wanakaa pamoja kuyatatua, lakini pale linapotokea tatizo ambapo kitengo kimoja wapo kimeshindwa na maradhi yale mfano pua, koo, masikio na yule mgonjwa akahitajika operesheni kubwa zaidi mfano wa kifua kwa sababu hivi vitu vimeungana, basi *department* hiyo ama kitengo kile huomba kukaa na vitengo vya wenzao.

Mhe. Spika, vitengo vile hukaa kwa pamoja ili kujadiliana na inaposhindikana mgonjwa yule hupelekwa moja kwa moja kwenye bodi ya madaktari ambayo ina mabingwa mbali mbali wote wako saba wale tuliokuwanao hapa Zanzibar, bodi ya daktari huamua aidha kumpeleka Tanzania Bara au nje ya nchi. Hizo ndio taratibu ambazo zinafanyika sasa hivi katika hospitali na ni taratibu ambazo zimepangwa na ile idara yenyewe ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na hivi karibuni zilitengenezwa na kubandikwa kabisa ili zijulikane miongoni mwa wafanyakazi wote na kuzungushwa. Ahsane sana Mhe. Spika.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akitoa majibu alieleza kuwa yako magonjwa sugu ikiwa ni pamoja na Kisukari, Presha na Saratani. Lakini kuna UKIMWI na Kensa na kensa hasa Pemba imeshamiri.

Je, swali la mwanzo ningetaka kujua ni sababu zipi zilizosababisha kupata maradhi haya ambayo hapo zamani ilikuwa hayatufikii.

Pili, katika jibu lake amesema kuwa maradhi haya yanatokea kutokana na watu kutokula chakula cha asili kama ilivyokuwa zamani na kufanya mazoezi, wakati zamani nchi hii ilikuwa na watu laki tatu tu, wala hakukuwa na tabia ya nchi, kulikuwa na ardhi kubwa ya kilimo na watu wakiweza kula chakula chao wenyewe. Lakini hivi sasa nchi hii ina watu hawapungui milioni moja na laki tatu sehemu kubwa imegemwa kwa maendeleo mahoteli na kadhalika, na sehemu ya kilimo watu wanajenga nyumba hawana pa kulima kiasi hicho, tunakula chakula cha kuagiza. Hiyo ni kama kutwambia kuwa kwa sababu ya chakula hiki cha kuagiza maradhi haya yatakuwa yanaendelea.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mjumbe kwa swali zuri sana alilouliza ambalo litaweza kunisaidia kutoa maelezo zaidi. Maradhi ya saratani yalikuwepo zamani lakini sio kwa wingi kama sasa. La kwanza.

Pili, yalipokuwa yanatokezea hapo zamani tulikuwa hatuna uelewa wa maradhi hayo, kwa hivyo tunaona tu kwamba mtu anaathirika anakuwa anaumwa mpaka kufikia kifo lakini hatujui yule kumbe ameathirika kwa kitu gani. Lakini sasa hivi teknolojia imeendelea tuna teknolojia ya *nuclear medicine*, kuna teknolojia hizi mashine za kisasa *CT* na *MRI* ambazo zinaweza kuona vitu vingi zaidi pamoja na *Bone scan*, vinaweza kuona vitu vingi zaidi katika mwili wa binadamu ndipo taaluma ile ya kugundua maradhi mengi zaidi nayo imetanuka.

Kwa hiyo, kwa sasa maradhi ya kensa ama saratani yamekuwa yakijulikana zaidi na yanafanyiwa *research* zaidi. Pia yanagundulika mapema zaidi hasa kwa akina mama saratani hii ya matiti wanasema tiba yake kubwa kabisa ni kugundua mapema. Kwa sababu inakuwa ni sehemu ndogo ya kinyama ambacho kinaota tiba yake ni kugundua mapema, ukigunduliwa mapema inaweza kuondoshwa mapema. Lakini pale inapochelewa kugunduliwa basi kwa kuwa zile *cells* huwa zinakua kwa kuongezeka na ile sehemu ambayo imeathirika huwa inaambukiza sehemu nyengine mpaka kufikia mapafu, kifua na kadhalika, basi mwanamke huwa anaathirika zaidi kwa saratani hii ya matiti kama haijagunduliwa mapema.

Kwa hiyo, tiba ya kwanza kabisa ya kensa ya aina yoyote ile ikiwa tezi dume, ikiwa kensa ya shingo ya kizazi, basi ni kugundua mapema na teknolojia zipo hivi sasa na zinaturuhusu, baadhi yake ziko

hapa Zanzibar baadhi yake tunashirikiana na wenzetu wa *Ocean Road* kule Dar es Salaam ambao tuna mkataba nao.

Mheshimiwa pia ameuliza sababu za maradhi haya. Sababu bado zinazungumzwa duniani hazijathibitishwa kwamba 100% hizi sababu za uhakika. Wengine wanasema sababu ni haya mambo ya kisasa tunayotumia kama vile maji yakikaa sana kwenye chupa ya plastiki halafu ile chupa imewekwa juani ikapigwa na mionzi ya jua sana, kuna *reaction* ambayo inatokea baina ya ile plastiki na ile mionzi ambayo mionzi ile huingia kwenye maji halafu maji yale yakawa yanakuwa *contaminated*. Ndio maana wale wanaouza maji wanashauriwa mara nyingi wasiweke maji yaliyokuwemo kwenye chupa kwenye jua kali. Lakini bado haijathibitishwa sababu hiyo.

Pili, wanasema ni hivi vifaa vya kisasa vinavyotumiwa *microwaves*. *Microwaves* ni teknolojia ya *rays* kali, kama kuna mtu anaweza kujaribu achukue foili siku moja hili la kawaida atie chakula mle ndani halafu aweke kwenye *microwave* ataona bomu litakaloripuka pale, ile *microwave* huripuka kama bomu kwa sababu kuna *rays* ambazo ni kali za *microwave* hutoka.

Sasa vyakula vyetu vingi huwa tunapasha moto kwa microwave, mara nyingi wataalamu wa afya wamekuwa wanasema kwamba kile chakula kikipashwa na *microwave* kisiruhusiwe zile *rays* kuingia moja kwa moja kwenye chakula lazima kifunikwe na plastiki na hiyo plastiki wakati huo huo tumekatazwa kuitumia.

Kwa hiyo, kuna mawazo mengi kwamba kensa husababishwa na mambo mengi zaidi. Lakini hakuna sababu moja kuu iliyopatikana mpaka sasa hivi inayosema maradhi haya yanasababishwa na hili, ila kuna wanaosema asilimia fulani au inawezekana kutokana na hivi, asilimia fulani inaweza kutokana na hivi.

Hizi sababu ziko nyingi sana ningeweza kuzieleza, lakini pia kuna kipeperushi ambacho Wizara ya Afya imetoa juu ya saratani na sababu zake nitajitahidi nikilete hapa kipeperushi hicho ili Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kupata taaluma hiyo.

Mwisho kabisa kuhusu upande wa vyakula vya asili. Ni kweli nakubaliana wewe Mheshimiwa hapo awali vyakula vingi vya kiasili vilikuwa vinapatikana hapa na ardhi ya kilimo ilikuwa kubwa na tunalima sehemu kubwa. *Population* imeongezeka kutoka watu laki tatu na sitini elfu miaka hiyo ya nyuma mpaka kufikia watu milioni 1.33 hivi sasa na wale wote wanahitaji makaazi na makaazi yetu bahati mbaya sana yanatanuka kwa kwenda chini hayendi juu kama wenzetu nchi zilizoendelea.

Wao makazi yao hutumia nafasi ndogo lakini watu wengi zaidi wanakaa, ukiangalia Hong Kong, Singapore, visiwa ambavyo *size* yake vimefanana kidogo na Zanzibar ingawa kule ni kudogo zaidi kuliko hapa wao huwa wanakwenda juu zaidi sisi tunatanuka.

Sasa walioweza kufanikiwa katika tatizo hilo naweza kusema ni nchini India. India kila penye makaazi au nyumba wamejitengea maeneo maalum ambayo wanaita *domestic garden*. Sasa utakuta mtu katika ile *domestic garden* anaweza kupanda vipando vingi zaidi na pale katika kile kile kibustani cha nyumbani, unaweza kupanda mazao yako ambayo wewe mwenyewe unakula sio ya kuuza. Nadhani tabia hiyo ingekuwepo na hapa kwetu Zanzibar, ingeweza kusaidia sehemu kubwa kupata chakula cha asili.

Watu wengi sasa hivi wameacha kula ndizi, muhogo, vyakula hivi vya mizizi na matunda tunakula mambo ya michele na mengineyo ambayo kama alivyosema tunaagizia zaidi kuliko kuzalisha wenyewe. Hata ukiangalia mchele huu tunaozalisha wenyewe unaozalishwa Tanzania Bara kule

Mbeya, tunaozalisha hapa Zanzibar mpunga ule ladha yake na *content* yake inakuwa tafauti na ule mchele wa kuagizia.

Kwa hiyo, nadhani serikali hapa inaweka msisitizo hata Waziri wa Kilimo na Maliasili alipokuwa anazungumza kuhusu kuzalisha chakula cha kiasili ambacho tunatumia zaidi na sisi upande wa Wizara ya Afya tunaweka msisitizo kwamba watu warudi kwenye ule wali wa mtama, mkate wa mawele na kadhalika. Ahsante Mhe. spika.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo tu lenye kipengele (a) na (b) Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa katika majibu yake alisema kwamba Zanzibar kuna madaktari saba bingwa;

(a) Ni wangapi wazalendo katika madaktari hawa saba bingwa.
(b) Madaktari hawa wamebobea zaidi katika maradhi gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nimesema madaktari saba ndio wako masomoni hivi sasa, Hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake ina madaktari 78 na hivi juzi baada ya wale madaktari waliokuwa wanasoma Chuo Kikuu cha Cuba madaktari 38 ambao wame-*graduate* nao wataungana na timu hii ya madaktari 78 kuongeza idadi ya madaktari, lakini watapelekwa sehemu mbali mbali chini ya menejimenti ya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Kwa hiyo, naomba hilo lifahamike kwamba hawa madaktari saba ndio waliokuweko masomoni.

Mhe. Spika, orodha ya madaktari pamoja na taaluma yao iko katika kitabu cha bajeti cha Wizara ya Afya iliyopita, orodha yote kwa sababu maradhi ni mengi na madaktari hawa ni wengi orodha ile ipo katika vitabu ukienda kule katika viambatanisho mwisho kabisa Waheshimiwa Wawakilishi wakiweza kufanya *reference* wataona. Ila kuna baadhi ya kada ya taaluma ambazo madaktari wake hatuna na hivi sasa tunajitahidi kada hizo madaktari wake tuwasomeshe, ili angalau yale matibabu ya mwanzo kwa sababu vifaa vyake ni ghali sana viweze kupatikana hapa hapa Zanzibar na ikishindikana basi ndipo wanapopelekwa kule *Ocean Road* na kada yenyewe ni *oncology,* hatuna *oncologist* pale Mnazi Mmoja.

Hilo naomba nikiri kabisa kwamba hatuna *oncologist*. *Oncologist* ni daktari bingwa ambaye anayeshughulikia maradhi ya saratani na madaktari hawa kwa kuwa maradhi haya yameibuka sana ni ghali na pia kusomesha kwao, yaani ile *specialization* baada ya huyu daktari wa kawaida pia nako ni ghali sana. Lakini tunashukuru sasa hivi tuna ma-*oncologists* wawili wanaosoma nje ya nchi watakapomaliza tu, tunatarajia kuanzisha kitengo maalum cha *oncology* ambacho kita-*deal* na saratani kuu aina tatu. Saratani ya matiti, saratani ya shingo ya kizazi kwa mwanamke na saratani ya tezi dume kwa wanaume. Ahsante sana.

**Nam. 43**

**Jengo la Ofisi ya Afya Pemba**

**Mhe. Marina Joel Thomas (Kny: Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa)** - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Afya Pemba inakabiliwa na tatizo la majengo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi na tatizo la makaazi ya kuwaweka wafanyakazi wake, na kwa kuwa kumekuwepo na jengo la hoteli ya Wete na jengo la hoteli ya Mkoani ambayo hayatumiki kwa sasa.

(a) Serikali katika kuhakikisha kuwa inatumia rasilimali zake ipasavyo. Je, haioni umuhimu wa kukabidhi jengo la hoteli ya Wete kwa Wizara ya Afya Pemba ili lifanyiwe ukarabati na hatimae litumike kwa ajili ya ofisi zao.

(b) Katika kutatua changamoto ya makaazi kwa wafanyakazi wa sekta ya afya. Je, serikali haioni umuhimu wa kuwakabidhi Wizara ya Afya jengo la hoteli ya Mkoani ili litumike kwa ajili ya makaazi.

(c) Serikali imeweka mikakati gani katika kukabiliana na ukosefu wa ofisi kwa wizara zake mbali mbali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu pamoja na Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali, kwamba Wizara ya Afya tayari imeliona tatizo hilo na imeyapokea mawazo hayo na tayari Wizara ya Afya kwa upande wa Pemba imeshawasiliana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kwa majengo ya hoteli hizo za Wete na Mkoani.

Mhe. Spika, katika kutatua changamoto ya makaazi na nafasi ya ofisi kwa wafanyakazi wake, wizara imejitahidi kujenga nyumba za wafanyakazi kwenye baadhi ya vituo hususan vile vituo vilivyokuwa *remote areas* (vijijini), chini ya mradi ule wa *ADB*. Hata hivyo, Sera ya Afya kwa sasa inahimiza ujenzi wa nyumba za wafanyakazi kila kwenye kituo cha afya. Kwa manitiki hiyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi na Jamii zetu kuelekeza hivi sasa kujenga nyumba za wafanyakazi badala ya kujenga vituo vipya vya afya.

Vituo vya afya sasa hivi vimeshakuwa vya kutosha na tayari Zanzibar inaongoza katika yale malengo ya *millennium* kuwa na vituo vya afya chini ya kilomita tatu. Malengo ya *millennium* ni chini ya kilomita tano sisi naweza kusema katika Bara la Afrika nzima tunaongoza na kuwa na vituo chini ya kilomita tatu.

Thamani ya nyumba ya wafanyakazi wa vituo vya afya ni sawa na thamani ya kituo cha afya chenyewe. Kwani umuhimu hapo baada ya kujenga kituo cha afya huwa kwa wafanyakazi, panapokuwa hakuna makaazi au nyumba za wafanyakazi kwa vile vituo vya afya kile kituo nacho pia hupungua thamani kwa sababu hukosa wale wafanyakazi.
Kwa hiyo, pakiwa na makaazi mazuri ya wafanyakazi basi wale wanaokizunguka kituo kile cha afya huwa wanaweza kupata huduma za afya katika jamii masaa 24. Kwa sababu yule daktari ama *nurse*, ama muuguzi wa aina yoyote au kada yoyote nyegine anaweza kwenda kugongewa mlango hata ikiwa usiku wa manane kuamshwa na kuja kituoni pale kuhudumiwa kuliko wale wafanyakazi wa afya wakiwa wanakaa nje ya eneo lile.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge waelekeze jitihada zao zaidi sasa hivi sio kwenye vituo vya afya, ukijenga kituo cha afya na ikijenga na nyumba ya makaadhi ya afya thamani yake ni sawa na naamini kwa wananchi pia ni sawa.

Pia sera ya afya ya jamii pamoja na sera kuu ya afya inasisitiza sana mashirikiano kati ya vituo vya afya na kamati za afya za shehia ili vituo hivyo vionekane zaidi ni vyao wao jamii hatupendi sana mfano kule

kwa Mhe. Salum Abdallah Hamad kituo cha Mtambwe hatupendi sana kionekane kituo cha Wizara ya Afya tunataka kionekanae zaidi kwamba ni kituo cha shehia ua jamii inayozunguka pale Mtambwe na ndio maana tunashirikiana sana na Kamati ya Shehia na naweza kusema kuwa kuna baadhi ya Waheshimiwa. Sitaki niwataje, sasa hivi lakini ikibidi kuwataja nitakuja kuwataja wanaongoza kwa hilo kwamba viyuo vya afya ni *partnership* ni ubia kati ya Wizara ya Afya, waheshimiwa husika na jamii ya pale kupitia Kamati za Shehia, na vituo hivyo vyote ukiviangalia ndivyo vinavyoongoza kutoa huduma na kutoa mashirikiano, na vinavyoongoza pia kwa kuwa na dawa za kutosha pale, panapotokea mapungufu yoyote ili kusaidia jamii. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alisema Wabunge na Wawakilishi wajikite katika kujenga nyumba za wafanyakazi kuliko vituo vya afya. Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri imefanyika tathmini halisi ya mahitaji halisi za nyumba za wafanyakazi zinazohitajika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nashukuru kwanza kwa suala zuri aliloliuliza. Tathmini imefanyika na tathmini hiyo ilifanyika wakati *ADB* ilipokuwa inajenga nyumba za wafanyakazi na tathmini ya mapungufu ama upungufu uliokuwepo vituo vyote vya afya viliokuwepo Unguja na Pemba ni 142. Nimebahatika kuvitembelea nusu tu bado nusu maana ni vingi sana na *inshaallah* kila muda utakapoendelea nadhani nitakamilisha kutembelea vyote ili nipate kuvijua.

Kwa hiyo, ni vituo 142, katika vituo hivi mapungufu hasa katika vile vituo vinavyotoa huduma pana zaidi *PATCU* na *PATCU+,* vimeonekana ni vituo 42 ndio vyenye upungufu wa maakazi wafanyakazi wa afya. Mara nyingi hupata tabu sana kituo kimoja nilichokitembelea kiko Tazari pale, wafanyakazi bahati nzuri wamesaidiwa na ile kamati ya shehia wao wenyewe jamii wamejitolea vyumba ambapo wale wafanyakazi wanakaa kwa kodi ndogo kuchangia. Lakini hapo mwanzo walikuwa wanapata tabu sana kutoka kule eneo la Nungwi kuja mpaka mjini.

Kwa kujibu jibu lako ni vituo 42 ambavyo vimeonekana vina tatizo moja moja kwa makaazi kwa ya wafanyakazi na wale wafanyakazi wengi huwa wanatokea maeneo ya mbali sio wa pale pale. Kwa hiyo, tunasisitiza sana hata kwa wale ma- *orderly* tuwaajiri ndani ya jamii zilizokuwa zinawazunguka ili iwe karibu mtu na anakaa kwake, anaweza kwenda kuitwa na kuja kuhudumia.

Kituo ambacho kimefanya vizuri sana ni kituo cha Kijini Matemwe kwa sababu wafanyakazi wake ni jamii ya pale pale, yaani hicho kituo naweza kusema kuwa ndicho kinachoongoza kujihisi cha jamii yenyewe ni kituo cha Kijini Matemwe. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, katika swala lako mama ulisema kuwa ulizungumza na Katibu wa Fedha.

(a) Je, ni jibu gani alililokupa kuhusu kadhia hiyo.
(b) Uliwataka Wabunge na Wawakilishi waweze kusaidia katika ujenzi huu wa nyumba za madokta. Je, huoni iko haja kuwambia Waziri wa Fedha akatuongezea fedha za mfuko wa jimbo baada ya mfuko tuliokuwa nao sasa hivi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:**

(a) Mhe. Spika, jibu tulilopata kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha bado linashughulikiwa kwa sababu zile *properties* ziko katika ile Idara ya Mitaji ya Umma. Kwa hiyo, bado wanaendelea natumai Mheshimiwa ananisikiliza na mara tu baada ya uhakiki wao ndani tunatarajia tutapata jibu, lakini kwa kuuliza suala hili pia ni changamoto ya kufatilia kwa karibu zaidi ili tupate jibu mapema iwezekanavyo na bahati nzuriMhe. Waziri wa Fedha yumo humu humu ndani kwa hiyo na yeye analisikia.

(b) Kuhusu fedha za Mfuko wa Jimbo hata mimi kwa kuwa ninalo jimbo la Kiembesamaki, naomba niungane mkono na wewe kulipigia debe hilo na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha yuko humu ndani na amesikia na hii *hansard* pia imeandika naamini atakuwa na jibu bora kuliko mimi zaidi, na itakapofikia wakati mzuri muafaka umetuna basi naamini mfuko wa jimbo huo utaongezeka. Ahsante sana Mhe Spika.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, la kwanza ombi la Mhe. Makame Mshimba kwa niaba ya Wawakilishi hatua za kuongeza fedha katika mfuko wa jimbo naomba niseme kama ifuatavyo:-

(1) Ningeliwaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kushirikiana kusaidiana katika kufanya mapato na kuwahimiza walipa kodi na walipe kodi kama inavyotakiwa.

(2) Nataka niseme tu kwamba mapato ya serikali ni kodi za wananchi. Pale Wizara ya Fedha inapoleta maombi kwa Waheshimiwa Wajumbe ya kutaka tuanzeshe kodi fulani au tuongeze kodi fulani kwa faida yote sote nadhani wasiwe wakaidi, tukubaliene ili tuwe na kodi muafaka na hatimae mapato yetu yatakapoongezeka ndio faida ya kuongeza mfuko wa jimbo itakapojitokeza. Tutakumbuka Mhe. Spika, Wawakilishi wetu hawakuwa na mfuko wa jimbo, mfuko wa jimbo tumeuanza kwa milioni nadhani kumi sasa, hivi mfuko wa jimbo uko milioni kumi na tano. Nia yetu kusiwe na tafauti kubwa sana ya wao na Wabunge.

Nitaomba sana tushirikiane katika kukusanya kodi kwa sababu kuna wengine tunapokusanya kodi wanakuja wanatwambia eeeh, kuna wengine tunaomba hapa Barazani tuongeze kodi wao wanakuwa ni wakali katika kuongeza kodi, nchi yetu hii itajengwa kwa kodi za wananchi. Kwa hivyo, naomba tushirikiane na hatimae tutakubaliana kuongeza mfuko wa jimbo.

Kuhusu hoteli za Wete kuzigeuza kuwa ni Afisi za Wizara. Mhe. Spika, wazo letu serikalini bado zile ziendelee kuwa ni hoteli na sasa hivi wameshajitokeza wawekezaji wanazitaka kuzikarabati na waendelee kuzifanya hoteli. Lakini kama nilivyokuwa nikisema awali kwamba tuna mpango wa serikali kujenga mawizara na maofisi kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba na tumeshaanza na hili litatekelezwa kikamilifu, pale tutakaposhirikiana katika kukusanya kodi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa majibu hayo muafaka. Tunaendelea.

**Nam. 49**

**Ukiukwaji wa Sheria za Ujenzi Mji Mkongwe**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Sheria za Uhifadhi Mji Mkongwe wa Zanzibar zimeweka kikomo mwisho wa idadi za ghorofa kwa majengo yanayojengwa au kukarabatiwa kuwa ghorofa tatu. Hivi karibuni tumeshuhudia majengo ya zaidi ya ghorofa tatu yakijengwa katika mji huo.

(a) Wizara kazi yake kusimamia sheria au kuvunja sheria kutokana na ujenzi huo kufanyika na viongozi dhamana wanashuhudia.

(b) Kwa nini wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji wanaruhusiwa kujenga zaidi ya ghorofa tatu na wananchi wanyonje wakikatazwa na sheria hiyo hiyo, kitendo hicho si cha ubaguzi wakati Katiba ya Zanzibar inasema binaadamu wote ni sawa mbele ya sheria.

(c) Kufanyika kwa vitendo hivyo bila ya viongozi dhamana kuchukua hatua tunajenga misingi ya Utawala Bora au tunabomoa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara kazi yake ni kusimamia Sheria na sio kuvunja Sheria.

(b) Mhe. Spika, kinachozingatiwa katika kutoa ruhusa ya kuwa na ghorofa mbili au tatu ni yafuatayo:-

(i) Kwenye kiwanja ambacho jengo lilianguka na kumbukumbu zipo za jengo liloanguka, Mamlaka ya Mji Mkongwe inafuata kumbukumbu hiyo katika kuamua idadi ya ghorofa ya nyumba mpya inayotaka kujengwa.

(ii) Kwenye kiwanja ambacho kumbukumbu za idadi ya ghorofa za jengo lililoanguka hazipo, Mamlaka inatumia kigezo cha idadi ya ghorofa za nyumba za jirani katika kuamua.

*(iii)* Ikitokezea nyumba za jirani urefu wa ghorofa zake ni mkubwa kulingana na jengo jipya, jengo jipya linaweza kuwa na ongezeko la idadi ya ghorofa bila ya kuipita urefu nyumba ya jirani, kwa kulinda urefu wa majengo ya eneo hilo.

(iv) Mamlaka ya Mji Mkongwe imepewa fursa ya kuruhusu ongezeko la nyumba kwenda juu kwa ujenzi wa sehemu ya kupumzikia kwa mujibu wa taratibu za uhifadhi.

(v) Mamlaka ya Mji Mkongwe inazingatia maombi ya kila muombaji bila ya kuzingatia nafasi au hali yake, Sheria ndiyo inayoongoza katika kutoa maamuzi

(c) Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe inazingatia maombi ya kila muombaji, sawa, bila ya kuzingatia nafasi au hali yake, Sheria hiyo inayoongoza katika kutoa maamuzi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya wala kiwango kama ZBS kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar sheria namba 1 ya mwaka 2011, vile vile nimuombe radhi Mhe. Naibu Waziri kwa kulidanganya Baraza hili. Namuombe radhi na mara yangu ya mwanzo kusema hivyo.

(a) Mhe. Spika, mimi nimezaliwa shamba nimekuwa shamba, nimesoma shamba na hivi sasa naishi mjini. Mhe. Naibu Waziri uko tayari kufatana mimi na wewe kukuonesha maeno ambayo yalikuwa wazi wamejengwa ghorofa tatu nne na tano, maeneo ya wazi kabisa hakuna nyumba hata iliyoanguka. Uko tayari kufatana na mimi kwenda kuonesha maeneo ambayo yako wazi yamejengwa ghora tatu, nne na tano ukiwa na watendani wako pamoja na Mkurugenzi wako na kama ikithibitika je, wengine utawaruhusu naomba *hansard* ziekwe sawa, utawaruhusu bila kutuletea ubaguzi.

(b) Serikali inakuwaje kitu cha mwanzo kati ya mchoro na ramani kipi kinchokuja mwanzo, baadae kuwaruhusu na mie watendaji wakuu wa serikali mupo, kitendo

hiki si kuvunja Katiba ya Zanzibar na mupo tayari kujiuzulu baada ya kushindwa kusimamia majukumu yenu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Kwanza nataka nirejee jibu kwamba kama nilivyoeleza hapo awali kwamba utaratibu wa kufanya shughuli zetu kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe unaenda kisheria. Hili niseme kwamba niko tayari kufatana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kufanya ukaguzi wa hayo maeneo ambayo yamejengwa na tukishafanya ukaguzi tutaangalia hali halisi ya wale mambo wenyewe yalivyo katika maeneo hayo yaliyojengwa nyumba hizo.

(a) Kwa hiyo, mimi sikatai, hata juzi nilipojibu suala la aina hii kwamba nilimwambia kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, niko tayari kutoka mimi na yeye kwenda kuangalia hayo maeneo na sikukataa yeye mwenyewe tu akiwa tayari basi tutaenda kuangalia mimi pamoja na watendaji wangu, hilo mimi niko tayari.

(b) Mhe. Spika, naomba kidogo alirejee.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Serikali inakuwaje kuruhusu ujenzi kufanyika hasa ukizingatia mchoro na ramani kipi kinachokuja mwanzo. Baadae kutokuruhusu ujenzi ule kusimama njiani haoni kuwa anavunja Katiba ya Zanzibar. Na kuweka sawa swala la mwanzo. Pindipo akithibitika ataruhusu kumruhusu mjenzi huyo kuendelea na ghorofa zake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, michoro ndiyo inayotangulia na hatimaye ramani ambayo hutafutwa na yule mjenzi hufuatana na michoro hiyo. Kwa hiyo mara zote sisi tupo katika kuliangalia suala hili kwa umakini bila ya kuwa na matatizo yoyote. Kwa hiyo ningemuomba Mhe. Mwakilishi katika suala hili la michoro na ujenzi na kuruhusiwa katika ujenzi unaofanyika katika maeneo tunayoyatoa, basi awe makini katika kuzingatia. Lakini ninachomthibitishia kwamba michoro hufuatana na ramani zake.

**UTARATIBU**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kifungu cha 37, Waziri au mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa ana wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Swali langu kwamba hakuwahi kulifafanua kule mwanzo. Nilichomwambia pindipo ikithibitika kuwa maeneo hayo ni hatua gani atazichukua au na wengine atawaruhusu. Alikuwa anijibu atawaruhusu au hawaruhusu. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, naomba niongezee majibu ya Mhe. Jaku Hashim kama ifuatavyo.

Mheshimiwa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, kwamba serikali inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria inayotokana na Katibu iliyopo na haina nia yoyote ya kubagua yoyote katika eneo lolote ikiweno na sekta hii ya ujenzi. Hakuna mwenye fedha au asiyekuwa na fedha sheria ni msumeno na utaratibu lazima ufatwe.

Alichokisema Naibu Waziri hapa kwenye majibu yake alielezea vizuri sana alisema kwamba:-

Pale ambapo eneo lipo tupu ujenzi unaruhusiwa kwa ghorofa tatu. Pale ambapo nyumba za jirani zinategemea idadi ya ghorofa zilizopo ikiwa zipo ghorofa nne basi ujenzi huo unaofata utaruhusiwa kuwa wa ghorofa nne na wakati mwengine huruhusiwa kuongeza sehemu ya juu sehemu ya kunywea chai, sio ujenzi ile varanda kabisa ambapo huwekwa watu wapunge upepo na kadhalika. Kwa hivyo, kama lipo eneo na Mheshimiwa amesema yupo tayari wafuatane yeye na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wende wakaoneshane pale ambapo pamevunjwa taratibu, basi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Ni vizuri twende tuone, tuelewe kosa lipo wapi, basi hatua nyengine za kisheria zitafuata. Kwa hivyo, naomba avute subra na waende na Mheshimiwa, alichokijibu Mheshimiwa ni sahihi kabisa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku ninadhani tu...

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, alisema eneo la ardhi mwisho ghorofa tatu, ndiyo ninataka kujua arekebishe hapo, ndivyo sivyo. Ni hapo tu Mhe. Spika, kwa faida ya wananchi na hiki chombo kipo kwa niaba ya wananchi.

**Mhe. Spika:** Yaani hukusikia vipi, hebu tukufahamu vizuri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, alisema hapo Mhe. Waziri alipokuwa akijibu kama eneo tupu ni ghorofa tatu na arekebishe ndivyo sivyo basi, ni dogo tu ni hilo.

Alipokuwa akijibu alisema eneo la wazi anaruhusu ghorofa tatu.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa umelifahamu hili swali lake, haya hebu tuje.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naomba kufanya ufafanuzi. Nimemueleza hivi, pale ambapo ni kiwanja kitupu ambapo hapana majengo mengine, utaratibu uliowekwa ni ghorofa tatu. *(Makofi)*

Pale ambapo pana ujenzi mwengine katika maeneo hayo ya Mji Mkongwe, ikiwa kuna jengo la zaidi ya ghorofa tatu basi hilo hilo jengo jipya linaruhusiwa litalingana na hizo ghorofa zilizopo, kama ni nne watapewa ruhusa hiyo.

Na vile vile ipo ruhusa ya kuwa na ile sehemu ya juu ya kupungia upepo au sehemu ya kunywia chai ambayo hiyo haitakuwa na vyumba. Huo ndiyo utaratibu. Sasa kama Mhe. Jaku analo eneo limejengwa kinyume na utaratibu huo akatuoneshe ili taratibu za kisheria zichukuliwe. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Hija Hassan Hija swali la nyongeza.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, ninakushukuru na nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais kwa majibu mazuri sana.

Mhe. Spika, kwa hakika inaonekana wazi kwamba nadharia na ukweli kwamba Mji Mkongwe wa Zanzibar, masuala ya urithi yamepitwa na wakati na hata kama utalazimisha kwamba tuendelee kukubaliana na matakwa ya *UNESCO*, lakini hali halisi ya mahitaji ya Zanzibar kwa Mji Mkongwe kwa vyo vyote vile tayari inalazimisha kwamba mji upanuke na twende juu.

Hata hivyo kuna watu wanang'ang'ania kwamba tuendelee kukubaliana na matakwa yale ya kuhifadhi mji kwa kisingizio kwamba *UNESCO* ndiyo wanatusaidia.

Mhe. Spika, hali hiyo imevinza hata jengo la Wizara ya Afya ambalo wahisani wametufadhili kwenda kujenga ghorofa tatu, kwa misingi hiyo ya kukubaliana na matakwa ya kuhifadhi mji, jengo hili limeazimiwa kujengwa ghorofa mbili kiasi kiasi ambacho Wizara ya Afya imekula hasara kiasi kikubwa.

Swali langu Mhe. Spika, hivyo Serikali ione sasa haja kwamba tufanye tathmini upya ya mafanikio yanayopatikana ya kuhifadhi Mji Mkongwe chini ya *UNESCO* na mahitaji ya mji wetu kwa ajili ya kupanua mji ili maendeleo ya kisasa yaweze kupatikana, duniani miji yote ambayo inajenga hasa nchi za visiwa kama Singapore na nchi nyengine, hakuna utaratibu wa kujenga nyumba hizi za kuelekea, nyumba za train kuelekea Bububu mpaka Nungwi, watu wanaelekea juu kwa ajili kuhifadhi nchi.

Hivyo, Serikali haioni haja ya kufanya tathmini Mhe. Spika, ili tukajenga majumba ya kisasa ya ghorofa tatu, nne, kumi na kwenda juu badala ya kupata msaada wa *UNESCO* ambao hatuuoni.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli upo umuhimu mkubwa wa kufanya tathmini ya hali halisi ya Mji Mkongwe na tayari Serikali inafanya jambo hilo. Mengi yanayojitokeza Mhe. Spika, katika suala la Mji Mkongwe yametokana na sheria yetu wenyewe inayosimamia Mji Mkongwe.

Kutokana na sheria hiyo, tumeona kweli yapo mapungufu ambayo yanakwaza maendeleo katika Mji Mkongwe. Hivyo, sasa Serikali inachukua hatua ya kurekebisha sheria hiyo ili pia kuhifadhi Mji wetu Mkongwe, tuhifadhi taratibu za *UNESCO* lakini wakati huo huo tuendeleze Mji wetu Mkongwe uwe na haiba inayolingana na wakati pia wa leo.

Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante sana. Nimemsikiliza kwa makini sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na majibu yake mazuri sana.

Mhe. Spika, ametamka rasmi kuwa Mji Mkongwe unaruhusika kujengwa ghorofa tatu, wakati hapo hapo tuna sheria tumeitunga hapa hapa na msimamizi ni yeye kuwa sheria ni mwisho kujengwa nyumba ghorofa mbili.

a) Je, haoni hiyo ni kuipinga mwenyewe sheria yake aliyoisimamia.

b) Duniani hivi sasa kuna nchi nyingi zinahifadhi ya Mji Mkongwe na Mji Mkongwe huo huo unasimamiwa na *UNESCO*. Mhe. Waziri haoni kutamka wazi na hivi sasa vyombo vyote vya mitandao unatusikia sisi katika Baraza lako kubwa sana la kutunga sheria, kuwa leo anatamka kupinga sheria ambayo *UNESCO* inayosimamia ya kuwa Mji Mkongwe, hifadhi nzuri na isiharibiwe kwa kutamka suala hilo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ningeomba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk asikilize kwa makini na masikio yake ayafungue vizuri wakati tunapojibu maswali. Hatujasema hata kidogo kwamba tuna nia ya kwenda kinyume na *UNESCO*. Tunachokisema *UNESCO* wanaitizama sheria yetu ambayo sisi tumeipeleka kule na sheria hiyo kwa njia moja au nyengine inakwaza kwa sehemu nyengine maendeleo ya Mji Mkongwe.

Nia yetu ni kuendelea kuhifadhi Mji Mkongwe lakini pia kuangalia hali halisi ilivyo leo. Kwa hivyo tunafanya marekebisho katika sheria yetu, ili tuhifadhi Mji Mkongwe, bado mji wetu uhifadhike lakini yale mambo muhimu ambayo yangehitaji kufanywa kwa maendeleo ya wakati sasa nayo pia yaweze kufanyika.

b) Suala la ujenzi wa ghorofa tatu Mhe. Spika, limo ndani ya hiyo sheria yetu ya Mji Mkongwe inaruhusu kujenga ghorofa tatu na pale ambapo ujenzi wa Mji Mkongwe upo zaidi ya ghorofa tatu basi wahusika hutizama utaratibu huo kutokana na ile hali halisi ya Mji Mkongwe na kuruhusu idadi hiyo inayolingana na inayotokana na majenzi ya zamani. Mhe. Spika, naomba hilo lieleweke wazi kabisa hatuna nia ya kuvunja utaratibu wa *UNESCO*, lakini tuna nia ya kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru nyote. Kabla ya kuendelea Waheshimiwa Wajumbe ninaona na leo kuna vijana vijana pale juu ambao ndiyo wageni wetu wa leo na wageni hawa ni kundi la pili la wanafunzi wa Chuo cha *Institute of Continuing and Professional Studies*. Jumla yao wapo 50 na wanaongozwa na mwalimu wao Mr. Gilbert Patrick.

Naomba wote wasimame pamoja na mwalimu wao. *(Makofi)*

Karibuni sana. Sasa tunaendelea

## HOJA ZA KAMATI

### Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya 2014/2015

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea lakini ninataka tukumbuke kwamba tu kidogo tupo nyuma ya ratiba, shughuli zetu bado zimebakia nyingi. Muda ambao tulipanga tumalize shughuli ni tarehe 31/03/2015 lakini bado kuna kamati mbili hatujaweza kufanya kazi pamoja na shughuli nyengine mbili kubwa ambazo nazo pia hatujazigusa.

Kwa hivyo tunapaswa kabisa kujaribu kujitahidi ili tusije tukaongeza muda mkubwa kwa shughuli za mkutano huu. Mkutano huu ulikuwa na wiki tatu barabara ambazo zinaashia tarehe 31/03/2015, lakini inaonekana bado shughuli itakuwa hazikumalizika.

Kwa hivyo tuendelee na majadiliano lakini tuelewe kwamba muda wetu umebakia mfupi sana. Naomba nimkaribishe Mhe. Salim Abdalla Hamad baadae Mhe. Jaku Hashim Ayoub wakati Mhe. Hassan Hamad Omar anajitayarisha.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kutoa maelezo yangu kidogo kuhusu utekelezaji wa Wizara tatu husika kutokana na maagizo ya kamati.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati moja kwa moja nianze na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Spika, ukurasa wa tatu wa kabrasha hili la utekelezaji tulilopewa kuna kuna agizo nambari 10 la kamati ambalo linaeleza kuwa haja kubwa ya kutilia mkazo zaidi suala la kuongeza ununuzi wa mizani za kisasa za upimaji wa karafuu, ili kuondoa malalamiko yanayohusiana na upimaji wa karafuu.

Utekelezaji ni kwa sentesi ambayo haikukamilika, inayosema kuwa, "Juhudi zinaendelea kuchukuliwa kuongeza mizani hizo ambazo ni mizani kumi na nne". Hapo hakumaliza lakini ninafikiri pengine ni kuwa zimeshanunuliwa.

Mimi Mhe. Spika, kwa hili ninapenda kueleza kuwa utaratibu uliopo katika ununuzi wa karafuu hauridhishi. Mara nyingi ununuzi wa karafuu uliokuwa haufiki kilo huwa unakatwa, hatujapatapo mtu kupata au karafuu zako uzito wake mfano ni kilo ishirini na robo, hii robo mara nyingi huwa haitajwi.

Ninaamini pamoja na uchakavu wa mizani zetu tulizonazo si kweli kuwa kiwango hiki hakioneshi. Lakini imani yangu ni ukorofi tu wa wanunuzi ndiyo wanaosababisha hivyo. Hawajipunji wenyewe wakasema ni kilo mia kasorobo, lakini siku zote robo inaondoka.

Sasa Mhe. Spika, kwa mujibu wa karafuu bei yake zilivyo na ninampongeza Mhe. Waziri kwa hilo, ni kuwa tunanunua pishi yenye kilo moja na nusu kwa jumla ya shilingi ishirini na mbili elfu na mia tano. Ni sawa na kusema kuwa kilo moja hakipungui shilingi elfu kumi na tano.

Sasa robo ya kumi na tano ni shilingi elfu tatu na kidogo. Kwa hivyo kila unapokata robo kilo, unakata shilingi elfu tatu na kidogo za Kitanzania. Kama watakuja watu kiasi mia moja, ushawakata hazipungui shilingi laki tatu kwa siku moja. Kama kwa mwezi mmoja itakuwa haipungui shilingi milioni tisa. Kwa hivyo kwa hesabu hii utaona kuwa wakulima wanadhulumika sana.

Hivyo wito wangu Mhe. Spika, ni kuwa tujitahidi na hasa huu mfumo uliopo kuwa inapofika wakati wa zao la karafuu wanachukuliwa watu tu kutoka mawizara mbali mbali; wakiwemo Wizara inayohusika kwenda kununua. Tunawaona wanapoingia kabla ya kununununua na tunaona wanavyokuwa baada ya msimu.

Mhe. Spika, wito wangu kwa Mhe. Waziri ni kuwa atoe somo maalum kwa wanunuzi, waone kuwa hata asilimia moja juu ya nane ya haki ya mwenye mali anayeuza, kwa hivyo ipatikane. Tunajua hata Mwenyezi Mungu amelani sana, anasema, *"Waylun lilmuttafifina, aladhina alannasi yastawfuna..."*. Sitaki niendelee hiyo ni aya ya *Qur-an* na yeye ni Al-hajj anaajiri watu, ijapokuwa Mwenyezi Mungu amekataa kuhukumu kosa la mtu mwengine, lakini ninaamini dhima yote ni yake kwa sababu anajua, anajua pesa anazozitoa, anajua kima cha karafuu zinazorejeshwa na zile zilizozidi. Ninasikia kama ni kweli wamenipa wale walionunua kwamba na hii mimi naomba pamoja na juhudi ya kununua hizo mizani mpya za kisasa, lakini vipimo viwe uangalifu sana.

Jengine Mhe. Spika, ni agizo la kumi na mbili ukurasa huu wa tatu wa Wizara hii ni kuwa wakati wa *ZSTC* lipo katika mageuzi makubwa. Hoteli ya Makonyo nayo inahitaji mageuzi kwa kufanyiwa ukarabati mkubwa, kuimarishwa kwa usafi na kuweka utaratibu mzuri wa zamu za wafanyakazi.

Aidha, Wizara itoe ushirikiano mkubwa katika kufanikisha uimarishaji wa hoteli hiyo. Kaeleza Mhe. Waziri kuwa tayari ukumbi wa mkutano umeshafanyiwa marekebisho makubwa, lakini kasema *ZSTC* itaifanyia ukarabati Hoteli ya Makonyo ili nayo iweze kuwa katika hali nzuri. Ni lini hakuweka.

Ninamuomba Mhe. Waziri kwa kupitia kwako ni bora atupe tarehe na kujitazama hali yake aliyonayo na uwezo wake, ni lini ile hoteli itafanyiwa marekebisho makubwa kwa sababu ni hoteli ambayo inatumika na watu wazito wazito, hata Waheshimiwa Wawakilishi hapa wanapokuwepo Pemba kwa kamati wanaitumia hoteli hiyo.

Mhe. Spika, agizo la 18 la Wizara hii hii ambalo linaeleza kuwa linapotokea mchukuzi kufariki, shirika ni vizuri kuwa mstari wa mbele katika kutoa mchango wake hususan wa kifedha kwa ajili ya mazishi ya wafiwa marehemu.

Utekelezaji wake ameeleza kuwa suala hili limezingatiwa katika sheria ya maendeleo ya karafuu na kanuni zake. Limeangaliwa vipi hatujui kuwa limekubaliwa au halijakubaliwa. Kwa uzito wa suala hili tunajua wachukuzi wanafanya kazi mpaka wengine ni vizee na wanapokufa wanakufa ni maskini, kwa

sababu kazi zao ndiyo hivyo na malipo siyo ya kuridhisha kiasi hicho. Kwa hivyo uangalizi huu uwe wa kukubalika na huu ushauri wa kamati.

Mhe. Spika, nikiendelea ukurasa wa nne wa Wizara hii katika shughuli za utekelezaji ni kuwa, agizo la 16 la kamati linasema kuwa, "Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama izidishe juhudi za kudhibiti magendo ya karafuu, kwa kuwa karibu zaidi na wananchi, ili kuweza kutambua mbinu mbali mbali zinazotumiwa na wajanja wanaosafirisha kwa njia za magendo na kuchukua hatua zinazofaa.

Maelekezo ni kuwa Kikosi Kazi Maalum kilichoundwa na Serikali kinaendelea katika kazi hii ya ulinzi wa karafuu. Mimi Mhe. Spika, kwa hili kwanza nimpongeze Mhe. Waziri amewahurumia sana wakulima wa karafuu kwa kuwapa asilimia 80 ya bei ya dunia kuwa ni mali yao katika manunuzi.

Karafuu hizi naona zinafanyiwa mipango ambayo pamoja na juhudi hiyo ya Wizara, lakini kuna fedha nyingi inatumika pasi na ulazima na kwa maana hiyo faida iliyokusudiwa kufika kwenye Wizara ndiyo kwenye Serikali haipatikani.

Kuna *task force* ukiangalia Mhe. Spika, ni ya viongozi wenye ngazi kubwa kubwa Serikalini, wenye mishahara mikubwa mikubwa na wengine hata huo uwezo wa ufuatiliaji hawana, ijapokuwa uwezo wa kimaarifa wanao kutokana na umri wao. Hawa wanatembea wanatumia mafuta mengi linatoa shirika, inatoa Wizara. Lakini wakati kuna Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), kina kazi kinafanya vile vile hizo karafuu.

Halafu kuna askari wanakaa barabarani na magongo yao ya kuzuwia barabara, wanafanyakazi hiyo ya karafuu. Inakuwa wizara inalipa watu wengi katika fani mbali mbali wanaoshughulikia karafuu hizo, bila ya kuwa na ulazima na inapoteza pesa nyingi sana.

Mhe. Spika, mimi ningeomba wizara ishauriane vizuri na serikali iweke utaratibu mwingine, kuliko kuajiri watu bila ya ulazima na kupoteza pesa nyingi kwa sababu ya karafuu.

Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba kwanza hii *task force*, kama itakuwa iwekwe kwa wakati ambao wanalipwa pesa nyingi sana na serikali ni wakubwa tu, basi isingelazimika wizara kuwalipa tena kwa shughuli za karafuu wafanyakazi wa karafuu, kwani kazi mbadala kwa malipo yao ya wizarani.

Halafu na kikosi maalum cha kuzuwia magendo kiimarishwe kiweze kufanya kazi zake ipasavyo.

La mwisho suala la kuweka vizuizi barabarani wakati karafuu zinachumwa, ati zisipitishwe na kusafirishwa kwa magendo. Hili suala anafanyiwa binadamu. Mimi naona ni kama kuwaambia wananchi tafuteni njia nyengine ya kupita. Hakuna mtu yeyote atakayekuwa na karafuu zake akapitisha, wakati anajua barabarani kuna maaskari akazipitisha huko, badala yake ningeomba kama itawezekana na kama kutakuwa na watu waaminifu, kuwe na kamati maalum vijijini katika yale maeneo yanayochumwa karafuu, wawe wanafanyakazi hizo.

Pili, zikishachumwa karafuu yale magongo yanaondoka, kamati inavunjwa na kazi inabakia pale pale. Hii haina maana kuwa ikivunjwa hii kazi ndio karafuu hazisafirishwi kwa magendo. Mimi ningeomba ulinzi wa karafuu uwe ni wakudumu na yale mambo ambayo sio ya lazima yaondolewe, ili utaratibu unaofaa ambao utasababisha na hili shirika lenyewe kujiona kuwa linafaidika, baada ya kujitahidi na kuwahurumia wakulima inapatikana.

Jengine Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati naomba kidogo niende katika Wizara ya Kilimo na Maliasili. Hii nitaanza na hoja ya kamati, hoja namba moja ambayo inasema, pamoja na uhaba wa fedha uliopo,

kuna haja ya wizara kuangalia kwa karibu wafanyakazi wake kwa kuwapatia maslahi yao yanayostahiki, japokuwa kwa awamu kila inapoingizwa fedha, ili kujenga ari na mori ya kazi kwa wafanyakazi wake.

Majibu yameelezwa kuwa fedha hiyo imelipwa kwa wafanyakazi, naamini huko hakuna tatizo, wanalipwa fedha zao kama kawaida. Lakini kuna hawa wafanyakazi ambao wamekuwa na likizo, waliolipwa ni wafanyakazi 101 tu na wafanyakazi 250 ambao wamelipwa kwa masaa baada ya kazi. Naamini kutokana na maelekezo ya kamati, watu wa aina hii wako wengi ambao bado hawajalipwa.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, kwa kupitia kwako namuomba Mhe. Waziri afanye kila inavyowezekana, watu hawa ambao wanadai pesa zao za likizo na hawa wanaodai pesa za baada ya kazi walipwe kama wafanyakazi wa kawaida, ili tatizo hili liweze kuondoka. Hii ni haki yao wasihangaike.

Mhe. Spika, tukienda katika agizo namba mbili, ambalo hili linaeleza kuwa katika kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi, wizara pamoja na wizara inayohusika na ajira, inapaswa katika kutilia mkazo suala la uajiri wa wafanyakazi watakaojaza nafasi za wafanyakazi waliostaafu na waliofariki kabla ya kushughulikia ajira mpya.

Mhe. Spika, tumeona katika takwimu hapa utekelezaji, kuna wafanyakazi 124 wanahitajika kwa Unguja na Pemba; Unguja 72 na Pemba 52. Lakini kwa sababu ya utaalamu wakutoa shughuli zao za utekelezaji, wizara hii naipongeza imeongeza *column* ya maelezo, ambayo wamesema kwa hili kwa kuwa suala la ajira linasimamiwa na wizara nyengine, inapelekea kuchelewa kuzijaza nafasi hizo kwa wakati.

Mhe. Spika, wafanyakazi 124 kuwa ni upungufu, ina maana katika wizara kuna pengo kubwa la ufanisi katika shughuli zake za kazi na hii ni hatari. Mhe. Spika, wakati pakiwa pana pengo ni lazima lijazwe. Kwa hivyo, mimi naiomba wizara husika, wasifanye nikakata tamaa kama wizara inayohusika ya kilimo, kwa kupelekea kuchelewa kwa kuajiriwa watu hawa. Naiomba wizara ilione hili, naiomba wizara ijuwe hawa wafanyakazi wanahitaji kulitumikia taifa hili kwa faida yetu, na hii Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio wizara ambayo tunaitegemea ifanyekazi, kwa kukuza uchumi na kutusaidia sisi kupata chakula safi na bora, na kujiepusha na maradhi kama Waziri wa Afya alivyoeleza katika kipindi cha maswali na majibu. Hivyo basi, hili suala nasisitiza litiliwe mkazo sana.

Halafu Mhe. Spika, kuna suala hili la mpunga limeelekezwa kuwa wizara ihakikishe kuwa inalima kwa wakati, inatafuta mbegu bora na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Suala hili Mhe. Spika, mimi naomba nieleze kuwa tunao wataalamu wetu kweli katika Chuo cha Kilimo. Lakini Mhe. Spika, mpunga kuna mbegu tofauti. Katika sayansi kuna *generic name*, halafu na *specific name*, yaani kuna mbegu tofauti. Kama utofauti wa mbegu ulivyo na mara nyingi huenda sambamba na utofauti wa sehemu zile mbegu zinapoweza kunawiri na kuvuna mazao bora.

Tumeona hapa, kulikuwa na mbegu ile ya *nerika* ilisifiwa na Mhe. Rais kenda kaizindua, katika kuvuna mashuke makubwa na yeye alivuna na ikapandwa nchi nzima. Sasa imebakia kuwa ni historia. Huu ni mfano sahihi wa kueleza kuwa hiyo *nerika* ina sehemu maalum. Hata katika hii Zanzibar na kwenye mazingira maalum inaweza ikamea, lakini katika sehemu nyengine haiwezekani na ndiyo mbegu nyengine zilivyo.

Kwa hivyo, pamoja na kazi kubwa iliyotolewa na kamati na maelekezo ya wizara. Ushauri wangu kwa wizara ni kuwa, ihakikishe inawatumia wataalamu hawa kufanya utafiti wa kutosha, hata katika ardhi yenyewe mbolea ya kutumia, wakati wa kulima na mazingira ili mbegu tofauti ziweze kuota katika sehemu tofauti kama ilivyokuwa hapo zamani. Zamani kulikuwa na mbegu za juu, kulikuwa na mbegu za vuli na kadhalika. Kwa hivyo, naomba huu mpango ufanywe, vyenginevyo tutabakia katika njaa kila siku.

**Mhe. Spika:** Una dakika mbili.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, dakika mbili siwezi kueleza lolote. Kwa heshima kubwa na taadhima naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Nimkaribishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mdomo uliteleza anafuata Mhe. Hamza Hassan Juma, na sio Mhe. Hassan Hamad na baada ya hapo Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, mwanzo kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nakupumua pumzi zake alizoniazima, ambapo sijui wakati gani atazihitaji. Ni neema kubwa, niendelee kumshukuru kwa kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo. Ingekuwa sio haki ukaliona jambo ovu kama hukutumia mdomo wako, au mkono wako au kulichukia. Mimi nitakuwa sio mchangiaji sana kwa eneo hili, lakini kuna kitengo kilichonitia huruma sana na kamati yako Mhe. Spika, ilikaribia kulia hapo Kizimbani, Kitengo cha Kusarifu Mazao.

Mhe. Spika, kitengo hiki ni muhimu kupita kiasi, ni jambo la kusikitisha! Kuna jengo limejengwa kwa gharama kubwa na Kampuni ya Korea, baadaye sijui walikatisha na kinachohitajika ni pesa kidogo sana, shilingi milioni 361. Wizara ya Kilimo na Maliasili imefika pahali hakuna jawabu inayopatikana. Lakini kamati baada ya kukaa na kushauriana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Ahmed Nassor Mazrui, yuko tayari kukipokea kiwanda hiki kwa maslahi ya Wazanzibari. Yupo hapa na kama nasema sivyo anaweza kunikosoa na kamati ilikuwa shahidi.

Mhe. Spika, kama Wizara ya Kilimo na Maliasili imefika pahali mmeshindwa likabidhini jengo hili, haina uwezo, bajeti mnayopata ni ndogo. Kitengo hiki cha kusarifu mazao ni muhimu. Leo kuna vifaa viko bandarini vimeshaanza kuoza, kamati imekwenda kushuhudia. Huu ni mwaka wa tatu, Mhe. Hija Hassan au wa pili?

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mwaka wa pili.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mwaka wa pili karibu, kwa shilingi milioni 361, huu u- *serious* uko wapi hapa. Kitengo cha kusarifu mazao, kazi iliyobaki shilingi milioni 361 kwa mujibu wa ripoti ya kamati Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi niwaombe ndugu zangu Wizara ya Kilimo na Maliasili kama imefika pahali limeshakushindeni jukumu sio aibu, mkabidhini Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko yuko tayari kupokea. Imekuwa kama kile chombo cha *DNA* kilichokuja, masikio mbali na miguu mbali, mpaka leo kiko pale Maruhubi, ni kitu cha kusikitisha!

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha aangalie umuhimu wa kuvipatia fedha hivi vitengo. Kuna sekta nyengine muhimu huwezi kuzilaza kama afya na kilimo. Leo mnasema 'kilimo kwanza', hali yenyewe ndio hii. Kitengo hiki kutokana na umuhimu wake kamati inaiomba serikali kufanya juhudi za makusudi zitakazowezesha kazi za wizara hii kupata fedha za kutosha, lakini imeingiziwa asilimia 15 tutafanya nini.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kwenye Wizara ya Fedha. Kwanza niiombe tena Wizara ya Fedha na hili suala tumeliomba kwenye kamati na kurudia tena hapa, sio mbaya. Niwashukuru Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wake wa Benki ya Watu wa Zanzibar *PBZ*, kwa kazi nzuri wanayofanya na sisi sote ni mashahidi. Benki hii imetoka katika mdomo wa chewa huo ndio ukweli ulivyo, kwa anayefahamu kwamba ilikuwa na wakati mgumu tayari ilikuwa imeshataka kubinafsishwa sio kufilisiwa, kutokana na uwezo wake kuwa mdogo. Mimi mmoja ni shahidi nimeliona. Lakini kwa hekima na busara za Rais

mtaafu Dk. Karume nimshukuru kwa hili kulisimamia tukafika hapa, haki yake apewe. Amelisimamia na baada ya kufahamishwa akazuwia zoezi hili kufanyika, Dk. Abeid Aman Karume.

Benki hii ikasimamishwa ikaanza kujiendesha katika wakati mgumu, kama mtu anapokuwa *ICU* mfano wake. Vijana wamefanyakazi kubwa sana PBZ niwashukuruni sana kwa hali mliyofikia. Leo tunashuhudia matawi mangapi wanayo PBZ. Leo Wizara ya Fedha inaomba kwao kitu kidogo tu pesa za kodi bilioni 5, waambie angalau watie nusu, unaweza kuomba 5 ukapata 2. Sheikh Omar Yussuf Mzee hii benki ukiniuliza mimi historia yake naijua kiasi fulani.

Leo Zantel kuna faida mliyoipata, leo kuomba kodi ile kuwaachia wale benki na sio kwamba mnawagaia, kuomba kuongeza mtaji wao kutokana na mashindano ya benki yaliyokuweko mengi Zanzibar. Sadaka huanza nyumbani, taa huwashi nje unawasha ndani ya nyumba. Wafikirieni wameomba bilioni 5 watilieni japo bilioni 2.5 kuwapa moyo. Benki ilikuwa na wakati mgumu, na mabenki tunaona ushindani mkubwa sasa hivi.

Mhe. Spika, kuna CRDB, FBME, KCB, NBC, na nyengine zinakuja, kina Amana, BARCLAYS, ushindani utakwenda wapi, kutoka bilioni 5 walizoomba wapeni japo nusu, hamjapoteza hapa, mmewekeza na sio kwamba hawatolipa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kwenye maslahi ya wafanyakazi wa Bima. Hapa kidogo Mwanasheria itabidi unifahamishe kama kuna sheria tatu au nne. Hawa wafanyakazi wamelia kilio kikubwa kwenye kamati kuhusu Bima, maslahi yao wengine wamepewa na wengine kutokupewa. Kwa nini wengine wapewe maslahi vitengo vyengine na wao wasipewe Bima, wamekosa nini, tuna sheria ngapi hapa.

Itabidi niseme tu ikiwa PBZ maslahi yako juu hawa wamekosa nini Bima. Suala hili Mhe. Waziri wa Fedha nitahitaji jawabu, kuhusu maslahi ya wafanyakazi hawa yamekuwa ni muda mrefu, hakuna utendaji na wamefanyakazi. Sasa hivi wana ofisi Mbeya, Arusha na Mwanza, sivyo walivyokuwa mwanzo. Mtoto akizaliwa hendi mbio, hutambaa akasota, akapata mguu mmoja akasimama akakamata kiambaza mpaka akachanganya.

Mhe. Spika, huu sio ubinadamu wafikirieni hawa watu, hapa ndio pahala pa kusema sio marikiti wala Makunduchi wala Muyuni, hichi ndio chombo cha kuwasemea wananchi, maslahi yao angalieni, tunawalea au tunawabinya. Leo KIRA wamewabana, wanataka kuanzisha Kitengo cha Bima ya Kiislamu TIRA wamewakamata. Asilimia 98 ya Wazanzibari ni Waislamu, wanaogopa wengine kukata Bima zilizokuwa zina mashaka ndani yao, kwa nini tuzuiwe Zanzibar kama ni nchi. Leo wanatafuta maslahi ya Bima ya Kiislamu na wako tayari watu kujitokeza kwa suala hili, leo wamezuiwa na TIRA. TIRA nani. Maendeleo hayaji namna hii, tufike pahali tukamate.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kwenye Mfuko wa Barabara ambayo imesimamiwa na kamati hii. Mhe. Waziri kitendo kilichofanywa sijui kama bandari au manispaa cha makalbi yaliyowekwa pale, mzigo ule mpaka barabara kubomoka halafu pesa mmewachangisha wananchi Malindi, makalbi yale alipokuja Rais yameondoshwa na leo yamerudishwa, mzigo umekuwa mzito.

Mhe. Magufuli alizuwia kuna boti kupelekwa Mwanza kutokana na huo ufinyu wa barabara, leo tunazuia barabara wenyewe kwa makusudi. Sisi wenyewe tunauona uchafu umewekwa pale, baadaye alipokuja Rais umeondolewa baada ya kuondoka Rais tukarudisha tena, ni kitu cha kusikitisha.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije na kilio cha Wazanzibari hasa wafanyabiashara kuhusu *TRA*. Mhe. Waziri hapa mimi nafikiri hamko *serious*, mzigo uliotoka Kenya, Rwanda, Burundi ukaingia Bandari ya Dar es Salaam hauna mashaka. Lakini mzigo ukitoka Zanzibar ukiingia Bandariya Dar es Salaam, utafikiri umeleta unga, kwa nini tumefikia hatua hii. Wengine wasibanwe, lakini mzigo ukitoka Unguja ukiingia

Dar es Salaam utaoza na utausamehe. Ni vigezo gani vinatumika Tanzania moja, TRA moja na *formula* moja. Tunafanya nini, tunalea au tunasaidia.

Mhe. Spika, kitu cha kusikitisha siku zote katika kero za Muungano suala hili halipatikani *formula* yake. Zanzibar ni ndogo, biashara ziende kule na wengi wao wanatufuata sisi baada ya kuwa vigezo. Zamani ulikuwa unaonekana kama ni muhalifu, baada ya PBZ kuanzishwa, *formula* ya kuwa na dola na wao wakaridhi kutoka kwetu, sio kitu cha kuridhisha hata kidogo Mhe. Waziri. Ni lini hasa mtakuwa tayari kuifuatilia hasa kero hii.

Mhe. Spika, mimi nimeshazungumza Bungeni sio mara ya kwanza, sio mara ya pili wala mara ya tatu kwa suala hili, nikasema Zanzibar inajulikama kama nchi ya kigeni mzigo ukiuleta hapa unalipa ushuru, ukienda Bara unalipa mara mbili zaidi, imekuwa ni nchi ya kigeni tunakiuka hati ya makubaliano ya Muungano.

Mhe. Spika, baada ya hayo nije jengine kuhusu mambo leseni. Kodi zimekuwa nyingi, pamoja na kuwa tunakusanya kodi maslahi madogo, lakini kuku anataga yai moja ukamlazimishe atage mayai manne kwa wakati mmoja utamuuwa, tutakosa sote. Halmashauri inataka kodi, Manispaa inataka kodi, ZRB inataka kodi na TRA inataka kodi, hao wafanyabiashara watakuwa vipi, tunawasaidia nini sisi. Ndio tunataka kodi kwa maslahi ya wananchi vile vile, lakini hizi kodi zimekuwa nyingi mngetafuta *formula* kitengo kikawa kimoja tu.

Mhe. Spika, baada yapo nimshukuru mfanyabiashara mmoja wa Pemba baada ya kujaribu kuziweka bidhaa za mchele, unga wa ngano na sukari kuwa katika kiwango kimoja kwa Unguja na Pemba, ambapo ilikuwa ni tofauti kubwa. Niendelee kumshukuru huyu mfanyabiashara, nafikiri mheshimiwa Haroun unasema unamjua huyu mtu ni mtu ambaye amepiga kazi kujitolea, mzigo wake anashusha Mombasa na kila kontena sasa hivi karibu ni dola mia nne au mia tano, faida yake hizi dola mia nne ndio anazo-*survive* nazo.

Soko lilikuwa tofauti sana Unguja na Pemba. Kwa sababu gani mzigo umeshushwa hapa usafirishwe ulipiwe ni gharama nyengine yeye Mwenyezi Mungu kamjaalia ana meli yake, anachukua mzigo kule anaupeleka Pemba. Soko karibu kaliweka sawa kwa sawa, ni mtu wa kupigiwa mfano na kumshukuru mtu huyu, kuweka sawa sawa soko la Unguja na Pemba, ni mtu wa kumfikiria kila wakati huyu.

Bidhaa za Pemba zilikuwa ziko juu tofauti na Unguja kwa mzigo wowote unaoshushwa hapa Unguja, yeye katafuta njia nyengine mzigo anashusha Mombasa anachana kontena anapeleka pale kwa meli yake, faida yake ni ile dola mia nne kushusha lile kontenda.

Mhe. Spika, baada ya hapo nataka niendelee kuwashukuru watendaji wawili na Mhe. Waziri wa Fedha, hawa watu tuwatizame na ni hazina kubwa huko mbele tunakokwenda. Kamishna wa TRA ndugu yangu au jamaa yangu Mcha huyu jamaa mswalihina, mchamungu simsifu kwa kuwa mimi ni mfanyabiashara na watu wengine wote wanajua; huyu jamaa vigezo alivyoweka pale bila ya ubaguzi wowote. Anaviweka kwenye *level* moja bila ya kumbagua mutu, sio kama namsifia kwa sababu ni mfanya biashara mimi, sifanyi biashara wakuleta mchele wala sukari, wala unga wa ngano. Mimi sijaenda kwake hata siku moja nikamwambia nina kontena hii wala hii, lakini jamaa kazi anayofanya ya kupigiwa mfano, bila ya ubaguzi wowote.

Vile vile nimshukuru Kamishna wa ZRB naye Abdu ni mtu ambae naweza kusema tokea kidole cha gumba mpaka kwenye kichwa hiki, nasema ni mweupe, ni Kamishna anayefanya kazi bila ya kutumia vigezo vya ubaguzi wa aina yoyote, ni msikivu na mtulivu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi nafikiri nimalizie kuhusu kiwanda cha kusanifu mazao, Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo amefika pahali tayari limeshinda jukumu hili, naomba ulikabidhi kwa Wizara ya Biashara, wako tayari kuokoa hali ilivyo. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura naendelea tena kukushukuru kunipa nafasi hii kwa mara nyengine na mimi nikaweza kuchangia ripoti hizi ambazo Kamati ya Fedha na Uchumi na Kilimo na Biashara ambazo wametuwasilishia hapa.

Mhe. Spika, mimi kwanza kabla sijaanza kuingia kwenye mchango wangu, nilikuwa kwanza nataka nitoe ombi na nilikuwa nataka nitoe ombi kwetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Wawakilishi wenzangu hasa Wenyeviti, lakini vile vile nataka nitoe ombi kwa Serikali kwa sabu tunafanya kazi kwa pamoja kwamba sasa hivi tunachangia ripoti za utekelezaji wa Wizara hizi katika bajeti hii ya mwisho 2014/2015.

Tumekuwa tukipokea ripoti za kila mwaka kwa hivyo naomba tukishamaliza kikao hiki kikao kinachokuja ni kikao cha bajeti, kwa hivyo basi ni busara tukafanya samari ya kazi ambayo tumeifanya kwa kipindi cha miaka mitano hii ya Serikali ya awamu ya saba, na kwa sababu tulikuwa tukipata mafunzo mbali mbali Mhe. Spika, mafunzo ambayo ulikuwa ukitupa wewe kupitia ufadhili wa *UNDP* ambao tunawashukuru.

Kwamba katika mipango hii ya MKUZA kuna mipango ya muda mfupi, kuna mipango wa muda wa kati na kuna mipango ya muda mrefu, basi angalau tunapokuja sasa wakati wa bajeti ukiacha ile bajeti ya kawaida lakini angalau tuwe na *summary.*K Wizara mafanikio ndani ya miaka mitano, hili tutapata kupima kwamba je, Serikali ya Awamu ya saba ilikumbana na Changamoto gani na iliweza kuzitatua vipi. Mimi nafikiri hiyo itaweza kusaidia.

Pia na sisi kama Baraza la Wawakilishi kupitia Wenyeviti wenzangu unajua Mhe. Spika, unapokuwa kiongozi kwa sababu uongozi kwanza ni taaluma, uongozi sio unaamka tu unakuwa kiongozi. Kuna elimu ya uongozi, na katika taaluma ya uongozi kuna mambo lazima unatakiwa uyawekee mikakati. Je, na sisi kama Baraza la Wawakilishi Wajumbe tulikuwa tuna mpango gani katika mkakati wa kuhakikisha tunaisimamia Serikali wanaweza kuondoa moja, mbili, tatu nne na lipi tumeweza kufanikiwa na lipi hatukuweza kufanikiwa tukifanya hivyo Mhe. Spika, tutakuwa tumejitendea haki na tutakuwa tumeitendea haki Serikali yetu na wananchi ambao walituchagua.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika kuchangia hii ripoti. Kwanza nataka nianze kuwapongeza Mawaziri, nawapongeza wote lakini kuna baadhi nitawatawapongeza zaidi. Nataka nimpongeze sana Mhe. Mahamoud Thabit Kombo Naibu Waziri wa Afya, nataka nimpongeze sana kwa sababu gani, sasa hivi tunavyojibiwa masuala ya Wizara ya Afya tunaridhika kabisa, maana yake sio tunajibiwa tunaelimishwa. Sasa Mhe. Mahamoud Thabit Kombo usigeuke mgema endelea na kazi yako nzuri.

Kwa sababu katika kipindi kifupi ulipokabidhiwa Unaibu Waziri wa Afya hakuna suala unaloulizwa ukawa hulijui, kwa sababu unafuatilia na hiyo ndio kazi inavyotakiwa. Kwa kweli leo nakushukuru sana ulipokuwa unajibu masuala hasa katika vituo vya wananchi, hukutaka tu kuvitaja lakini naamini ungetaja.

Kwa nini nikafurahi kwamba kwa muda mrefu tulikuwa tukipiga kelele kwamba hivi vituo tuviendeshe kwa mashirikiano baina ya sisi wananchi na Serikali. Tunashkuru kumbe kilio umekisikia sasa hivi, wewe ndio unahimiza kwamba Wawakilishi. Sasa vile vituo tusivifanye kwamba vya Serikali. Kwanza tumevijenga wenywe, halafu vinaendeshwa na Serikali leo. Inafikia pahala mpaka *selling board;* moja kuna vituo vya afya humu vilikuwa *selling board* moja linageuka mpaka rangi ya *broun.* Waheshimiwa kwa sababu waliomba kwamba hivi ni vituo vya afya kazi yake Serikali.

Kwa hivyo hilo Mheshimiwa, kwa kweli nakupongeza sana na nimepata taarifa zako kutoka hospitali yetu ya Kwamtipura, tunaomba tu kile kilemba kidogo, sasa hivi kina matatizo na kimeanza kurishai rishai kidogo na unajua jengo letu lile zuri ambalo tunashukuru sana Serikali imelipokea vizuri. Tunafanya kazi sasa hivi kama vile tulivyokuwa tunatarajia.

Kwa hivyo tunaushukuru msaada ambao umeletwa na Serikali kupitia ahadi ya Rais kutumalizia ghorofa ya pili katika jengo letu la hospitali ya Kwamtipura, na tunashukuru sasa hivi inafanya kazi vizuri huduma ya macho nadhani pale kwa kweli inafanya kazi vizuri sana, na nampongeza sana Dk. Slim mpelekeeni salam zetu kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika hospitali yetu ya Kwamtipura.

Mhe. Spika, nilisema nitamtaja Mhe. Mahamoud Thabit Kombo kwa sababu leo alinigusa lakini na Mawaziri wengine wote nawashukuru kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Jengine Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwanza kwa kuwa msikivu ingawa sio yote tunayomwambia anayasikia na anayafanya, lakini mengi anayafanya na kwa kweli tunamshukuru na ndio maana hata Mhe. Rais safari hii katika hotuba yake ya sherehe za Mapinduzi, mimi kwa bahati nilikuwa sipo nipo safarini lakini nilikuwa nafuatilia, aliisifu sana Serikali yake na akawasifu sana watendaji wake hasa wa bodi ya mapato, ZRB na TRA, kwa kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato, hata na mimi kwa kweli nawapongeza. Lakini hili tujiulize ilitokana na nini ndio maana pale mwanzo nikasema hebu tufanyeni tathmini ya miaka mitano.

Mhe. Spika, utakumbuka tulikuwa wakali sana hapa mwanzo tunai-*shout* Serikali mianya ya mapato, uvujaji wa mapato wengine mkawa mnatuona wabaya, lakini matunda yake ndio hayo. Sasa hivi Serikali inatwambia mapato yameongezeka sio maradufu mara dufu katika Serikali hii ya awamu ya saba. Na ukiangalia huoni vianzio vipya ni vile vile lakini mashimo yale yamezibwa, kwa hivyo ina maana sasa hivi fedha zinaingia katika mfuko mkuu wa Serikali, lakini katika ile tathmini niliyosema hebu tujifanyie tathmini sisi kama Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, leo Mheshimiwa Makame Mshimba hapa alimchokoza kidogo Mhe. Waziri wa Fedha na akachokozeka, akaambiwa basi kama tushirikiane na Wizara ya Afya katika kujenga nyumba za Madaktari, basi utuongezee mfuko wa jimbo. Mhe. Waziri karudisha tena changamoto ile akasema tujitahidi kuibua vianzio vipya vya mapato, lakini vile tuhakikishe kwamba tunaisimamia vizuri Serikali ili hivyo vianzio vipya vya mapato viweze kuingia ndani ya mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa kazi hii tumeifanya na katika kianzio kipya kimoja cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kianzio hicho ambacho kilikuwa hakipo tulikigusa sisi kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa fedha ni kodi ya *Income Tax* ambayo wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar; kianzio kile kilikuwepo lakini kilikuwa hakikusanywi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tulimbana Mhe. Waziri wa fedha na tunamshukuru kipindi kile akawasiliana na Mheshimiwa Lugimbo Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, katika Waziri aliyetusaidia, Waziri wa fedha mmoja aliyetusaidia Marehemu Mheshimiwa Mgimwa. Namuomba Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo amueke katika makazi ambayo yamekuwa mazuri zaidi.

Kwa sababu alitusaidia na anaendelea kutusaidia kitu alichotufanyia Mhe. Mgimwa ni sadakatul jaalia, alikaa na Mhe. Waziri wa Fedha akamwambia wawakilishi wanalalamika. Kuna mapato ambayo kuna huduma wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wanaofanya kazi Zanzibar, wanapatiwa huduma zile lakini huduma zile hawazilipii.

Kwa hivyo Serikali inapata hasara kuwahudumikia wao huduma zile hawazilipii, alipomwambia huduma gani akamwambia kodi ya *Income Tax,* akamwambia basi kuanzia mwaka ujao mtachukua. Ingawa

mwaka ule wa mwanzo sheria kidogo kule ilikuwa na matatizo hatukuzipata, lakini kuanzia mwaka ujao tumezipata nafikiri sasa hivi kwa mwaka tunapata karibu bilioni kumi na saba.

Kwa hivyo Mhe. Spika, bajeti yako ya Baraza la Wawakilishi tumeitafuta sisi wenyewe Baraza la Wawakilishi bajeti yetu kwa mwaka mzima haizidi bilioni kumi na nne, sisi tumeokoa kianzio kipya tumeibua kianzio kipya bilioni 17, kwa hivyo bado Mhe. Waziri wa Fedha nakuomba katika zile fedha za mfuko wa jimbo katika kile kianzio kipya tulichokitafuta kina bilioni tatu zimebakia.

Sasa zile tunaomba uangalie uwezekano wa kutuongezea katika mfuko wa jimbo kabla hatujaanzisha vianzio vipya. Kuna kitu ambacho kilikuwa hakipo tumekileta, kimeingia ndani ya Serikali kwa hivyo basi kama mwaka huu unasema utatupa milioni 15, lakini mimi nakumbuka kama ilikuwa ishirini vile tulivyokubaliana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ishirini bwana na hili ukija naomba utujibu vizuri mwaka huu hatujachukua, lakini tukichukua tunategemea ishirini sio kumi na tano.

Kwa hivyo Mheshimiwa nilikuwa nakukumbusha tu kwamba katika huo mfuko wa Serikali unapojaa basi sehemu ya mchango wetu wa mawazo kuweza kusaidia, na kwa sababu umerejesha nidhamu kwa watendaji ambao wanashughulikia masuala ya fedha, kuona kwamba hizi fedha sio za kwao, ni fedha za wananchi. Zilikuwa zinahitaji kwenda katika mfuko wa Serikali.

Mhe. Spika, katika mafanikio na kuna changamoto, kwa bahati safari hii katika *speech* yangu sikuwepo lakini nilitaka niliingize hili katika mafaniko ya Baraza la Wawakilishi. Moja hilo kuibua vianzio vipya, Serikali imepata mapato, lakini moja katika changamoto ambalo Baraza la Wawakilishi tumefeli na sijui kama tutakubali tufeli kushindwa kuanzisha sheria ya utawala wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, ninakuomba tena nakuomba sana kupitia kwa Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Muhammed Aboud Mohammed Serikali kwa nia njema imeamua kuchukua ile sheria yetu, sheria ile ambayo katiba ya Zanzibar imelitaka Baraza la Wawakilishi haikuitaka Serikali. Katiba imelitaka Baraza la Wawakilishi kutunga sheria yake ya utawala wa Baraza, tulifanya kazi hiyo tumejitahidi Mhe. Spika, umetupeleka kwenda kujifunza nchi tofauti. Tumeleta sheria mwanana haina doa, Serikali mpaka leo sheria yetu imeikalia.

Nitakuomba Mhe. Spika, nilileta barua nitaikumbushia barua yangu ya kuwasilisha hati mezani; Sheria kusomwa kwa mara ya kwanza, Sheria ya utawala wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu sheria ipo tayari tumeshaipeleka *government press* kuchapwa nikapigwa *stop,* naomba sasa hivi Serikali muondoe mkono wenu, sheria ije kwa sababu sheria na nyinyi inawahusu vile vile. Kwa sababu sote humu ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tukiweza kuipitisha sheria ile Mhe. Spika, tutakuwa Serikali ya awamu ya saba imeweza kusimamia utawala. Mpaka sasa hivi utumishi uliokuwepo bado utumishi wote wa Serikali hatuna utumishi wa Baraza la Wawakilishi. Hii ni kasoro moja katika masuala ya demokrasia Mheshimwa. Wewe ndio unayetupeleka katika mikutano ya CPA na hayo ndio mafunzo ambayo tunayapata.

Kwa hivyo changamoto hii naomba Waheshimiwa wawakilishi wenzangu pamoja na Serikali twende nayo, lakini tuhakikishe kwamba kabla ya kumaliza mwaka huu, kabla ya kuvunja Baraza hili la Wawakilishi basi tuwe na sheria yetu ya utawala angalau tuweze kufanya kazi zetu vizuri zaidi kuliko tunavyofanya kazi sasa hivi.

**Mhe. Spika:** Una dakika tano.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Haya Mhe. Spika, nataka niende kwenye ripoti, humu kuna suala ambalo mwenzangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub amelizungumza. Kwa kweli na mimi nasikitika sana kuona kwamba na katika hii ripoti ya kamati kwenye kitabu, ipo ukurasa wa 74 kile kituo cha *food process*,

yaani kituo cha usarifu wa mazao. Mhe. Spika, humo tunamokwenda Duniani moja katika maendeleo ya nchi zile na ukiangalia nchi zile zina vianzio vyengine vya kiuchumi, lakini moja ni usarifu wa mazao, leo tuna mazao hapa inafikia pahala yanaoza.

Leo tunategemea kwamba mradi huu kama ungeliweza kufanikiwa wananchi wetu wangeliweza kupata taaluma, wangalipata elimu nzuri wakaweza angalau kusarifu haya mazao angalau wakaweza kuuza katika kiwango, sasa hivi tunaambiwa tuingie katika soko la AGOWA, utaliingia vipi wakati huwezi kusarifu mazao.

Leo milioni 390 hizi, mimi nafikiri Serikali katika eneo moja katika *programm* ya kuondoa umasikini eneo moja la Serikali ikilikwamua hili na mimi sikufurahia sentensi ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, aliyosema Mheshimiwa Mazrui yuko tayari kukichukua kile serikali inafanya kazi kwa pamoja huwezi kusema Wizara ya Kilimo wao wasamehe wachukue Wizara ya biashara ina maana hii Serikali tumegawana mapande. Haiwezekani Wizara ya kilimo ni jukumu lenu kama fedha zinatoka huko huko mfuko mkuu wa Serikali, fedha zinatoka Serikalini, haiwezekani leo Wizara ya Biashara ikaweza kukamilisha mradi huu, Wizara ya Kilimo basi na Waziri ajiuzulu kashindwa kazi. Kama Waziri mmoja anataka kukamilisha kazi ile Waziri mwengine akashindwa, ina maana yule Waziri kashindwa hawezi kazi. Tunataka mradi huu Mheshimiwa ukamilike, ili Serikali yetu iweze kupata nafasi na wananchi wetu waweze kupata hiyo taaluma.

Lakini chengine Mhe. Spika, sitaki kwenda sana kwenye ripoti kwa kwasababu ni mambo ambayo ripoti imeshaeleza Mhe. Waziri atakuja kujibu, lakini nilikuwa nataka kuna baadhi ya mambo ambayo Serikali bado haijatufanyia vizuri Mheshimiwa mradi wa ZUSP.

Mradi wa ZUSP tunajua uko Baraza la Manispaa lakini hizi fedha zinazimamiwa na miradi yake inasimamiwa na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa katika muathirika mmoja wa ukosefu wa kufeli kwa mradi wa ZUSP ni Jimbo langu la Kwamtipura, mradi huu wa ZUSP ambao ungelitegemea kutengeneza mitaro mpaka leo mwaka wa tatu, mwaka wa tatu naambiwa tunaitisha tenda tenda miaka mitatu haijaitishwa Mheshimiwa hebu Mhe. Waziri wa Fedha aje aniambie. Waziri wa Tawala za Mikoa hayupo hapa, lakini Mhe. Waziri wa Fedha aje aniambie kwa sababu mradi huu uko Tawala za Mikoa lakini fedha zinatoka Wizara ya Fedha.

Kwanza mradi huu kwa taarifa ambazo sio rasmi nazifanyia kazi na Kamati ya Katiba na Sheria wafuatilie hata hayo magari mliyoyanunua hayana kiwango, ni ubadhirifu huo. Kamati ya Katiba na Sheria ndiyo wanayoshuhulikia hizi Tawala za Mikoa, wafuatilia ununuzi wa magari ya huu mradi wa ZUSP *failure* na mradi wenyewe mpaka leo umekwama, kila siku *tender, tender*. Nataka nije niambiwe mtaro wa Kwamtimpura tenda inatoka lini?

Mhe. Spika, kwa kumalizia dakika zangu hizo tano ulizosema nilikuwa nataka niwapongeze Benki ya watu wa Zanzibar. Mimi naiambia Serikali katika benki ambayo inasaidia uchumi wa Zanzibar sasa hivi, inasaidia mpaka wajasiri amali, inasaidia wafanya biashara ni Benki ya watu wa Zanzibar. Serikali kuipa mtaji kuweza ku-*compete*. Mimi naishukuru sana Serikali ya awamu ya Sita, benki ilikuwa inakufa ilikuwa mahututi ICU, Karume akasema mtafufuka. Karume akasema kila anayedaiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar alipe. Walilipa na Benki ikapata uhai na serikali ikaongeza mtaji. Leo Benki inataka mtaji wa kuweza ku - *compete*, tunashindwa serikali.

Mhe. Spika, hapa tulitaka ianzishwe Benki ya wanawake, ikapigwa dana dana hapa, Maalim Harouna sijui yuko wapi, kesho, keshokutwa tutaanzisha mpaka leo hakuna. Basi angalau hii Benki ya Watu wa Zanzibar inayosaidia wafanyabiashara wetu tuijali. Sasa hivi unaambiwa katika Benki ambayo ukitaka kwenda kukopa pesa za kigeni hukosi ni Benki ya watu wa Zanzibar, leo wanataka kushinda kibiashara.

Hebu naomba Mhe. Waziri wa Fedha fanya jitihada zako muwape hiyo afueni, lakini nawapongeza sana kwa kuweza kusikia kilio cha wananchi wa Kwamtipura baada ya kupata maafa ya upepo na leo Mhe. Sheha wangu amenipigia simu akanambia tayari wananchi wangu wamepata mabati na miti, basi naomba Mwenyezi Mungu awape moyo zaidi wa kuweza kutusaidia katika mambo haya. Mengine Mhe. Spika, nitakuja malizia katika wizara nyengine. Nakushukuru asante.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naanza kwa kumtaja na kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia neema zake tukiwa hai na wazima, tukiendelea na shughuli zetu hapa.

Nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu katika mjadala huu wa hoja ya ripoti ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara, lakini pia ripoti za utekelezaji za Wizara tatu ambazo zinasimamiwa na Kamati hizi.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza kwanza Mawaziri wote watatu waliowasilisha ripoti zao. Kwa sababu ripoti angalau zilikuwa zinamaelezo ya kina katika yale ambayo yalikuwa yameagizwa, nalipongeza hilo. Kuna baadhi ya maeneo machache ambayo labda maelezo yaliyotolewa na maoni tofauti nitayagusia hapa katika dakika hizi ambazo nitazitumia.

Mhe. Spika, kabla ya kwenda na yale maeneo ambayo labda nilikuwa nataka ama kuwa na maoni tofauti au kutaka maelezo zaidi katika ripoti hizi. Mimi nataka nianze kwa kupongeza sana Benki ya Watu wa Zanzibar katika Wizara ya Fedha. Kama kuna mfano wa kuonesha kwamba vijana wetu wakiaminiwa wanaweza wakafanya kazi nzuri basi ni PBZ. Naitaja PBZ kwa sababu ndio imetajwa hapa, lakini kwa jumla ningesema kwamba ziko taasisi kadhaa Zanzibar ambazo wamekabidhiwa vijana hasa na wameonesha mfano kabisa katika kuingiza mbinu za kisasa za *management* ambazo zimeleta mabadiliko makubwa sana.

Mimi nitakuwa sitendi haki Mhe. Spika, katika kulizungumza kama sitatambua mchango mkubwa wa Rais Mstaafu Dokta Amani Abeid Karume, katika taasisi mbili ambazo nakumbuka katika hotuba yake ya kuja kuliaga Baraza hapa mwezi Agosti mwaka 2010, aligusia katika mafanikio yake. Suala la kuifufua na kuirudisha katika nafasi yake Benki ya Watu wa Zanzibar. Lakini pia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa maana ya (ZSSF).

Mhe. Spika, naomba Waziri mimi kidogo pamoja na maagizo yaliyokuwa yametolewa na Kamati katika ukurasa wa 89 na mtizamo wao kuhusu suala la ZSSF. Mimi naomba kidogo Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja anisaidie. Tunaendelea kufatilia na hapa sio mahali pake, kwani *style* tunayoitaka... lakini bajeti haipo mbali. Tunaomba aje atusaidie zaidi. Kwa sababu kuna taarifa kwamba yale mafanikio yaliyofikiwa mpaka wakati Dokta Karume anaondoka ZSSF sasa yanaelekea kuingia katika mashaka kwa sababu ya namna ya uwekezaji wa ZSSF inavyojiingiza nao.

Mhe. Spika, miradi mingi ambayo imetokana na serikali yenyewe ambayo imeingiza, kwanza gharama zake zimekuwa ni *inflated* kwa maana ya kukuzwa sana, kuliko thamani halisi. Lakini na namna ya kazi yenyewe ambayo inafanyika kwamba haielekei kwamba kutakuwa na mrajesho wa maana wa faida wa ZSSF.

Tukitambua Mhe. Spika, kwamba ZSSF si fedha za serikali ni fedha za wafanyakazi masikini waliochangia kwa ajili ya kujiwekea hatima yao.

Kwa hiyo nilikuwa nasema tulitegemea mfuko huu usaidie kunyanyua maisha ya wafanyakazi wetu na sio uwe tija kwa wanaosimamia. Hili naligusa tu kwa sababu limegusiwa katika ukurasa wa 89, ripoti ya Kamati. Lakini nasema kamati ilipaswa iende kina kikubwa zaidi kuangalia haya masuala ya uwekezaji wa ZSSF kwamba hayajaturejesha yale mafanikio yaliyokuwa yamepigwa mpaka Dokta Karume

anaondoka, tukaja kurejea kule kule tulipokuwa tumetoka. Nilikuwa naomba sana hili Mheshimiwa. Kama nilivyosema hapa tunapita tu, mkutano bajeti tukijaaliwa.

Mhe. Spika, la pili ambalo nilikuwa nataka nilitolee kauli ni ukurasa wa 81 wa ripoti kuhusiana na mradi wa ZUSP, ambao nashukuru kaka angu Mhe. Hamza Hassan punde hivi kamaliza kuugusia.

Nikwambie neno moja Mhe. Spika, mimi nilikuwa napanga kuleta hoja binafsi kuhusu mradi wa ZUSP na nikitaka tuunde Kamati Teule kwenda kuuchunguza mradi wa ZUSP. Lakini mambo mawili yananirejesha nyuma. Moja, wakati kwamba uhai wa Baraza hili hauna muda mrefu tena kabla ya uchaguzi tukijaaliwa, tuna kikao kimoja cha bajeti ambacho kwa kawaida mambo kama haya hayapewi nafasi sana.

Pili nikarudi nyuma kwamba zile ripoti za Kamati Teule zilizofanyiwa kazi huko nyuma hazijaleta tija yoyote kubwa ya maana. Kwa hiyo nikasema tutakuwa tunaponda fedha kwenda kufanya uchunguzi ambao pangine yakirudi yanakuwa yayo kwa yayo. Lakini hiyo haina maana kwamba tusichangie katika idara kama hiyo.

Mhe. Spika, mimi nautilia mashaka mradi mzima na utekelezaji wake kwamba huu kama, miradi mengine mikubwa imenufaisha watu fulani badala ya kunufaisha wananchi wa Zanzibar waliokuwa wanyonge. Bahati mbaya nimelisema hili wengine limewakera sana. Kwamba mradi huu Mhe. Spika, tumeutumia kumfanya Rais atoe ahadi kubwa kubwa mara tu baada ya kuingia madarakani. Leo wananchi baada ya miaka mitano hawaoni chochote.

Mhe. Hamza Hassan Juma, mfano mmoja hapa analalamika kuhusu jimbo lake na kila mmoja hapa kaguswa. Ile dhana nzima kwamba utaimarisha miji yetu haipo. Nilisema juzi hapa na mimi nataka kuthibitisha kwamba magari yanayoletwa hata kwa kuyatizama macho hayataki hata mtu kuwa mtaalamu, unaona kwamba hayana uwezo.

Leo Mhe. Spika, wakati natoka nyumbani nimekuta gari la manispaa hayo mapya linaweka hayo makontena yanayokusudiwa kutupiwa taka. Yale makontena ni madogo zaidi kuliko yaliyokuwepo. Wakati tumesema hapa uzalishaji wa taka unaongezeka. Lakini pengine limefanywa makusudi ili ile gari kwa sababu haina uwezo wa kuchukua lile kubwa iweze kulibeba. Sasa tunataka kufidia udhaifu wetu mahala fulani kwa kukwamisha mafanikio ambayo yalipaswa yawepo.

Mhe. Spika, nataka kutoa mfano mdogo tu. Katika paragrafu ya (iv) kwenye ukurasa wa 81. "Kazi za ujenzi za kufanywa vizimba vya taka", sitaki kusoma kwa kuokoa muda kwa sababu nina mengi ninayoyataka kuyazungumza. Lakini hapa tunaambiwa kwa makisio ya gharama ya shilingi za Kitanzania mia nane tisini na tatu milioni, laki moja kumi na tatu elfu mia sita tisini (893,113,690), ilikusudiwa kujengwa vizimba 193. Vilivyojengwa kutokana na ukosefu wa maeneo vimekuwa 80.

Mhe. Spika, najiuliza kama thamani hii ni halisi kwa hivyo vizimba vilivyokusudiwa mwanzo 193 basi maana yake kizimba kimoja gharama yake nimefanya hesabu hapa ukigawa kwa 193 ni milioni nne laki sita ishirini na saba elfu mia tano thalathini na mbili (4,627,532).

Sasa kizimba Mhe. Spika, nakuomba tena ukipata nafasi vitembelee uvione, vipo katika maeneo yetu. Hebu nambie kuna *value for money* kwamba kizimba kile ni shilingi milioni nne. Haitaki hata utaalamu kwenda kuona, fedha zimetafunwa. Mimi nimuombe sana CAG katika hili, wakafanye uchunguzi wajiridhishe kweli pale kizimba kile kilichowekwa pale, mimi tangu kinajengwa katika eneo langu nakishuhudia mpaka kinamalizika kwamba kina-*cost* milioni nne, laki sita, ishirini na saba elfu (4,627,000), hata siku moja!

Lakini hapajatolewa mchanganuo mzuri na Kamati, kama ikiwa fedha hii imetolewa kujengewa hivyo vizimba 80 kwa sababu ya kuchukua nafasi, basi hiyo maana yake ni balaa zaidi kwa sababu maana yake ni kizimba kimoja kimegharimu milioni kumi na moja, laki moja sitini na tatu elfu, mia tisa na ishirini na moja (11,163,921).

Naomba Kamati wafanye kazi lakini na CAG alifanyie kazi. Hapo Mhe. Spika, ni mfano mdogo tu. Mimi naamini katika magari hivyo hivyo, mambo mengi.

Turejee hotuba ya kwanza ya Mheshimiwa aliyozungumzia humu ndani akiwasilisha bajeti alivyouchambua mradi wa ZUSP, akatujengea fikra ya matumaini makubwa sana ambayo leo hatuyaoni. Kama tunavyosema miradi yote mikubwa kila mmoja anaekuja hapa mabilioni yametumika, lakini hakuna tija iliyofikiwa Mheshimiwa. Tunanufaisha watendaji wachache lakini sisi tumekaa hapa kazi yetu kupiga makelele kila siku hakuna linalokuwa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, pili ambalo nataka nilizungumzie, wenzangu wamepongeza na mimi napongeza suala la kukusanya mapato ambalo limetajwa katika ukurasa wa 86 wa ripoti ya Kamati kuhusiana na ZRB. Kwamba mapato yanayokusanywa yameongezeka kutoka makusanyo ya shilingi mia moja arubaini na moja bilioni (Sh 141 bilioni) mwaka 2011/2012 kufikia shilingi bilioni mia moja na sabini na saba nukta saba mbili (Sh 177.72).

Mhe. Spika, tumeambiwa hapa makadirio yamevukwa kwamba ni asilimia 103 ya makusanyo. Suala langu linarudi pale pale na nimeliuliza katika kila Kamati kama mapato yameongezeka mbona huduma haziongezeki kwa wananchi. Mbona kila wizara tunayoisimamia tukenda inalalamika kwamba OC hawaingiziwi kisawa sawa.

Narejea kusema Mheshimiwa kwamba tusidanganywe kwa kuambiwa kwamba hawa wafadhili wamezuia fedha. Fedha za OC hazitokani na fedha za wafadhili. Kwa nini leo Idara nzima inaingiziwa shilingi milioni mbili, ifanye shughuli gani Mhe. Spika, katika OC na huku tunaambiwa mapato yameongezeka. Kama yameongezeka fedha hii inakwenda wapi. Sitaki niseme inatafunwa, lakini ninachotaka kusema kwamba nataka majibu kwamba ikiwa mapato yameongezeka mbona utendaji wa serikali unarudi chini kila siku. Kisa kila anaekuja hapa anatwambia ufinyu wa bajeti, ufinyu wa bajeti, ufinyu wa bajeti. Naomba maelezo katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hapo hapo naomba maelezo kwa sababu hili suala linagusa kamati yangu kidogo. Hapa pametajwa TRA na Mhe. Hamza Hassan Juma amepongeza suala la kufanikiwa kubana hadi kupata fedha za kodi ya *pay as you earn* (PAYE) bilioni 17 kwa mwaka. Lakini vile za mwanzo tulizozipigia kelele hapa na tukasema serikali ikakubali kwamba ziingie kulipa sehemu ya deni la ZECO kwa TANESCO, kila tukenda ZECO sisi Kamati tunaambiwa kwamba hazijalipwa mpaka leo na bado TANESCO inasema inaidai. ZECO zinajumuishwa katika deni. Naomba hili Mhe. Waziri akija atwambie, kwamba hawa ndugu zetu wanaotupenda sana Watanganyika, kwa nini fedha yetu hii milioni 17, hawataki kuilipa kwa upande wa deni. Lakini wao TANESCO wanaweza kutukumbusha deni lao kwa ZECO.

Jengine Mhe. Spika, niseme wenzangu wamegusia suala la TRA ukurasa wa 87 wa ripoti, kwamba muundo wake ni kwamba Naibu Kamishna aliyekuwepo Zanzibar yupo katika ngazi ya nne katika muundo wa utawala. Mimi hili naliona ni sawa sawa na la BOT ambalo katika agizo la Kamati mwaka jana agizo namba 35 na limetolewa maelezo hapa ya Mhe. Waziri wa Fedha, kusema kwamba kuna haja kwa Benki Kuu ya Tanzania BOT kuishauri mara kwa mara Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika masuala mbali mbali ya kiuchumi ili kusaidia kuimarisha uchumi wake.

Mhe. Spika, haya maelezo mengi yemetolewa hapa na haya ambayo yamo katika ripoti ya Kamati mimi nikiyatizama naona kama tunapiga maneno tu Mhe. Spika. Katika muundo wa Muungano uliokuwepo,

ambapo Tanganyika inaendelea kuvaa koti la Muungano. Na bahati mbaya katika balaa lililofanyika Dodoma tunaendelea na mfumo ule ule katika Katiba iliyopendekezwa, kwamba Tanganyika iendelee kuvaa koti la Muungano. Tukayasahau yale yote ambayo tuliyokuwa tukiyasema katika Baraza hili kwa miaka mitatu ya mwanzo, hapa hapana tija wala hapana manufaa kwa Zanzibar.

TRA na BOT zitaendelea kuitendea Zanzibar kama vile ni Mkoa tu wa Tanganyika kwa sababu sisi wenyewe tumekataa kusimamia yale tuliyokuwa tukiyazungumza miaka mitatu mfululizo katika Baraza la Wawakilishi. Tulipofika Dodoma Mhe. Spika, tukaufyata, hatukuyasimamia tena tuliyokuwa tukiyazungumza humu ndani.

Mhe. Spika, nimalizie nukta yangu ya mwisho katika hilo hilo kwenye ukurasa wa 82. Ukurasa wa 82 wa ripoti ya Kamati, umezungumzia Idara ya Fedha za Nje na ukazungumzia suala la kashfa ya *accounty* ya Tegeta *Escrow* na kusema kwamba Zanzibar ime-*safer*, imeumia au niseme imeumizwa kwa sababu mafisadi wa Tanganyika wameamua kuchota fedha za Tegeta Escrow Account.

Jana Mhe. Muhammedraza kazungumza sana hapa, lakini Mhe. Spika, akasema hili sio suala la muungano. Lakini sasa tunarudi pale pale. Katika mfumo wa Muungano uliokuwepo hili litaendelea kuitafuna Zanzibar na kama sisi hatutaki kuwa wakweli tunasema vile tukiwa Zanzibar tukifika Dodoma tunaufyata yatarejea yale yale Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hapa Tanzania kwa jumla yake tunavyoambiwa kwa ripoti za magazeti imezuiliwa takriban shilingi trilion moja. Sasa kwa kuchukua asilimia 4.5 tu mbali ya yale maeneo makubwa, maana yake hizo hazipungui bilioni 45 za Zanzibar ambazo zimeshindwa kuja, kwa hivyo zimekwamisha miradi ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ninachosema haya maagizo yanayotolewa humu kwamba mazungumzo yaendelezwe, tutafute utaratibu mwengine. Hakuna utaratibu chini ya mfumo wa muungano unaoendelea kupendekezwa na Katiba hii pendekezwa. Zanzibar itaendelea kuwa koloni la Tanganyika maisha haiwezi kusonga mbele.

Mhe. Spika, ninachokisema ndio kinasikitisha sana, kwamba Kamati zinaendelea kurejea yale yale, ambayo miaka mitatu iliyopita tulikubaliana humu ndani kwamba na majibu ya maswali tuliyokuwa tukiuliza, majibu ya mawaziri kwamba tukifika pahala tuyasimamie haya katika Katiba mpya. Tumewasaliti wananchi wa Zanzibar Mhe. Spika, tunarejea katika mfumo ule ule unaoukandamiza Zanzibar, halafu tunaendelea kupiga kelele.

Mhe. Spika, katika hali kama hii kwamba tunasema jengine tunatenda jengine, tusitegemee kwamba Zanzibar itaweza kuondoka hapa ilipo, labda waje viongozi wanaoipenda Zanzibar, wakweli, wanaosema na kutenda yale yale. Asante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Asante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) aliyetupa uzima na tukaweza kufika katika Baraza hili na tukazungumza machache.

Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati, lakini naona nizungumze tu kidogo kuweza kuunga mkono katika Kamati yangu. Kwanza nianze na pale alipomalizia mwenzangu kwenye Bima. Ningeomba Utumishi kwanza iwache mkono kwenye Bima, wawaachie wajipangie maslahi yao wenyewe. Hili tulikwenda tukaliona na ilikuwa ni changamoto kubwa zilizowapata watu wa Bima.

Mhe. Spika, mimi nitakuja katika ukurasa wa 78, Shamba liliyopo Bagamoyo. Changamoto zilizokuwepo tulikwenda Kamati, tulipofika Bagamoyo tulionana na Uongozi wa Wilaya pamoja na uongozi wa kijiji. Shamba lililokuwepo Bagamoyo kwa maelezo makini tuliyopewa ni kwamba shamba hili sijui tuseme si

letu tena au hatupewi hata sijui nini tueleze. Kwa sababu maneno tuliyoyapata kwa Mkuu wa Mkoa ni kwamba siye tupewa Kilwa, shamba wanataka kulifanya kijiji cha kisasa na wanataka wajenge Bandari Kuu.

Mhe. Spika, la kusikitisha shamba hili watu wazima waliokuwepo ndio waliopeana kuwa tukate shamba hili. Shamba letu limekabidhiwa watu wa Kilimo Kizimbani na wanaweka mabango yao kila pahala. Tulikwenda pale tukaambiwa tayari wameshaweka pikipiki za ulinzi na kila kitu. Mwenyekiti anathubutu kutwambia kwamba mnalinda kinyume ya sheria kwamba shamba sio lenu.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa hatukulipata shamba hili wamechukuwa wenyewe basi sisi tusipewe kilwa wala tusipewe kisiwani kwa binti Abedi tubakie na shamba zetu tulizonazo hapa Zanzibar, ni kwamba hili shamba Mhe. Spika, wanasema sisi si letu na tumelitupa wao wanataka tuweke mji wa kisasa. Ikiwa shamba ni letu, basi ikiwa ni mji wa kisasa hawa waliopewa watu wa kilimo wachukue sehemu zao na palipobaki wakate viwanja wapewe Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nitakuja kwenye Taasisi ya Utafiti hii Kizimbani Mhe. Mwenyekiti na hapa pana Chuo cha Kilimo kilichopo Matangatuani watafiti hawa Mheshimiwa wana changamoto kubwa kwa utafiti wanaoufanya kuwa hawana zana za kisasa kwa kufanyia utafiti za aina mbali mbali za mimea na hata udongo wanaofanyia utafiti, kwa kikwazo cha pesa, hawana pesa. Ni kweli wanapata matatizo makubwa na kila tukenda kilio chao ni hiki. Utafiti uliopo Matangatuani hawa wanafanya utafiti mashamba haya ya Mikarafuu, wana ekari zao pale wana utafiti, lakini na wao wana kikwazo cha changamoto cha pesa hawawezi kuendeleza utafiti huu na ukaweza kuleta matunda kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza tunasema watu wote waliomo wanakaribia kutaka kustaafu, waweze kusomeshwa watu utafiti na waweze kuja pale kupata huduma kabla wale wakongwe hawajaondoka kwa kustaafu, wawe washaingia wapya ili kupata ile taaluma zaidi wa kuweza kutufanyia utafiti katika kusarifu mazao na mambo mengine, mimea, udongo na kila kitu. Mheshimiwa wana changamoto sana hawa, tunaomba Wizara ya Fedha iwaone na wasiwakamate mikono. Kilimo ndio kitu kinachotukwamua wananchi wote.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nitakuja katika Wizara ya Biashara, biashara kwa kweli hatwendi mbele ila tunarudi nyuma, hasa mimi nitazungumzia kwa Pemba. Biashara zinazochukuliwa Mombasa na zikateremka Wete, risiti zinaandikwa Chake Chake, hapawezi pale kuajiriwa watu wa kuandika risiti, wewe uwe na mzigo umeutoa huko umeshafika Wete ufuatilie risiti Chake Chake za malipo, hiki ni kikwazo na wananchi wanaumia kiakili na kimawazo katika biashara zao. Halafu bei wenzangu wanasema hapa bei, kweli Pemba bei ya vitu ni kubwa wanaonunua kwa huyu anaevileta na wao wanazotia ndani ya maduka yao basi bei zao ni kubwa kwa sababu na wao wanauziwa bei kubwa kutoka pale.

Mhe. Spika, tunaomba Wizara ya Biashara iwe makini kwa hili. Kwa sababu tunampa Wizara kwa kumuamini kwa sababu na yeye ni mfanyabiashara aweze kuwalilia wananchi. Vitu kupanda bei kiholela au upande mmoja ikawa bei ni kubwa zaidi kuna kitu gani kinachowakwamisha ya kuwa wao hawawezi kufanya mambo watu waka-*base* na wote tukawa pahala pamoja. Na ikiwa kwamba makontena yanateremka Unguja au makontena yanateremka Mombasa, basi tupatiwe angalau meli za kiasi ndogo ndogo zitakazotupelekea mizigo kule na hayo makontena yakateremshwa kule Pemba kuweza kupata na sisi unafuu wa hizi bei.

Mhe. Spika, ukiinunua biashara hapa hata ukisafirisha mfano kwa meli ya Maendeleo au meli ya Serengeti vikafika kule vitu, watauziwa vipi wananchi vitu hivyo, Sasa tupate unafuu atutetee Waziri aweze kusimamia na kutetea kwa sababu Zanzibar ni Unguja na Pemba.

Halafu Mhe. Spika, changamoto nyengine ninayoiona kilimo hiki cha umwagiliaji wana changamoto na wao. Kwanza tuna changamoto kubwa iliyotukabili katika kilimo na hapa tukae vizuri kuweza kuwafanyia wenzetu kuwachimbulia shamba zao mapema na matrekta Mhe. Spika, yaweze kuletwa yale yanayoweza kukidhi haja katika kilimo.

Mhe. Spika, naiomba Wizara ya Fedha iwe makini kwa sababu kila tunapokwenda kuna changamoto za fedha na hizi changamoto takriban katika Kamati zetu zote tumeziona. Wizara ya Fedha iwe makini kuweza kuwatizama watu hawa ili waweze kutatua matatizo yao na hata kuweza kufanya kazi zao kwa umakini.

Mimi ni mjumbe wa Kamati ilikuwa nikitaka nielezee kidogo na kuunga mkono katika taarifa yangu ya Kamati kwa hivyo Mhe. Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumbambingu na ardhi aliyeniwezesha kufika hapa leo nikiwa na afya njema. Pia, nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo sana katika wizara hizi tatu.

Mhe. Spika, naomba niwapogeze kwa dhati kabisa mawaziri wanaohusiana na maagizo ya Kamati hii kwa majibu yao waliyoyajibu ndani ya nyaraka hizi. Pia, niwapongeze sana wana Kamati ya Biashara na Kilimo kwa kufanya nzito ya kuzunguka katika maeneo tofauti na kuona changamoto au kero zilizomo ndani ya wizara zetu.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye maoni na maagizo ya Kamati namba 23. Namba 23 maagizo ya Kamati yanasema;

"Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo wa ulipaji risiti wa *electronic"*.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri sana, lakini katika majibu yake pia wizara haikujibu vibaya, imelipokea suala na hatua za kukamilisha ziko mbioni kama kawaida yetu. Lakini nataka niseme hili ni jambo zuri sana la kuanzisha huu mfumo kwa sababu mfumo huu unaweza kusaidia Serikali sana katika kukusanya malipo hasa katika mahoteli ya kitalii.

Mhe. Spika, utaratibu wa sasa wa malipo unaruhusu mianya ya kupotea kwa baadhi ya mapato ya Serikali. Kwa hivyo, ni vyema Serikali ikafanya haraka kuanzisha mfumo wa malipo kwenye huduma zote hotelini ili Serikali ipate mapato yanayostahiki.

Mhe. Omar Yussuf, hapa Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu suala alisema kwamba tukusanye sana kodi ili pengine kodi ikiongezeka huenda kilio cha Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo kuongezea mfuko wa jimbo utaongezeka. Kwa hivyo, katika hili atakapoharakisha huu mfumo huu wa *electronic,* pesa za Serikali zitakuwa hazipotei na tutakusanya mapato ili kufanya shughuli zetu na nchi yetu ikazidi kuimarika.

Mhe. Spika, nataka nije katika agizo jengine namba 39. Katika agizo namba 39 juzi hapa katika Wizara ya Habari na Utalii nilimlaumu sana Mhe. Waziri katika mchango wangu, lakini baada ya kuona majibu ya Mhe. Waziri hapa kutoka agizo hili namba 39 nimeona kama wizara hizi hazina tatizo lakini tatizo lipo *ZIPA*.

Nasema hili kwa sababu *ZIPA* walitakiwa kuendeleza kutoa elimu sana kwa jamii au kwa wananchi pamoja na Serikali. Lakini kwa bahati mbaya katika maelezo hayua inaonesha *ZIPA* hawakutoa elimu au hawakufanya jitihada kubwa ya kuongeza elimu, baadae walishirikiana na masheha, Sheha wa Fundo, Sheha ambaye hakuwashirikisha wananchi wa Fundo na Uvinje katika uwekezaji huo.

Mhe. Spika, kwa maelezo ya watu wenyewe wa Fundo na Uvinje, Sheha alichukua tu majina ya watu akapeleka, sasa matokeo ya kupeleka majina haya bila ya kuwashirikisha wahusika Mhe. Spika, nataka nikwambie wananchi wa maeneo hayo kwa sasa wameshaanza kugomeana na kuhasimiana mpaka kwenye shughuli za mazishi kwa sababu ya fitna iliyoingiwa na *ZIPA*.

Mhe. Spika, sasa sijui suala hili waliokwenda kuliingiza pale mpaka kuwafanya watu wakawa wana hasama kiasi hicho ni kwa faida ya nani.

Kwa sababu tunavyofahamu uwekezaji huu ukiwepo pale ni neema kwa nchi nzima. Lakini kwa bahati mbaya matokeo ya hili wananchi wananyanyaswa na vikosi vyenye silaha jambo linalotisha na kuondoa matumaini kwa wananchi wa vijiji viwili hivi au visiwa viwili hivi vya Fundo na Uvinje.

Mhe. Spika, hatma ya watu wa Uvinje na Fundo katika uwekezaji huu siufahamu na juzi nililizungumzia sana hapa, lakini bado naendelea kulizungumza tena hapa kwa sababu pana mawaziri wenyewe husika wote wapo na wanalisikia hili.

Mhe. Spika, naomba kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Waziri wa Fedha, asitishe mara moja uwekezaji huu wa kibabe kwa maslahi ya nchi, kwa maslahi ya wananchi wa vijiji hivi, baadae yeye Waziri wa Fedha pamoja na mimi na wahusika wengine twende Uvinje na Fundo tukawasikilize wananchi, baada ya kuwasikiliza wananchi na maoni yao na utaratibu wao, wanaweza kuendelea kwa sababu hakuna hata mmoja anaelimishwa asielewe katika suala lolote lile.

Lakini tatizo hili lote limekuja kwa sababu *ZIPA* hawakutoa elimu kwa wananchi, walikwenda kwa mtu mmoja tu ambaye ni Sheha na masheha si rafiki sana na wananchi wetu, inavyotakiwa sheha awe rafiki na wananchi wetu, lakini kwa bahati mbaya masheha wetu hawako hivyo. Sasa hili limesababisha fujo na vurugu katika visiwa vyetu hivi, vyenginevyo, Mhe. Spika, bila ya Waziri wa Fedha kuchukua jitihada na hekma na busara zake kama tunavyomuelewa Waziri wa Fedha ni mtu wa hekma na busara, tukaenda kule kuangalia kero za wale watu basi uwekezaji huu hautaleta faida na hata hizo hoteli zikijengwa.

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu baada ya ujenzi wa hoteli hizi zikimalizika kinachotakiwa ni wafanyakazi, wafanyakazi wazalendo wakiwemo wenyewe wakaazi katika yale maeneo. Lakini pamoja na fujo linaloanza sasa hivi wakati wa ujenzi wa vikosi, sasa baadae hoteli hizi zitashindwa kupata mashirikiano kutoka kwa wananchi hasa suala hilo litakuwa ni gumu sana kuziendesha hoteli hizi na yale malengo hasa ya Serikali yetu yatashindikana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri tufanye hivyo nilivyomshauri aende akasikilize baada ya kusikiliza matokeo yatakayopatikana, nina imani wananchi wa vijiji hivi watakubali na wataelewa, ni uelewa tu bado ni mdogo baada ya kuelewa tutaendelea na shughuli zetu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nataka niendelee kidogo kwenye agizo namba 4 kwenye Mfuko wa Hifadhi, hapa nataka nipewe ushauri au nisaidiwe kidogo kwa sababu Mfuko huu wa Hifadhi ni kwa maslahi ya wananchi wetu umetungwa huu kwa mujibu wa sheria kama ilivyoelezwa na unaendelea kutangazwa ili tupate kujiendeleza. Lakini mimi hapa nina wasiwasi kwa sababu kuna watu wa aina nyingi, kuna wafanyakazi wa Serikali ambao mfuko huu mpaka kufikia miaka 60 au 65 na baadae kuna na vijana wetu wengine kama kule Pemba kuna makampuni yanayokuja kwa muda mfupi tu ya ujenzi na makampuni mengine.

Sasa wale na wao wanaingia pale katika mfuko lakini hawana kazi za kudumu, baada ya miaka 3, 4 na 5 pengine ile kampuni inaondoka. Sasa wale akiba yao hii sijui itakaa mpaka muda gani wakati wenyewe wana shinda na wanataka na wao wajisaidie.

Sasa naomba sana kwa sababu wenzetu wa Tanzania Bara Mhe. Spika, kuna mifuko mingi tu unaingia wanakopeshwa kwa njia mbali mbali za ujenzi, ninamuomba Mhe. Waziri ikiwezekana hebu hii sheria ya huu mfuko iangaliwe upya kwa sababu pesa hizi unavyoziweka ni akiba, lakini pesa yetu pia kila wakati inashuka thamani. Utapoweka pesa leo baada ya miaka 10 ile pesa baada ya kupanda inashuka, sasa katika hili kama tuseme hawa watu wa Mfuko wa Hifadhi, wataekewa kitu kama pengine ujenzi au chochote kile iwe kwa mkopo baadae wataiona hasa ile faida ya mfuko ule. Lakini kinyume na hivyo wanakuwa hawaoni faida yoyote, wanakaa tu na kuhangaika hatimayake ule mfuko unakuwa hauwasaidii.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia mimi sikutaka kusema mchango mrefu, mchango wangu ni mfupi mno, kwa hivyo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kusema machache na kama kawaida yangu sitoutafuna muda wako.

Mhe. Spika, wakati tunachangia au wakati tunapitia Ripoti za Kamati, Kamati ya Ustawi Wanawake na Watoto ilikuja na hoja iliyohusu Wizara ya Elimu na wao walikuwa wanaulizia kuhusu fedha ambayo walimu walitakiwa walipwe baada ya makato yaliyokuwa hayakutarajiwa pamoja na fedha ambazo ni mishahara kwa walimu ambao walikuwa hawajapata mishahara yao kwa mwezi wa Oktoba, 2014. Bahati nzuri Wizara ya Elimu hoja hiyo walisema haikuwahusu kwa sababu wao utaratibu waliufuata na Wizara inayohusika na Utumishi wa Umma na wao walisema hoja hii waliipeleka inakohusika yaani Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupata majibu ya walimu hao walipwe haki zao.

Leo tunapitia Wizara ya Fedha, naomba tu Waziri aniambie hoja hii kama mawaziri wenzake wamemfikishia na je, hawa walimu ambao wanadai haki zao watalipwa lini na labda angetwambia sababu za kwa nini watu hawa kukatwa mishahara yao na ikachukua muda mrefu hawajalipwa.

Na kwa nini ikachukua muda mrefu hawa ambao mshahara wao mwezi wa Oktoba walioajiriwa kazi mpaka hivi sasa Mhe. Spika, wakawa mishahara hiyo hawajalipwa. Waziri wa Elimu alijivua akasema hoja hii haiko kwake na Waziri wa Utumishi wa Umma alijivua hoja hii akasema haiko kwake, leo tuko kwenye Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, tunamuomba Waziri ya Fedha atwambie ni kwa nini watu hawa hadi leo hawajalipwa mishahara yao.*(Makofi)*

Mhe. Spika, hilo ni moja, sasa nakwenda kidogo kwenye Ripoti ya Kamati, hoja namba 26 au maoni na maagizo yalikuwa yanasema kwamba;

"Kamati inashauri kuwa ni vyema kwa Serikali kuchunguza kwa makini mfumo wa watalii kulipia wanakotoka (*package tourism*) na kuangalia taratibu zinazohusika na uwezekano wa kuondoa kwa kuwa unaonekana kuwa hauna tija ya kutosha hapa nchini".

Mhe. Spika, majibu ya agizo hili yalikuwa naomba niyaseme kwa ufupi kwamba ushauri umepokelewa. Hata hivyo, kutokana na uzoefu wa nchi nyengine za utalii kama vile Mauritius ni vigumu kuuondoa utalii wa aina hii. Kinachohitajika zaidi ni kudhibiti mianya ya uvujishaji wa mapato hasa kwa kutumia utaratibu wa *transfer pricing*. Kwa muda mrefu Tanzania haikuwa na Kanuni zinazoongoza uzuiaji wa *transfer pricing,* kwa sasa tayari Kanuni hizo zimetiwa saini na Waziri wa Fedha wa SMT na wizara kupitia *ZRB* itaangalia jinsi zinavyoweza kutumika kwa mapato ya *VAT* na hoteli.

Mhe. Spika, nilichojifunza hapa au ninachokiona hapa ni kwamba Kanuni hii imekubalika SMT na wala sio SMZ. Kwa hiyo, nina wasi wasi kwamba Kanuni hizi zikaja zikatumika hapa Zanzibar. Sasa sisi uchumi wetu tofauti na huo wa SMT kama tunavyosema siku zote. Kwa hiyo, tunapotunga Kanuni lazima na sisi tuwe na zetu, tusije tukatumia Kanuni za nchi ambao uchumi wake ni mpana baadae ukaja

ukatuharibia katika ulipaji wa kodi na mengineyo yanayoingiza fedha katika nchi hii. Hilo ndio ninalotaka nishauri zaidi kwamba *ZRB* haiko chini ya Muungano ni ya Zanzibar pekee. Kwa hiyo, wao hawatowajibika moja kwa moja kuzifuata Kanuni ambazo Waziri wa SMT amezitia saini. Kanuni ambazo sisi pengine tuna uwezo wa kuziepuka na wala tusizitumike.
Kwa hiyo, hapa ni lazima tuangalie zaidi nini kinachohitajika, ni Kanuni hizo au sisi tunahitajika tuwe na Kanuni zetu zitakazolinda uchumi wetu. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, lakini jengine wengi wamezungumzia kuhusu *TRA*, mimi nataka nizungumzie kwa aina nyengine labda kidogo.

Agizo Nam. 31 linahusiana na ushauri Kamati inaishauri *TRA* kufuatilia kwa makini malalamiko na usumbufu wanaoupata wananchi wa Zanzibar wanaosafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara ili kubaini kama kuna mapungufu au vikwazo vyovyote visivyo vya lazima viweze kuchukuliwa hatua.

Mhe. Spika, utekelezaji unasema hivi, tatizo kubwa ni kutumika mifumo tofauti ya kutathmini bidhaa ambapo Tanzania Bara wanatumia mfumo wa *Import Export Commodity Database* (*IECD*) na Zanzibar wanatumia mfumo wa zamani. Hali hiyo ndio inaopelekea kufanyika tathmini mpya kwa bidhaa zote zinazopelekwa Tanzania Bara kutoka Zanzibar na hatimae kutakiwa kulipa tofauti ya kodi inayojitokeza kama ipo.

Mhe. Spika, kwanza mimi napata wasi wasi ninavyofahamu mimi *TRA* ni chombo cha Muungano, sasa leo ukiniambia kwamba sisi tunatumia mfumo wetu Zanzibar na Tanzania Bara wanatumia mfumo wao, unanichanganya, hebu waziri atwambie sisi tunatumia mfumo mmoja unaotokana na *TRA* au tunatumia mifumo miwili tofauti na kwa nini tunatumia mifumo hiyo miwili tofauti?

Mhe. Spika, lakini jengine huu mfumo unaotumiwa hapa Zanzibar ambao wanaoita ni mfumo wa zamani umekubalika na Serikali kwamba utumike. Sasa ikiwa umekubalika na Serikali kwa nini wao wanashindwa kuutetea mfumo huu, wakati tunapokwenda na bidhaa zetu kule Tanzania Bara tukasema sisi tunatumia mfumo wetu, wakautetea ili kuthibitisha kwamba bidhaa yoyote inayoingia *entry port* yoyote pale unapotoka ndio unahesabika umeshatozwa kodi.

Mhe. Spika, mimi napata wasi wasi kwamba hapa tunababaishwa na kama hakuna ubabaishaji basi hii sheria moja tu ya *TRA* ingetumika, kama haitumiki hizo wao kwa nini wakatumia mfumo huu hapa Zanzibar ili kuwasumbua wafanyabiashara wetu. Ikiwa wameuweka makusudi mfumo huu kwamba wanautaka utumike Zanzibar, basi wautetee kwamba sisi tunatumia mfumo wetu huu Zanzibar wa zamani, kwa hiyo, tunataka tuutetee, utakapokwenda na bidhaa kule utambulike rasmi.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema sitaki kuutafuna muda wako, nakushukuru.
**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo sana katika ripoto hii ya Kamati tatu hizi ikiwemo Kamati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wana Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa maagizo yao waliyoyatoa kupitia wizara hizi kwa kutaka utekelezaji na ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, niseme tu na mimi kuwa naunga mkono maoni ya Kamati ili kutilia mkazo kwamba tunaiomba Serikali maagizo haya basi wachukue hatua muafaka za kuweza kushughulikia kwa ajili ya kupata ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, mimi nianze na majibu haya ya Wizara ya Fedha kama yalivyoelezwa hapa na nianze moja kwa moja katika agizo hili Nam. 7 linalozungumzia kuwa ni vizuri kwa Serikali kulifikiria kwa moyo wa

huruma suala la kulipatia eneo jengine Shirika la Bima kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya shirika hilo Kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, hili suala la kupatiwa Shirika la Bima jengo jengine niseme kwamba kwa Serikali yetu hii, suala la majengo ya Serikali limekuwa ni suala sugu, yaani ni changamoto kubwa katika Serikali yetu.Taasisi zote unazokwenda basi changamoto kubwa utaelezewa au utajionea kwa macho yako jinsi ya majengo ya maofisi yalivyo hasa katika Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, hii inasikitisha sana, inasikitisha sana na badala ya suala la maofisi, suala jengine linalofuatia katika Serikali yetu ni bajeti finyu ambazo kuwa wizara wataomba lakini kile wanachokiomba hawakipati, watakisiwa wapate hiki lakini hata hicho wanachokisiwa pia hakipatikani. Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Fedha masuala haya mawili ni masuala sugu katika Serikali yetu hasa katika Kisiwa cha Pemba ofisi zote unazokwenda zinasikitisha jinsi wanavyofanya kazi katika uzalendo wao wa kuweza kuvumilia mengi ndani ya ofisi hizo.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri tunaiomba Serikali kwa kupitia wizara yako mujipange muyaangalie maofisi ya Serikali wengine wanafika pahala hata mule ofisini mtu anaogopa kukaa, mtu anakaa ofisi macho yake yote yako juu anaogopa kuja kuelemewa na kiambaza. Kwa hiyo, Mhe. Waziri hili kiserikali liangalieni ni tatizo sana sana katika Serikali yetu hii.

Mhe. Spika, suala jengine nataka nizungumzie hili suala la agizo Nam. 16 anasema kwamba;"Mikakati maalum inahitajika katika kuimarisha utendaji wa wafanyakazi wa *PBZ* hususan wanapotoa huduma za moja kwa moja kwa wateja ili kupunguza malalamiko ya wateja kutokana na usumbufu unaopatikana".

Mhe. Spika, mimi *PBZ* niwapongeze lakini wakati mwengine hakuna kizuri kisicho kasoro hizi siku za nyuma kulitokea malalamika kwamba *PBZ* ilikuwa ukienda na shilingi elfu kumi kama umekwenda kuibadilisha inahitilafu kidogo basi walikuwa hawaichukui. Kwa hiyo, wasitufanyie hivyo au wasiwafanyie wananchi hivyo kwa sababu wao ni lazima watu waende pale kama pesa yake pengine imeharibika aende akabadilishiwe pale.

Sasa kwa hiyo ukimrudishia mwananchi hajui pengine pakuipeleka. Kwa hiyo, hili tatizo lilijitokeza, kwa hivyo, tunaomba kuwa wasiendelee kufanya hivi kwa sababu wao ndio wanakujua zile pesa wapi wazipeleke ili na wao wananchi wasipate usumbufu mle madukani au kwenye dalala.

Mhe. Spika, suala jengine ni agizo Nam. 17 ni vyema kwa taasisi za SMZ zenye ofisi Dar es Salaam kufungua *accounts* zao katika Benki ya Watu wa Zanzibar, kusaidia kuendeleza shughuli za benki hiyo huko Tanzania Bara.

Mhe. Spika, na mimi naungana mkono na agizo hili hizo taasisi zilizoko huko basi zifanye hivyo. Mhe. Spika, lakini si kufungua benki tu katika Taasisi za SMZ zilizoko huko, lakini kuna ile ofisi pale ambayo kuwa ni ofisi ya uratibu wa shughuli za SMZ kule Bara, Wazanzibari walioko kule hata kuitembelea ile ofisi hawana uzoefu huo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri na Serikali basi zile taasisi zilizoko kule za SMZ watambue uwepo na zile ofisi zao kama hizo Ofisi za Uratibu wa Shughuli za SMZ kule Dar es Salaam, si kuwa watambue tu kwenda kufungua kutumia Benki ya Zanzibar lakini hata ofisi zao zilizopo wazitambue katika ufanisi mzuri na lile linalokusudiwa liweze kutendeka.

Mhe. Spika, kuna suala moja nataka nilizungumze halimo humu kwenye ripoti, lakini nililikuta kwenye Ripoti ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Serikali, suala hili la deni ambalo Wizara ya Kilimo wanadaiwa deni na SUMA JKT, wanawadaia karibuni matrekta 50 nilivyoikuta kwenye ripoti yao.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Fedha tunakuomba hili mimi nadhani ni la ukweli kwa sababu mpaka sisi tulipokwenda juzi kwenye Kamati, tulikwenda SUMA JKT wenyewe wanalalamikiwa kwamba tayari walitoa matrekta yao na mpaka leo hii wameshindwa kulipa. Kwa hiyo, sio vizuri watu wameshasema "muamba na wako akutuma". Kwa hiyo, hili suala sijalisikia kuzungumzwa hapa na nililiona kwenye ripoti hii ya Viongozi Wakuu.

Kwa hiyo, nakuomba kama suala hili lipo basi Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wewe au na Serikali kwa ujumla basi hili deni mlipatie ufumbuzi. Wakati mwengine inaonesha masikitiko kwa sababu nilishangaa nilipolikuta kwenye Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu haijuulikani sasa kama ni Wizara ya Kilimo ndio waliokwenda kukopa wenyewe au ni Serikali ndio iliyokwenda kukopa matrekta yale. Kwa hiyo, naona kwa Wizara ya Kilimo hawana ubavu kutokana na bajeti zao. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali basi kama wamesahau hili deni wajue kwamba wenyewe wanalizungumza wanapowakuta watu kama sisi tunapotoka huku.

Mhe. Spika, niende kwenye hoja hizi za Wizara ya Kilimo agizo Nam. 2 linasema kwamba; "Katika kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi pamoja na wizara inayohusika na ajira inapaswa kutilia mkazo suala la uajiri na wafanyakazi wanaojaza nafasi za wafanyakazi waliostaafu na waliofikia kabla ya kushughulikia ajira mpya".

Mhe. Spika, na hili ni tatizo sugu hasa katika Wizara hii ya Kilimo, tangu mimi niko kwenye Kamati hii suala hili tunalizungumza la uajiri wa wafanyakazi wanaofikia pahala kustaafu wanatimiza sijui miaka mingapi nafasi zile hazijajazwa. Sasa na hii hali Mhe. Spika, tunazungumza lakini hata hao mawaziri wengine hawapo wakaweza kusikia hizi changamoto nyengine zilizopo.

Mhe. Spika, hili ni tatizo na wizara hii ambayo kuwa watu ndio wanaoelekeza ajira zao, Wizara ya Kilima kwamba mpaka leo hii wanafika pahala watu wanastaafu wanakaa miaka, wizara inaomba wafanyakazi lakini wafanyakazi hao hawapatikani, haipendezi kwa sababu wanajuulikana wanaotaka kustaafu na waliokuwa hawajafikia muda wa kustaafu. Kwa hiyo, tunaomba kuwa watu watakapostaafu basi nafasi zile zijazwe kwa utaratibu mzuri ili upungue ule usumbufu wa wataalamu na mambo mengine.

Mhe. Spika, agizo jengine kuna agizo hili Nam. 17 kwamba; "Wizara iwe makini katika kutoza ada kwenye magari makubwa yanayochimba kifusi", lakini huku katika maelezo ya wizara kasema kwamba maliasili zote zisizorejesheka kama mawe, kifusi, mchanga, kokoto na udongo huku ameseka kuwa tani moja ni shilingi laki moja, hii ni kwa mujibu wa Kanuni za mazingira. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri mwenye dhamana hii anayewasilisha wizara hii hebu aje anipe maelezo, kwa sababu sijajua elfu moja hii inayolipwa maeneo gani. Kwa sababu kama kule kwetu gari inayotoka ikaingia Micheweni kuchukua mawe au kitu chochote haitozwi shilingi elfu moja, pale inatozwa shilingi elfu nane na akienda tena analipa shilingi elfu nane.

Sasa kwa siku magari mangapi yahesabu yanayoingia kule, sasa aje anifahamishe hii shilingi elfu moja kwa mujibu wa Kanuni ya Mazingira ni wapi wanaochukua pesa hizi shilingi elfu moja. Na wale waliopo pale msituni au ni wengine kwa mujibu wa hili agizo linavyotolewa.

Mhe. Spika, agizo jengine la Nam. 20 linasema; "Kwa vile wana jamii katika skuli za wakulima wana taaluma ya kutosha ya kilimo bora isipokuwa wanaukosefu wa vitendea kazi hususan maji ni vyema wizara kwa kushirikiana na mamlaka inayohusika na huduma ya maji zikae pamoja kwa ajili ya kuona uwezekano wa namna ya kuwasaidia wana jamii hao juu ya kupata unafuu wa gharama za matumizi ya maji katika mashamba yao na katika maeneo yao mengine ya kilimo.

Mhe. Spika, na hili tumeshalizungumza katika Baraza hili na tukafikia pahali tukaambiwa kuwa gharama hizi hapa nazumzia yale mabonde ya umwagiliaji maji, wanaolima katika mabonde ya umwagiliaji maji

wenye visima wale wanatumia muda maalum wa kutumia vile visima. Lakini linalojitokeza pale ni wakulima wale kulipa ile *serving charge* na *VAT* ambayo kuwa kisima hakitumiki wao wanatumia kwa muda maalum lakini wakija wakitaka matumizi ya kisima kile kuna madeni tele kwenye mita.

Na hili siku moja lilitolewa ufafanuzi kwamba wizara itazungumza na hawa *ZECO* ili kupata unafuu wa gharama hizi. Lakini bado hili suala linaendelea kwa sababu tumekusudia kuwawezesha wananchi wetu katika shughuli za kilimo tena cha umwagiliaji maji basi waone umuhimu wa kuweza kuwaondolea haya mambo. Kwa sababu aghalabu wao hutumia maji katika msimu wa vuli, lakini katika msimu wa mvua za mwaka hawatumii visima. Sasa leo miezi yote ile inaendelea kuwepo madeni wakija wakifika pahali wanataka kutumia maji yale inaonekana kuwa tayari kuna madeni na wanashindwa kulipa deni lile.

Kwa hiyo, tunaomba hii Wizara ya Kilimo na Maliasili na hao watu wa *ZECO* wakae pahali pamoja wakubaliane na washauriane katika kuwapunguzia gharama hawa wananchi wetu kwa lengo la kuondoa huo umasikini.

Mhe. Spika, suala jengine nije katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko agizo namba 18 linasema; "Kamati inapendekeza kwa serikali kuwa Ofisi ya *ZSTC* ya Dar es Salaam zisifungwe na itaweza kutangaza bidhaa kwa shirika Zanzibar katika Soko la Afrika na kwengineko".

Mhe. Spika, hili Shirika la *ZSTC* lilioko Dar es Salaam ilikuwa hizo siku za nyuma hiyo nyumba ilikuwa ni ya kukodi na tukawa tunapiga kelele sana hapa kuwa basi shirika angalau waweze kununu nyumba yao kwa sababu wanafanya shughuli zao nyingi pale, biashara zao zinatoka na kipato wanapata, lakini linalowa-*cost* ni ile gharaka ya kulipia jengo hilo. Sasa hapa hapakutolewa ufafanuzi huo isipokuwa kwa majibu ya Serikali kasema huo ndio msimamo wa Serikali pia.

Kwa hiyo, naomba basi watueleze kuwa hili jengo tayari lishakuwa milki ya hili shirika au bado wanaendelea kukodi? Kama wanaendelea kukodi basi na hiyo Serikali itakuwa sio msimamo wao wa kuwataka watangazie hizo biashara zao huku isipokuwa itakuwa wanadanganya. Hili nalo naomba nije nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwa hayo, machache nakushukuru na naunga mkono hizi ripoti zote za Kamati. Ahsante sana.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kusimama hapa. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na kwa kweli mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana. Naomba nianze mchango wangu kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ukurasa namba moja kwenye agizo nambari 4, linalohusu Kiwanda cha Usarifu Chumvi Wawi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo mengi ya Mhe. Waziri amemalizia maneno yake katika ukurasa wa pili kwamba, eti wizara inaendelea na mazungumzo na kiwanda hicho ili kuzitafutia ufumbuzi kasoro hizo. Hapa ndipo penye masikitiko yangu makubwa, maana inaonesha kama Serikali ilivyokosa umakini na suala la uzalishaji chumvi.

Mhe. Spika, katika bajeti mbili zilizopita nilichangia suala la chumvi na nilihoji katika Baraza lako hili tukufu. Chumvi uzalishaji wake unasimamiwa na nani? Kwa bahati mbaya sana Serikali mara ya mwanzo ilinijibu kama chumvi inasimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini baadae Serikali hiyo hiyo imetanabahi na kunambia kwamba chumvi inasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, katika muda wote huo Serikali haijachukua hatua yoyote ya kuwasaidia wakulima wa chumvi ambao wengi wako Pemba kuongeza uzalishaji na kuwatafutia soko. Kwa kweli ni aibu, tena ni

aibu sana kuona Serikali yetu hii ikiruhusu uingizaji wa chumvi nchini kutoka nje wakati hapa petu pana wazalishaji wa ndani ambao wana uwezo mkubwa wa uzalishaji, lakini wanakosa soko.

Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha na sijui hata niseme vipi, lakini mimi nashangaa sana suala hili kuachiwa hivi, utafikiria labda Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ziko likizo, ni jambo la kusikitisha na mimi sielewi hasa na wala wakulima wa chumvi wa Wilaya ya Chake Chake hawawezi kuielewa Serikali.

Mhe. Spika, hapo mwanzo tuseme kweli chumvi ilikuwa haishughulikiwi lakini miaka miwili, bajeti mbili zishapita nazungumzia chumvi, leo hapa tunaambiwa ati suala hili wizara inaendelea na mazungumzo na kiwanda hicho ili kuzitafutia ufumbuzi kasoro hizo. Bajeti mbili Mhe. Spika, bado suala linatafutiwa ufumbuzi. Naomba nimalizie hapo kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, lakini Serikali ijue kama wananchi wazalishaji wa chumvi hawawezi kuielewa Serikali yao.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili, ukurasa wa nne kwenye agizo nambari 4. Wizara pia hapa inamalizia majibu yake kwa kusema kwamba; "Eti wizara imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa nguo za kazi kwa mafundi wa matrekta na hadi sasa fedha hizo hazijapatikana".

Mhe. Spika, mimi naishi jirani sana na Karakana ya Matrekta iliyoko Wawi na ni karibu miaka 30 sasa, naielewa vilivyo karakana ile, kilicho dhahiri ni kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili imeshindwa kuisimamie Karakana ile.

Mhe. Spika, hapo zamani ilikuwa Karakana ile ni Karakana hasa, lakini sasa imekuwa ni *garage.* wafanyakazi hawana nguo na viatu vya kazi, maslahi yao yako duni na baya zaidi hawana hata zile zana za kufanyia kazi achilia mbali *spares* na vilainisho. Mheshimiwa ikiwa Serikali imeshindwa kuwanunulia wafanyakazi mabwelasuti, maguo ya buluu, itaweza vipi kuwawezesha mafundi hao au kutengeneza matrekta ili wananchi wapate walimiwe. Kwa kweli ikiwa wizara inashindwa hata zile nguo *(uniform),* sifikirii kama itaweza kuendesha Karakana kwa kufanyakazi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba nilizungumzie kidogo ni agizo nambari 5 ambalo naomba nitoe kama ushauri katika agizo la Kamati lililosema kwamba; "Wizara ijipange katika kubuni miradi mipya ya kuendeleza wakulima". Wizara ilijibu kwamba wizara imejipanga katika kubuni miradi mipya.

Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba katika kujipanga huko kuna hii miradi ya wakulima ya mboga mboga inayoitwa *green house*. Taarifa niliyonayo ni kwamba miradi hii ina uwezo wa kuzalisha kwa kiwango kikubwa. Sasa, je, kwa vile mboga mboga nyingi zinazotumika katika mahoteli ya kitalii zinatoka Bara, kwa nini wizara haifanyi utafiti wa kujua je kilimo hiki kwa hali ya hewa yetu ya Unguja na Pemba vinaweza vikazalisha?

Mhe. Spika, je, kwenye vituo vyetu vya utafiti vya Kizimbani Unguja na Matangatuani Pemba kuna *green house* yoyote iliyowekwa kwa utafiti? Kama hakuna, hatuoni kuwa bado Wizara ya Kilimo na Maliasili haiko makini?

Mhe. Spika, hivi sasa wananchi wetu wengi wanaendelea kununua *green house* bila ya ushauri wa kitafiti kutoka Wizara ya Kilimo na Maliasili, lakini matokeo yasipokuwa mazuri, Wizara ya Kilimo na Maliasili itakuwa iliwaachia wapate hasara wakulima hao kwa sababu hawakufanya utafiti na wakulima wakawapa ushauri wa kitafiti.

Naomba nimalizie mchango wangu kwa Wizara ya Fedha. Kwanza kuna jambo moja ambalo linawaletea usumbufu sana wafanyabiashara wa Pemba. Wafanyabiashara wa Pemba wanapoagiza bidhaa zao kutoka Tanga zikifika tu pale Pemba Wete kabla ya kushushwa wafanyabiashara wale wanatakiwa waende

Chake Chake kwa ajili ya kulipia ushuru. Kwa kweli huo ni usumbufu sijui kwa nini Wizara ya Fedha haiandai utaratibu ikawa ule ushuru wanalipa pale kuliko mfanyabiashara atoke aje Chake Chake kwa kulipia ushuru.

Jambo jengine ambalo linanishangaza ni kuwa hivi vyombo vya ukusanyaji mapato *TRA* na *ZRB* haviko tofauti Unguja na Pemba, lakini sijui ni sababu zipi zinazosababisha bidhaa zinazouzwa Unguja na zinazouzwa Pemba kutofautiana sana kibei. Mhe. Spika, naomba nitoe mfano, hapa Unguja mfuko wa saruji ni shilingi 13,000/= mpaka 13,500; lakini Pemba ni shilingi 17,000, pana tofauti kubwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, tunamuomba atakapokuja atwambie ni sababu ipi iliyopelekea kuwa na tofauti hii ya bidhaa hizi Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, naomba niende ukurasa wa 12 ambako kuna agizo Nam. 19, Kamati imesema *PBZ* iongeze mikakati mingine ili benki hiyo iweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia. Majibu ya Mhe. Waziri ni mazuri, ambayo amejibu kuwa benki inatoa huduma mbali mbali kwa kutumia hiyo teknolojia. Sasa hapa katika agizo hili na kwa majibu ya Mhe. Waziri nina ombi moja ambalo nakuomba sana na wewe Mhe. Spika kwa unyenyekevu wa hali ya juu ombi hili ulikubali.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri katwambia hapa teknolojia hii inavyofanya kazi, naomba kama hii teknolojia iwanufaishe na Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Waziri atuwekee *ATM* katika jengo hili ambayo itasaidia sana kurahisisha huduma kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hata watendaji.Tulipokuwa Dodoma tulishuhudia, katika jengo lile kuna *ATM* ambayo ilikuwa ikitusaidia sana kupata huduma, sisi Wajumbe makini wa UKAWA na hata wale Wajumbe wenzetu.(*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Spika, hili Mhe. Waziri alipe umuhimu litasaidia sana kuokoa muda mwingi kwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kufuata huduma hii katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, nakushukuru nami kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika ripoti hizi za Kamati. Pia, niishukuru Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya wakati wa shughuli zao za Kamati.

Mhe. Spika, sasa nianze kujibu mambo ambayo yamechangiwa na hasa nianze kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama ifuatavyo:

Mhe. Makame Mshimba, alionesha masikitiko makubwa kwa mwekezaji anayetaka kuwekeza kwenye zao la mpunga na kuelekeza kuwa mwekezaji huyo anazungushwa hadi sasa. Napenda kumuelekeza kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji nchini, mwekezaji ni lazima apeleke maombi yake *ZIPA* pamoja na andiko la mradi, kitu ambacho mwekezaji huyo bado hajakifanya. Hata hivyo, Wizara ya Kilimo na Maliasili inafikiria kufika kwa mwekezaji huyo na kuwasilisha azma yake kutaka kuwekeza kwenye kilimo cha zao la mpunga. Aidha, wizara imemtaka alete andiko la mradi kwa ajili ya kupata michango juu ya mradi huo kitu ambacho bado hajatekeleza.

Kwa hivyo, sio kama wizara imekataa au inampiga danadana, isipokuwa kila kitu kina utaratibu wake. Sasa utaratibu ni kama sheria, kwanza utaratibu afike *ZIPA* halafu tuone na sisi tunakuwa tuko pamoja naye kwa kiasi gani. Wizara pia imechukua juhudi za makusudi za kumsaidia mwekezaji huyo kwa kumpatia matokeo ya tafiti za mpunga nchini, bajeti na ratiba ya uhamasishaji kwa wakulima kwa kuingia katika mpango huo pamoja na kumkutanisha na mshauri mwelekezi kutoka *Kilimo trust,* kupitia *Comparative Africa Rice* mnamo tarehe 24/03/2015 kwa ajili ya kupata msaada na maelekezo katika uandishi wa mradi huo.

Wizara pia itaendelea kumsaidia mwelekezaji huyo ili kufanikisha suala hili la uwekezaji katika zao la mpunga nchini.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kuwa kuhusu suala la sare za wafanyakazi wa Karakana. Hili limezungumzwa hata na Mhe. Salma Mohamed Ali, amezungumza sasa hivi. Suala hili la sare kuhusu Karakana ya Matrekta majibu tuliyoyaeleza yalikuwa ni kwa mwaka 2013/2014, lakini kwa hivi sasa mafundi wa Karakana wameshapatiwa sare hizo. Pia, tunapenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa wizara itaendelea kuwapatia sare mpya wafanyakazi hao kila hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili inajitahidi kuwalipa wafanyakazi wake fedha za *overtime* pamoja na malipo mengine ikiwemo likizo, lakini kutokana na hali ya fedha tunashindwa kuwalipa wote kwa pamoja. Hadi hivi sasa wizara imeshalipa asilimia 50 ya wafanyakazi waliokwenda likizo fedha zao za likizo. Hata hivyo, wizara inachukua ushauri huu na kuahidi kuufanyia kazi. Aidha, kuhusu suala la ajira wizara inaendelea kulishughulikia suala hilo kwa kushirikiana na wizara inayohusika na ajira.

Mhe. Spika, suala jengine la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na kukamilisha kwa jengo la usarifu wa mazao Kizimbani, kupitia fedha za maendeleo zinazotolewa na Serikali. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha shilingi 361 milioni utaharakisha ukamilishaji wa jengo hilo.

Aidha, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa jengo la usarifu wa mazao Kizimbani limejengwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani. Pia, kutoa elimu ya usarifu wa mazao kwa wakulima na wajasiriamali ili kuongeza tija katika mazao hayo.

Mhe. Spika, suala hili pia nililijibu hivi juzi aliuliza yeye Mhe. Jaku Hashim, lakini alikuwa hayupo, kuhusu suala lake kwamba jengo hili tuwape Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mimi namshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, leo alilifafanua vizuri kwamba hili jengo lilijengwa kwa ajili ya Wizara ya Kilimo la mafunzo ya usarifu wa mazao. Kinachotakikana hapa si chengine kutafuta fedha kuhimiza na kulimaliza jengo lile, ndicho kinachotakiwa, sio kutoa wizara kwenda kuwapa wizara nyengine, na hili juhudi za kutafutwa fedha hizi tunazo. Pia nilizungumzia hapa kwamba vile vifaa vilivyokuwepo pale bado havijaharibika, zilizoharibika ni *chemicals* tu.

Lakini na vifaa vile pia tayari tushawapigia wenye kuhusika kwamba waje watufungie, na saa yoyote wakija vifaa vile vitafungwa. Kwa sababu lile jengo kilichobakia sio kwamba kuna uzuizi wa kufungwa vifaa vile. Nadhani kazi iliyobakia ni sehemu ya juu kuweka *hard board.* Kwa hivyo, ufungaji wa vifaa watakapojibu tutavifunga kwa haraka.

Mhe. Spika, napenda kujibu hoja ya Mhe. Raya Suleiman Hamad kuhusu suala la wakulima kuwalimia mapema. Wizara ya Kilimo na Maliasili pia nayo inaendelea na jitihada zake za kuwalimia wakulima mapema na suala hili Mhe. Spika, lina pande mbili nalo. Kuna mtazamo mmoja mkulima naye anatakiwa achangie, kwa hivyo atakavyoleta mchango wake mapema basi bila shaka ukulima huu utaanza mapema mbali na kasoro tulizokuwanazo ambazo tunazishughulikia za matrekta kuwa mabovu, hili ni suala ambalo tunalipigia mbio. Hivi juzi tu karibuni nadhani miezi iliyopita tulipata matrekta yale yametusaidia hapa matrekta kumi (10). Kwa hivyo matrekta 20, kwa hivyo, na hili nalo wizara kupitia na serikali linapigiwa mbio ili kuona vifaa vya matrekta ambavyo uchakavu wa matrekta nao pia unapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, hata hivyo, wizara imo katika mpango wa kuwahamasisha wakulima kutoa malipo yao mara tu baada ya kumaliza mavuno yao ili kupata nafasi ya kuwalimia mapema. Ili pale wakishavuna tu wakulima na tukaanza michango yetu mapema basi ukulima tutaanza kulima kwa mapema.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili kwa kushirikiana na shirika la *USAID* kupitia mradi wa nafaka inaendelea na utafiti wa mbinu za uzalishaji mpunga katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ikiwemo Kilombero na Kipange kwa Unguja na Pujini, Tambini na maeneo mengine kwa Pemba.

Utafiti huu bado unaendelea na matokeo ya mwazo yanaonesha kwamba uzalishaji wa zao la mpunga unaweza kuongezeka sana kufikia hadi tani tano kwa hekta kutoka tani moja. Hii ni kutokana na matumizi ya mbegu bora, matumizi bora ya mbolea na uwekaji sawa ardhi na kuweka matuta ya kuzuia maji ya mvua.

Mradi huu pia umetoa mafunzo kwa wakulima elfu mbili mia saba (2700) kutoka Pemba na elfu moja mia tatu (1300) kutoka Unguja na kuanzisha vishamba vya maonesho arubaini (40) kuhusu utaalamu huo. Mradi huo unaendelea kwa awamu ya pili kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kitaalamu wakulima wa zao hilo ili kuongeza tija katika kilimo hichi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo pia nitoe shukrani kwa Wajumbe wa Baraza kwa kunisikiliza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Nashukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipatia mimi fursa ya kusema machache katika taarifa za ripoti zilizowasilishwa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, wizara yetu Wizara ya Biashara imeguswa na Waheshimiwa Wajumbe sita wa Baraza lako. Hoja zilikuwa ni nyingi lakini mimi nitagusia hoja chache kama ifuatavyo:-

Hoja aliyotoa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusu kiwanda cha Makonyo Pemba kuzalisha mafuta yatokane na majani ya mkarafuu. Mhe. Spika, hili tayari wizara inalifanyia kazi na siku kwa majani ya mkarafuu peke yake, lakini viungo vinavyozalishwa ambavyo vinatoa mafuta basi kufuatia utafiti uliofanywa na *TILDO* na hili nalo linafanyiwa kazi, kwa hivyo matokeo nayo yatatokana na taarifa ya ripoti hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mohammed Haji amezungumzia kuhusu suala la chumvi. Taarifa ya suala la usarifu wa zao la chumvi Mhe. Spika, wizara yangu imekuwa ikilizungumzia sana suala hili. Utaratibu wote wa uzalishaji uko katika Wizara ya Mifugo lakini usarifu wake uko chini ya Wizara ya Biashara, na hili tayari kupitia *ZSTC* limeshaanza kufanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa sio tu kwa matumizi ya chakula lakini pia chumvi imefanyiwa utafiti kwa kushirikiana na *ZSTC* na kamapuni moja ya biashara kule Japan, na kwa hiyo chumvi itakuwa na matumizi kadhaa ikiwemo kama kuzalisha chumvi ambayo itatumika kwenye maji ya kukoga, na kuweza kutumika kama dawa kwa viungo vya binadamu.

Kwa hiyo, chumvi sio kama imedharauliwa kama alivyosema Mheshimiwa, lakini sisi ndani ya Wizara ya Biashara tumelifanyia kazi hilo, na tayari wazalishaji wa zao hili la chumvi kule Pemba wanafahamu hivyo, kwa sababu wameshirikishwa katika kulifanyia kazi suala hili la chumvi.

Nimalizie Mhe. Spika, kwa kushukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuchangia katika wizara yetu hii, na masuala mengine yaliyobakia basi Mhe. Waziri atayazungumzia katika taarifa yake. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na mimi nataka nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wote ambao wamechangia kuanzia Kaimu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe.

Mimi ya kwangu yatakuwa ni machache, lakini nataka niseme kwamba maoni ya Wajumbe yote tumeyapokea na mengine yamechangiwa kutokana na taarifa ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti au Kaimu Mwenyekiti au Kamati hiyo inakusudia kujibu au kujibiwa katika kikao cha mwezi kama wa leo mwakani, lakini yale ya msingi Mhe Spika, nimeyachukua na nitaomba niyatolee maelezo.

La kwanza ambalo nahisi ni muhimu sana kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kufahamu Mhe. Spika, mimi nikiwa Waziri wa Fedha ninapokuja hapa kuzungumzia suala la makusanyo nataka Wajumbe wako waniamini na wala sidanganyi. Makusanyo tulipoingia mwezi wa Novemba mwaka 2010 jambo la kwanza nilijiuliza nitajipima mimi kwa kigezo gani? Nikaangalia makusanyo ya taasisi zote mbili; *ZRB* na *TRA* kwa mwezi nikakuta wastani ni bilioni kumi na tatu (13 *billions*) na ndio maana kila ninapokuja hapa kwenye Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, huwa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tusaidiane, na nataka niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako wamenisadia kwa nguvu zao zote.
Leo wastani kwa mwezi tunakusanya bilioni thalathini (30 *billions)*. Tokea tumeanza mwezi wa Julai kuna *fluctuation* inategemeana na watalii wanaongia, inategemeana na bidhaa zinazoingia lakini tumetoka bilioni ishirini na nane (28 *billions),* na nimegundua kuna mwezi mmoja tumekusanya bilioni thalathini na nne( 34 *billions)*.

Kwa hivyo, bado nitaendelea kuwaomba Waheshimiwa hawa Wawakilishi waendelee kunisaidia mimi mwenzao, kwa sababu jukumu la kukusanya kodi licha ya kwamba limekabidhiwa Wizara ya Fedha, lakini ni jukumu letu sote, kuwahimiza wananchi wetu walipa kodi watusaidie ili tuweze kupata kodi kwa ajili ya maendeleo yetu, hilo la kwanza.

Lakini la pili, Mhe. Spika, naomba sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wafahamu bilioni thalathini(30 *billions)* kwa nchi kama yetu sio pesa nyingi kulingana na matatizo tuliyonayo. Tuna matatizo mengi na tunahitajia fedha nyingi, nataka niyataje tu baadhi ya majukumu ambayo kila mwezi lazima Wizara ya Fedha itoe, yaani hizo ni lazima.

Nimeulizwa na Wajumbe wengi hapa, kila Waziri akija sina pesa, sina pesa na kweli hata mimi Wizara ya Fedha kama nitakaa hapa nikisema hasa ya kwangu mimi mwenyewe mumenisemea nyinyi. *PBZ* tu na *PBZ* ni ya kwangu mimi na mumenisemea nyinyi na sio kama sitaki kumlisha mtoto wangu ninayemlea, nataka sana, lakini na mimi sina. Nataka nitaje majukumu ya lazima kila mmoja ayajue na kila mmoja akamate kalamu.

Mhe. Spika, katika bilioni thalathini (30 *billions)* wastani tunazozikusanya kwa mwezi bilioni kumi na tano nukta tatu ni mishahara (15.3 *billions*). Hii ni mishahara inayokwenda katika taasisi zile ambazo sizipi ruzuku, zaidi ya asilimia hamsini, ni mishahara tu nalipa.

Katika Mfuko Mkuu kuna pesa za lazima Mhe. Spika, lazima nizitoe kama mishahara ya viongozi wakuu. Nikikwambieni mishahara ya viongozi wakuu nyinyi mnawatizama hawa watatu tu waliopo hapa, mimi sina watatu, nina mpaka wastaafu, Zanzibar tuna wengi zaidi ya kuwahudumia kuliko Serikali ya Muungano ni milioni mia moja nukta tano (100.5 *millions)*.

Safari za ndani za viongozi, maana yake hapa lazima tuyaone haya mambo, tena nataka nikwambieni wanaosafiri sana ndani ni *VP 1* na *VP 2.* Nyinyi nyote mpo hapa, kuna CCM kuna *CUF*, hapa msikae mkajibizana kisiasa, humu ndani tuangalie ile hali halisi hasa *VP1* na *VP 2* ndio wanaosafiri sana safari za ndani ni milioni mia tano (500 *millions)* kwa mwezi lazima niziweke.

Safari za nje za viongozi. Nyinyi wenyewe jiulizeni, Rais mwenye dhamana anasafiri mara ngapi nje milioni mia saba na thalathini na mbili kwa wastani kwa mwezi (732 *millions)*, riba na marejesho ya mikopo milioni mia sita na hamsini (650 *millions)*. Malipo ya umeme ya vituo vya maji lazima niwalipe

*TANESCO* milioni mia tano (500 *millions)*, nalipia mimi nazipeleka moja kwa moja wapeleke *TANESCO, ni* milioni mia tano.

Pencheni milioni mia nane na tisini (890 *millions)*, chakula cha viongozi milioni mia na arubaini (140 *millions)*, kiinua mgongo milioni mia nane na thamanini na sita (886 *millions)*, kutoka katika Mfuko Kuu wa Serikali ni bilioni nne nukta tatu tisa nane (4.398 *billions)* lazima nizitoe. Kwa hivyo, katika ile thalathini ( 30 *billions)* ukijumlisha na mishahara bilioni kumi na tisa nukta saba (19.7 *billions)* tayari zimekwisha, bado sijamaliza.

Ruzuku ambayo ni lazima niitoe kwa zile taasisi ambazo zilizopata ruzuku *2.8 billions*, matumizi ya kawaida ya lazima sasa nazungumza ya lazima, Mnazi Mmoja *Hospital* kila mwezi nawapa milioni mia moja ( 100 *million)* ku-*advance* halafu yale mapato yao wanayoyakusanya sidhani kama hata yanafika milioni 40.

Wizara ya Afya ku-*fast track* mambo yao milioni hamsini (50 *millions)* lazima wapewe. Chakula cha vikosi milioni mia mbili na kumi na mbili (212 *millions)*, wagonjwa ninaowapeleka nje kila mwezi wastani wa milioni mia tatu na thalathini na tano ( 335 *millions)* ambao ni wananchi wetu masikini.

Wizara ya Wanawake na Watoto lazima niwape milioni ishirini na tano nukta ( 25 *millions point something)* kwa ajili ya msaada wa wazee kila mwezi na matumizi ya maendeleo ya lazima 2.6 *billions.* Jumla zote nilizokutajieni hizo ni za lazima *25.82 billions* katika bilioni thalathini, umebakiwa na bilioni nne nukta moja nane (4.8 *billions)*. Hizi ndizo tunazogawana kwenye *OC's*.
Lakini nataka niseme Mhe. Spika, Wizara ya Fedha haina mamlaka ya kumpangia Katibu Mkuu *OC* yake aipeleke vipi, yaani hatuna mamlaka hayo sisi. Tukishampa Katibu Mkuu milioni zake mia nne hizo kwenye *OC* yeye ndiye anaangalia kipi kipaumbele, na tumepitisha hapa kwenye bajeti. Fedha za likizo ziko kwenye *OC,* kama wizara haitaki kulipa mfanyakazi wake likizo si jukumu la Wizara ya Fedha kwa sababu *OC's* zipo hapa kila mwezi na kila wizara wanapata kutegemeana na mapato tunayoyakusanya.

Waziri akiona safari ya kwenda nje ni muhimu kuliko kumpa pesa za likizo mfanyakazi wake ni jukumu la kwake na si la Wizara ya Fedha, mimi kazi yangu kuwapa *OC's,* wao wenyewe ndio wanaweka hizo *priorities*. Nilikuwa nasikiliza tu hapa mimi tokea tumeanza kila anayekuja Wizara ya Fedha haikunipa fedha. Hilo Mhe. Spika, nataka niweke utaratibu Waheshimiwa Wajumbe hawa wa Baraza lako Tukufu wafahamu jukumu langu mimi kama Wizara ya Fedha ni nini.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ninapoweka kodi na ukaipitisha kwenye Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, na nikaweka dhamira ya kodi ile kusaidia suala fulani tokea nimeingia Wizara ya Fedha huwa nasimamia jambo hili. Tusitangaze kodi hapa halafu wananchi kule wakapata *impression* kuna kodi inakwenda kwa ajili ya kitu fulani halafu sisi tusiipeleke.

Yalikuja mawazo hapa tumetoza kodi kwa ajili ya madawati hatujapeleka. Sasa nataka niseme mwaka jana tuliongeza kodi kwenye *Seaport Service Charge* na tukakubaliana hapa kwamba pesa hizo ziende kutengeneza madawati, makusanyo yote ya fedha hizo.

Bajeti ya mwaka jana hii 2013/2014 ilikuwa ni *two point two five four billions* (2.254 *billions*) makusanyo ya fedha hizo zote. Wizara ya Elimu nimewapa fedha kwa ajili ya kutengeneza madawati *two point five five three nine billions* (2.5539) asilimia 113. Mungeliwauliza huko madawati yako wapi? (*Makofi*).

Mhe. Spika, madawati ya pesa za mwaka jana yako wapi. Ninakuja tena mwaka huu, nyinyi munauliza pesa tu, hamuulizi kile kilichotokewa kutengenezewa pesa hizo. Hapa ndiyo Baraza lako Wajumbe wako Mhe. Spika, wanapotakiwa kuhoji! (*Makofi*)

Mwaka huu makusanyo yote tumeyafanyia makisio kwa ajili ya kodi hii muliyonipa, tutakusanya *two point eight four billions (*2.84 *billions).* Wizara ya Elimu nimeshawapa o*ne point eight four billions* (1.84 *billions)* asilimia 66 nishawapa mpaka Februari. Waulizeni madawati yako wapi?(*Makofi*)

Mimi Mhe. Ali Juma Shamuhuna ninamuheshimu sana. Mhe. Spika, Shamuhuna Waziri wangu amenilea miaka saba, lakini mimi nataka niwape *tips* Wajumbe wako nini wafanye. (*Makofi*)

Sasa ningelikuombeni basi mukienda huko, hebu jaribuni kabla hamujaenda kwenye kamati mukapita Wizara ya Fedha kwanza mukapata taarifa kidogo, halafu zitakusaidieni. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Spika, limekuja wazo hapa, suala limeulizwa hapa Utumishi. Wizara ya Elimu wamewatupia nyongeza za mishahara Wizara ya Fedha. Nimesikiliza kuna Mjumbe mmoja kasema tokea mwaka 2012 Wizara ya Fedha hawajajibu bado barua hiyo na hawajatekeleza, kuna nini Wizara ya Fedha?

Mhe. Spika, *with due respect*, Wizara ya Elimu wameniletea barua mwezi wa Februari mwaka 2015. Hiyo ndiyo barua niliyoipata mimi mwezi Februari, 2015 inahitaji *two plus billions* (2 *plus billions)* kwa mlolongo kama huu niliokuelezeni wa mapato, kweli nitazitoa kwa mwezi mmoja jamani? Sitoweza!

Lakini tuna utaratibu muafaka walimu, ma-*nurses* ukiwapangia kwenye vituo na kama hukuwa muangalifu wa kum-*trace* utalipa mshahara yeye hayupo kwenye kituo kile, hayupo kabisa. Tunajaribu sasa hivi kuwa *very careful* kuwaangalia hawa waliopelekwa, walioajiriwa, kwamba wapo kwenye vituo vyao. Lakini kwa taarifa nilizozipata *adjustment* za mishahara zimeshafanyika, kilichobakia ni haya madai yao ya nyuma, na tayari tumeshaandaa utaratibu wa kuanza kuzitoa na tutazitoa kabla hata hatujaingia kwenye bajeti nyengine, tutakuwa tumeshaanza kuzitoa kidogo kidogo ili waanze kulipwa.

Lakini ninachosema kwamba wanapouliza watu waulize na tarehe, tarehe gani mumepeleka. Niliwaambia watu wangu wanipatie barua hasa nije nikusomeeni hapa hiyo barua. Hilo Mhe. Spika, ni jengine ambalo nilikuwa ninataka niliweke wazi.

Jengine ambalo nataka wazi hili la *PBZ*. Limeulizwa hapa, wengine wamelichangia kwa nguvu zao zote, wengine wamesema kwa nguvu zao zote. Mimi nataka taasisi hii ninayoisimamia ing'are, iking'ara *PBZ*, atang'ara Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, aking'ara Katibu Mkuu nitang'ara na mimi Waziri wa Fedha, lakini nyinyi mukishakuambiwa tu kwamba tunataka pesa kwa ajili ya *capitalization*, tuna ushindani, kuna nini, Wizara ya Fedha haitaki kutupa basi, hamuendi tena hapo. Mukishakusikia fedha hazitoki Wizara ya Fedha hamuendi tena *deep* kuuliza.

Sasa ngojeni basi nikwambieni. Mimi nilikuwa ni mjumbe mmoja katika wale wajumbe ambao walioteuliwa kufanya *reforms*. Mimi nilikuwemo katika ile Kamati. *I feel so proud* kwamba kazi yangu niliyoifanya leo kuna matunda haya ya *PBZ*. Tumekaa nao mwaka jana, wameanza kuzungumzia kuhusu habari wanataka bilioni arobaini (40 *billions)* kwa ajili ya *capitalization*. (*Makofi*)

Tukawaambia watuletee *details*, wanataka kuzitumiaje hizo bilioni arobaini (40 *billions)*. Sehemu kubwa ya bilioni arobaini wanataka kujenga Makao Makuu. Nyinyi mumezungumza ushindani wa mikopo sijui, sijui nini wa mikopo. *PBZ* ile miaka minne mfululizo, hailipi kodi kama mabenki mengine yanavyotakiwa na sheria ya *BOT,* na ile *dividend* tumewaachia.

Mwaka jana *PBZ* ametengeneza faida, mwaka juzi ametengeneza faida bilioni sita ( bilioni 6). Bilioni sita akitoa kodi, kama bilioni nne na kitu hivi zinabakia za kwake. Mwaka jana tumetengeneza faida bilioni kumi ( bilioni 10). Kwa nini hizi asizichukue aka- *plow back*, anatafuta, lazima Serikali itoe wakati Serikali yenyewe ishakutajieni mapato yake.

Nimewaambiwa watu wangu, mimi taasisi ninazozisimamia nikiona kwamba inahitaji msaada, nitaisaidia, kama haihitaji msaada nitasema wewe huhitaji msaada sasa hivi. Nimewaambia watu wangu kwanza tupeleke *special audit* pale *PBZ*, tuone matumizi yao kwanza. Sio kuanza kufikiria *capitalization* tu.

Kwa hivyo na hili nalo muliangalie. Sehemu ya kubadilisha mfumo wa *system* tumesema kwamba hili tutawasaidia ili *system* ile tuibadilishe. Kwa hivyo ndugu zangu suala la *PBZ* sio kwamba hatulitaki, lakini kwanza fedha hatuna, lakini na wao haya wanayoyapata mapato yao kwanza waanze kuyarudisha kule badala kufikiria kupanuka tu kutaka kujenga tu, kila pahala wanataka kujenga. Huwezi ukajenga ukakodi kwa bei ghali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni maslahi ya watendaji wa Bima. Hili sina maneno makubwa. Wametakiwa kupeleka Utumishi na sisi tunawasaidia. Ni kweli maslahi ya watendaji wa Bima ni madogo kweli. Hili tutawasaidia kwa sababu fedha zao wanazo, tutazungumza zaidi na Utumishi waweze ku-*release* ili wawafanyie maslahi yao na wale watendaji wasiweze kutukimbia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine ambalo nitakalolitolea maelezo ni *ZSSF*. Ni kweli kama hatukuwa na tahadhari, miradi hii inayoekezwa na *ZSSF*, kama hawakuwa na tahadhari tunaweza tukajikuta Serikali ikalipa. Wazo hili mimi nimelipokea na sasa hivi ninaliangalia kwa undani zaidi. Ninamshukuru Mwenyekiti mpya wa Bodi aliyeteuliwa na yeye ana mtazamo wa *investment* ambazo zina tija. Kwa hivyo nimemwita Mwenyekiti mpya wa Bodi na *management*, nimeomba nikutane *second week* ya mwezi wa Aprili tuzungumzie masuala haya. Na ameshanijibu Mwenyekiti yupo safarini lakini akirudi atakuja, ninataka Mwenyekiti na Bodi kuhusu haya. Kwa hivyo, hilo tumelipokea.

Mhe. Spika, jengine ambalo ninataka nilizungumzie hapa kuhusu *ZUSP*. Mhe. Spika, *ZUSP* kuna miradi mingi sana mule ndani, karibu miradi sita imo mule ndani. Kuna ukarabati wa jengo la Manispaa, kuna utiaji wa taa za njiani Mji Mkongwe, kuna *Sea Wall* Forodhani kujenga ukuta, kuna masoko Pemba na kuna mtaro.

Ni kweli, lazima pale pahala ambapo pamekwenda kombo tukubali yamekwenda kombo. Utendaji wa *ZUSP* hata mimi sikufurahika nao. Nimekuwa nikipata taarifa *time* nyengine zinanisikitisha. *Time* nyengine ninasema hata ile *Tender Board* inayosimamia *ZUSP* niivunje niiunde nyengine. (*Makofi*)

Habari nyengine ni ovyo tu, ovyo tu. Hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hili nitalisimamia, lakini ninataka niseme tu mtaro umechelewa kwa sababu ya *design* ya mwanzo iliyochorwa ilikosewa. Msimamizi mpya amekuja ametengeneza *design* nyengine. Lakini tayari tumeshakamilisha *evaluation* imeshakamilika, imeshapelekwa *World Bank*, tunasubiri *no objection*, tunatarajia mradi huu utaanza kwa ukamilifu mwezi wa Mei na ujenzi utachukua miezi kumi na nane (miezi 18). *(Makofi)*

Mhe. Spika, mradi wa ujenzi wa Uvunje na Vunjo. Mhe. Farida Amour Mohammed nimekubali maombi yako. Nadhani nitakuja Pemba, tutakutafuta na wewe tutazungumza na wananchi. Nasaha zangu kwa wananchi wa Zanzibar, kila penye mradi wenye tija tusiukatae, na kama kuna kasoro wananchi tueleze kasoro za ule mradi ili Serikali iingilie kati, lakini tusikatae. *(Makofi)*

Na ugomvi hautatupa faida yoyote baina ya wananchi na wawekezaji. Nitakuja kama nilivyofanya kwa soko la Tumbe na tukafanikiwa vizuri na sasa soko linafanya kazi vizuri na kwa mradi huu nitakuja mimi na uongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na uongozi wa Wizara yangu ili tuje kwa pamoja tuzungumze na wananchi katika mradi huu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mashine za kulipia. Hili kwa kweli tunalihimiza haraka sana na tunazitaka haraka sana. Ni wajibu wetu kuliharakisha hili ili tuweze kufanikisha ulipaji wa kodi kutumia mashine hizi.

Deni la *TANESCO* liliulizwa vile vile hapa. Sisi jukumu letu tumeshawaandikia Serikali ya Muungano, tunakudaini bilioni kumi na nane (bilioni 18), bilioni kumi na nane zipelekeni kupunguza deni la *TANESCO.*

Mimi nimemuandikia Waziri wa Fedha Marehemu Mgimwa, timu hii iliyopo nishakuwakumbusha na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kamuandikia Waziri Mkuu. Sasa sisi kwetu tumeshalitoa bilioni kumi na nane (bilioni 18). Ni wajibu wao kufuata utaratibu na kuzilipa.

Tarehe kumi tunakutana na Mhe. Waziri wa Fedha wa Muungano hapa Zanzibar, nitalikumbusha zaidi ili wao waandae ule utaratibu wa kifedha tuwalipe hilo deni la bilioni kumi na nane (bilioni 18), wakati sisi huku kwetu tumeshaanza tumelitoa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mambo ni mengi tumeyakusanya yote. Hapa nimejibu machache tu lakini naomba nimalizie mawili ya mwisho.

Waheshimiwa Wajumbe tusaidiane sana, na ukikaa kiti cha Wizara ya Fedha ndiyo utaona. Dkt. Mwinyihaji ninayoyasema anayaona hasa, maana kakaa zaidi ya miaka minane pale na sasa hivi nikiondokaondoka yeye ninamwambia akaimu.

Mhe. Spika, wazee hapa wamezungumzia suala la mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wetu. Hebu tujiulize lengo hasa ilikuwa ni nini? Tulipoanzisha huu utaratibu wa kutoa mikopo kwa elimu ya juu kwa wanafunzi wetu, lengo lilikuwa ni nini, *Is it charity?*

Hebu tujiulizeni ilikuwa ni kama sadaka tu, kila mwenye mtoto anataka kupata sadaka. Ilikuwa Serikali baadae marudisho yarudishwe ndani, lengo ilikuwa ni nini? Mimi ninasema haikuwa sadaka, Sheria tukiisoma vizuri mutaiona. Wanafunzi wanatakiwa wapate mikopo lakini watakapopata ajira waanze sasa kurudisha mikopo yao. Na yapo pale matangazo kwenye Sauti ya Tanzania Zanzibar tunayasikia.

Niliwaambia wenzangu bahati mbaya hawajaniletea hiyo takwimu, tokea tumeanza kutoa hii mikopo Serikali imeshatoa kiasi gani. Hii mikopo tumeanza zaidi ya miaka kumi sasa hivi kama kumbukumbu zangu ni sahihi. Ikiwa kila mwaka tunatoa bilioni moja (bilioni 1) , zaidi ya bilioni kumi (bilioni 10) tayari tumeshatoa.

Lakini hebu mukienda huko muulizaneni makusanyo kiasi gani. Nyinyi munakimbia kutoka tu, hebu tujiulizeni tukienda kule tumeshazikusanya kiasi gani na zile pesa hazirudi Hazina, tumekusudia kufanya *revolving fund,* na kama hatukuwa *serious* katika kuzikusanya hizi pesa, *revolving fund* haitofanikiwa, kila mwaka mutatenga bajeti zitakwenda. Watoto ni wetu, sisi ndiyo wazazi, hatusimamii urudishaji wa hizo pesa. Kwa hivyo ninataka tushirikiane katika kusimamia.

La mwisho Mhe. Spika, nimesikia kwa ukaribu zaidi, nimesikia siyo siku moja siyo mara moja, siyo mara mbili malalamiko juu ya mradi wa *e-government.* Ninataka niseme maneno matatu tu kwenye hili.

La kwanza, lazima tukubali kwamba ule mradi ni mpya sana. Katika Wawakilishi tuliomo humu ndani thamanini, sitaki niseme hivyo kwa kejeli Mhe. Spika, *including myself*, tukipewa swali moja tu la *e-government* tujibu humu ndani zaidi ya asilimia 70 tutafeli. Tunafeli kwa sababu *something is new to us*. Na kitu chochote kikiwa kipya basi hata uelewa wake saa zote tunakuwa tunapata shida.

Lakini mradi huu Mhe. Spika, walioanzisha wameanzisha kwa nia safi kabisa, na kama kuna kasoro, kuna kamati sasa hivi tunazifuatilia hizo kasoro. Kitengo cha *e-government, ZANTEL*, mimi mwenyewe nimo na Mhe. Waziri wa Habari jana amezungumza vile vile, tunazifuatilia ili tuweze kuzirekebisha hizo kasoro.

Mwaka juzi katika bajeti ya 2012/2013 nimeeleza *break down* ya matumizi ya zile pesa Dola milioni ishirini (Dola milioni 20). *Hansard* ipo isipokuwa katika *training* tu iliandikwa hamsini milioni, ni *fifty thousand Dollars* (50000) kwenye ile *component* ya benki.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninataka niwaombe tu Waheshimiwa Wawakilishi wa-*keep trust*, tuaminini Mawaziri, pale tutakapokuwa tumefanya vibaya tumekosea tukosoeni, mukihitaji kutufuata ndani ya maofisi yetu njooni tutashirikiana katika kutekeleza majukumu yetu. Serikali ni yetu sote, tunawatumikia wananchi sote, hakuna haja ya kushutumiana.

Ninamalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, na ninataka niwaambieni tu kwamba chombo chetu hichi tukiendesheni vizuri sana wala tusilumbane kisiasa, sisi sote tunajenga nchi moja, sisi sote tunawatumikia wananchi hao hao.

Mimi ningelifarijika sana tungelitumia lugha ya kuwaelimisha wananchi zaidi kuliko lugha ya kuonekana sisi tunaanza kulumbana lumbana wenyewe, mambo ambayo hayana msingi wowote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa hakuna utaratibu. Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa maelezo uliyotoa lakini ninakushukuru zaidi kwa maneno ya mwisho uliyoyasema kwamba tupo hapa kujenga kwa ajili ya wananchi sote. Hili ni suala muhimu ambapo tulizingatie ili shughuli zetu zote ziwe zinatuelekeza katika kuwasaidia wananchi.

Waheshimiwa Wajumbe muda umefika tukapumzike lakini niwaombe Waheshimiwa Wajumbe jioni saa kumi na moja tufike kwa wingi, *quorum* itimie, wanapata tabu sana, na kwa kweli siyo halali kufanya maamuzi chini ya *quorum*.

Mara nyingi huwa nahangaika sana tunapokaribia kufanya maamuzi, kuwatuma vijana kutoa matangazo, ili tuhakikishe kwamba tunafanya maamuzi yetu kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

Kwa hivyo, jioni tuna nafasi ya kuwasikiliza Waheshimiwa Mawaziri wawili; tutaanza na Waziri wa Kilimo na kumalizia na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, baadaye tumwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ili ahitimishe na tupitishe jambo hili hapo jioni.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe, ninaahirisha kikao hichi hadi saa kumi na moja jioni, leo.

*(Saa 6:58 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni kikao kilirejea)*

*(Muda mfupi baada ya wajumbe kuingia umeme ulizimika)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, umeme ulikuwa umekatika kwa muda tu ni matatizo ya kawaida, lakini tumearifiwa kwamba sasa tunaweza kuendelea. Katibu.

## HOJA ZA KAMATI

**Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2014/2015**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili):** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nikushukuru Laasiri hii ya leo kwa kunipa wasaa wa kufanya majumuisho kwa hoja mbali mbali walizozungumzia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza letu tukufu, wakati wakichangia ile hoja ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo, pamoja na yale maagizo waliyonipa.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo, kwa kuwasilisha vizuri na kwa umakini ile hotuba au ripoti ya kamati yetu.

Mhe. Spika, ripoti ilikuwa na mengi imezungumzia yale waliyoyaona katika ziara na katika majumuisho yetu. Lakini kwa jumla mazungumzo yetu takriban kwa kipindi chote kilichopita. Mawazo yao mengi tumeyachukua, tunashukuru kama kawaida tutajitahidi tuyazingatie na wao wasichoke tuzidi kubadilisha mawazo. Tutaona Mhe. Spika, na yeye mwenyewe kwamba tujitahidi kuyajibu kadiri ya uwezo wetu yale maagizo yao, naamini yametusaidia sana katika kufanikisha utendaji wa wizara yetu.

Kwa ujumla Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Waheshimiwa waliochangia ni pamoja na mwenyewe aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti na Mhe. Naibu Waziri ni jumla 13. Naomba niwatambuwe mmoja baada ya mwengine. Kwanza kabisa kama nilivyosema ni:-

1. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Kwa niaba ya Mwenyekiti
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohammedraza Hassanali
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
8. Mhe. Raya Suleiman Hamad
9. Mhe. Farida Amour Mohammed
10. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
11. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
12. Mhe. Salma Mohammed Ali
13. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili

Mhe. Spika, naomba nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Naibu Waziri, kwa kweli mengi ya masuala au hoja kutoka kwa wajumbe amezijibu vizuri, kwa kifupi na kwa ufasaha na nafikiri Waheshimiwa Wajumbe wameridhika na majibu yale, kwa hivyo, mimi sitorudia tena na wao zaidi wamekazia na pale ambapo labda walitaka kufahamu Mhe. Naibu Waziri kwa kweli alizidi kusisitiza.

Mhe. Spika, nianze na Mhe. Mjumbe aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti, ambaye alizungumzia suala la ule mradi wa *MIVAP* wa miundombinu ya masoko katika wilaya zetu na akazungumza suala la mavumbi katika utayarishaji wa zile njia na alisema kwamba imekuwa kero.

Mhe. Spika, ni kweli, unajua wakati wa ujenzi ni lazima tukubali vumbi linakuwepo, lakini alisema hata baada ya ujenzi ile *material* yenyewe iliyojengewa kidogo sio nzuri, inakuwa vumbi tu. Sasa suala hili kwa kweli wizara yetu tumekaa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Mfuko wa Barabara, kwa pamoja tumekubaliana hilo tatizo tushirikiane ili tulitanzuwe kwa barabara zile kutiwa, wanaita ile lami chafu au lami nyepesi. Nafikiri suala hilo linafanyiwa kazi na *Inshaallah* litatekelezwa ili hilo tatizo liweze kuondoka.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Mhe. Mjumbe alilizungumzia kwa niaba ya Mwenyekiti, na ambalo halijajibiwa ni suala lile la magodauni au *stores* za ghala ya vyakula. Kweli ni suala muhimu na hili kama Serikali na kama sera yetu tumeshaamua kwamba lazima tuwe na *strategies then resolve,* kama wenzetu Bara wanavyofanya na sisi kwa kuanzia basi wizara imeagizwa na Serikali, zile ghala za Malindi pale mbili zilizokuwa za Wizara ya Kilimo na Maliasili, tuzichukuwe halafu tuzikarabati kwa ajili hiyo. Kazi hiyo Mhe. Spika, inaendelea vizuri na *Inshaallah* baada ya muda sio mrefu kazi hiyo itakamilika.

Kwa hivyo, naomba kumuhakikishia Mhe. Mjumbe aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti, kwamba agizo lake alilotupa, hilo tunalichukua na tutalifanyia kazi ipasavyo. Suala la Razaba alilizungumza Mhe. Naibu Waziri kwa ufupi, lakini naomba nitilie mkazo tu kwamba ni kweli kuwa lile shamba letu liliopo Razaba wamekabidhiwa Chuo cha Kilimo Kizimbani. Wizara inaendelea kufuatilia upatikanaji hati miliki pamoja na kupanga matumizi bora ya shamba hilo. Kwa kuzingatia uzito wa suala hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanizbar ilipeleka ujumbe mzito ukiongozwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa ajili ya kushughulikia ipasavyo suala hilo la Razaba hivi karibuni.

Mhe. Spika, baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwasilisha ripoti yake serikalini, basi Serikali imeagiza kwamba Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Waziri wa Kilimo na Maliasili waende kule Razaba na timu nzito ya wataalamu, kwenda kupanga mipango madhubuti ya kuliendeleza na kulifufua shamba lile. Kwa hivyo, ninachoomba kwa kweli tuwe wastahamilivu, sasa tumedhamiria kwa makini sana tulifufuwe shamba lile na tuone kwamba linaleta tija kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Mhe. Mjumbe aliyewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti, alilizungumza ni suala la Kituo cha Utafiti Kizimbani, alitusisitiza kwamba kituo lazima kifanye kazi zake kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, tunakubaliana na ushauri wake. Nataka kusema tu kwamba hivi sasa tumo katika taratibu za kukamilisha Kanuni, hizo Kanuni zikishawekwa na kama ilivyoagizwa mwanzo, basi tutajitahidi kupanga hadudi rejea kila mmoja ajuwe wajibu wake na Kanuni nazo zitafuata mkondo wake. Kwa hivyo, ushauri wake kwa kweli tumeusikia na tutajitahidi kuona kwamba hilo tunalitekeleza mapema iwezekanavyo.

Mhe. Mjumbe mwengine alikuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wa Kitope, kwa kweli tunamshukuru sana kwa michango yake mingi, yenye ufasaha na ambayo mengine aliifuatilia vizuri, lakini mingine ilitolewa maelezo kwa ufasaha na Mhe. Naibu Waziri, sitopenda kuirejea. Lile suala la Kiwanda cha Sukari na lile la kiwanda cha kutengenezea maziwa kwa kutumia kokwa za fenesi, nitamwachia Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko aje atolee maelezo, yeye ana uzoefu mzuri wa viwanda hasa hivyo vya kutoa maziwa.

Mhe. Mohammedraza Hassanali, tunakushukuru sana kwa michango yako na uzoefu wako katika masuala haya ya biashara. Wewe pia una mabonde kule Mchangani na mabonde ya Uzini. Kwa hivyo, masuala ya mpunga najua unajukumu la kusimamia kilimo ipasavyo. Kwa hivyo, tunakushukuru kwa mchango wako.

Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe na wewe pia tunakushukuru, ulizungumza suala la ajira na Mhe. Naibu Waziri alilijibu vizuri tu. Kubwa ambalo nataka nilijibu ni lile suala ulilouliza kuwa mbegu ya nerika iko wapi, imepotea ilikuwa nguvu ya soda tu. Nataka kukuambia Mhe. Salim Abdalla, kwamba suala la mbegu ya nerika haikuwa nguvu ya soda tu, ni kweli.
Labda ulijuwe tu lile jina lenyewe nerika linasimama kwa niaba gani, ile kwa Kizungu wanasema ni *new rice variety for Africa.* Yaani ile ni mbegu mpya ya mpunga iliyopendekezwa kwa Bara zima la Afrika, na mbegu ile kule katika kituo cha utafiti wa mbegu za mpunga Godiva ndiko walikoitowa na ile ni mbegu ya juu ya mpunga. Unajua mpunga uko wa mabondeni na uko wa juu. Pemba tunaita Mtemani kule.

Sasa tatizo lililotokezea ni kwamba tuliipanda mbegu ile mabondeni, tulipoipanda mabondeni mpunga ukazaliwa kwa wingi sana, kwa bahati mbaya wote ukajakuzama kwa maji. Kwa hivyo, kama nilivyosema uzuri wake kwamba ule ni mpunga wa juu, *up plant rice*. Kama unavyoupanda muhogo, mgomba na tena unastahamili ukame, hiyo ndio sifa yake nyengine kubwa kabisa.

Sasa hapa kati kulikuwa na tatizo la mbegu, ni kweli. Lakini nataka kuwajulisha tu kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi sasa imefarijika kuona kwamba wakulima hususan wa Pemba wamehamasika katika kuzalisha mbegu hiyo. Katika msimu uliopita wizara ilinunua jumla ya kilo zipatazo 234 za nerika kwa ajili ya kuzisambaza kwa wakulima wengine. Hata hivyo, tunapenda kuwasisitiza wakulima kuwa mbegu hizi zinaimarika zaidi katika kilimo cha juu na sio cha mabondeni, suala hili naomba sana wakulima walifahamu na tujitahidi sana kujua.

Mhe. Spika, wewe huwezi kuamini Bambi kwenye jua kwa Mhe. Mohammedraza kule uliota mpunga ule ukazaa, Mtende juu sio bondeni juu kabisa. Pemba kule kama nilivyosema mabonde ya Mtemani, kule ndiko unakonawiri vizuri, lakini ukipata maji haukubali vizuri. Sasa hapo kidogo wakulima wetu walikuwa hawajafahamu. Lakini sasa Mhe. Spika, tunajitahidi kuwafahamisha na tunakwenda nao vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye kubwa alizungumza suala la kusarifu mazao pale Kizimbani. Nafikiri sitaki kurejea maelezo mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri. Pia, Mhe. Hamza Hassan Juma, ulizungumza hivyo hivyo.

Mhe. Bi Raya Suleiman Hamad, ulizungumza kwa urefu suala la Razaba, utafiti wa Kizimbani na waliostaafu nayo pia Mhe. Naibu Waziri niseme kwamba aliyajibu. Lakini nasikitika sana suala la wakulima kuchimbuliwa mapema. Nakubaliana na wewe ni kweli, lakini tatizo linalotokezea ni kwamba wakulima wanachelewa upande mmoja na wao kuchangia kile walichotakiwa wachangie, takriban nusu basi wanachelewa kwenye kukaa pamoja kwenye Jumuiya zao. Sasa kwa kuwalimia kwa mmoja mmoja, kwa kweli haighalisi vizuri. Kwa hivyo, ninachowaomba sana mtusaidie wakae pamoja vizuri, wachange pesa zao inakuwa rahisi matrekta kuja kulima kwa mara moja. Lakini ushauri wako uliotupa tunashukuru tunaupokea.

Mhe. Farida Amour, kwa ujumla na wewe tunashukuru kwa maelekezo yako. Mhe. Abdalla Mohammed Ali wa Mkoani na wewe pia tunakushukuru. Mhe. Bikame Yussuf Hamad, kuhusu suala la magari yale ya vifusi na michanga. Tulieleza ule utaratibu wa bei tulipojibu zile hoja au maagizo.

Mhe. Salma Mohammed Ali, tunakushukuru suala la sare Mhe. Naibu Waziri kalieleza vizuri, sitaki kulirejea. Lakini nataka kusema tu kwamba kwa kweli kwa upande wa vifaa vya matrekta, unasema wewe mwenyeji wa Machomane pale. Nataka kusema kwa upande wa matrekta, kwa kweli wizara ilitoa tenda ya vifaa vya matrekta vinavyogharimu shilingi milioni 545, ambavyo viligaiwa kwa Unguja na Pemba.

Aidha, kwa suala hili naomba nitowe shukrani za dhati kabisa kwa Wizara ya Fedha kwa kuona umuhimu wake, walitupatia fedha hizi na tukafanya kazi nzuri sana. Lakini kwa kweli mahitaji yamekuwa makubwa, matrekta machache na tunajitahidi matrekta hayo nayo angalau kila sehemu yaenee. Lazima tutambuwe yale matakwa ya kila mmoja kuona anataka kulima kwa trekta. Kwa kweli hayo mahitaji yamekuwa makubwa, lakini tunawashukuru Wizara ya Fedha wamejitahidi kutupatia fedha hizo na tukatengeneza kwa mapema, lakini uchakavu wa matrekta nayo unachangia pia na kuchelewa.

Mhe.Salma Mohammed, ulizungumzia suala la *greenhouse*. Nataka kuwajulisha kwamba kwa upande wa kilimo cha mboga mboga ambacho umekizungumzia, wizara imejitahidi kuelimisha na kuwahamasisha wakulima wa mboga mboga juu ya uzalishaji wa mboga kwa kutumia *greenhouse*, kwa kupita mradi wa *Tanzania Horticultural Association (TAHA)*. Pia na *Zanzibar Agriculture Investment Development* au (*ZAID*).

Madhumuni ya matumizi ya *greenhouse* ni kuongeza uzalishaji katika eneo dogo. Aidha, *greenhouse* inahifadhi unyevu pamoja na kukinga mimea na maradhi na wadudu. Kwa kweli mboga mboga sote tunajua wadudu wanazipenda sana na maradhi. Sasa *greenhouse* zile zinasaidia sana kujikinga na wadudu na maradhi, ndio hasa madhumuni yake.

Kwa hivyo, wakulima wamehamasika sasa, wanazinunua wenyewe na wanaziendeleza, sisi kama wizara tunajitahidi kuwapatia elimu ili waweze kuzalisha vizuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kweli mengi ameyajibu yale maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nisiongeze zaidi nikaharibu mambo. Lakini ninachowaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kilimo bado tunakitegemea, hasa kwa upande wa chakula kwa nchi yetu, vipando vya juu, vipando vya bondeni kwa mpunga.

Kwa hivyo, kama wawakilishi tuna wajibu mkubwa sana wa kuwahamasisha wakulima katika mabonde yetu kuzalisha kipato. Tunachotaka sasa ni kilimo cha tija, tuone kwamba kilimo kinaongeza pato la mkulima na pato la mwananchi, tusichukulie ile dhana ya zamani kwamba ninalima tu kama *hobby,* hapana. Mfano mzuri sasa, tizama kilimo cha mboga mboga kama matunda, matikiti maji yalivyokuwa na tija na yanavyopata soko. Utashangaa wewe unavyoyaona yanateremshwa kwa mafuso. Zamani tukisema yanatoka Bara tu, leo hapa hapa yanazalishwa. Ukienda Chonga kule kwa Mhe. Abdalla Juma, ukija zako Mchangani, kwenye mabonde mengi wanazalisha, hasa kipindi kinachokuja cha kipupwe ndio zaidi.

Kwa hivyo, lengo letu Mhe. Spika, ni kupata tija kwa wakulima wetu. Kwa hivyo, naomba sana waheshimiwa kilimo tukikazie sote katika majimbo yetu, ni suala la kufa na kupona, tuone kwamba kweli tunapunguza mzigo wa kuagiza chakula kutoka nje.

Mhe. Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, naomba tena kukushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuja kutoa maelezo ya ziada kufuatana na maelezo na maswali mbali mbali ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameyatoa hapa. Kwa hivyo, naomba kwa ruhusa yako nianze kutoa maelezo kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, yote ambayo ni miongozi tumepewa na Waheshimiwa Wajumbe, tunayachukua kwa udhati kabisa, mashauri yao ni mazuri na tutayafanyia kazi na ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wote wataridhika na kazi tutakayoifanya.

Lakini la pili, ningependa kuwashukuru wale wajumbe wote ambao wamechangia katika ripoti hii, waliochangia katika ripoti zote ni zaidi ya 12, lakini waliotuchangia sisi Wizara yetu ni kama wafuatao:

Mhe. Viwe Said Abdalla, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mohamediraza Hassanali Mohamedali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Salma Mohammed Ali na vile vile namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri Biashara, Viwanda na Masoko kwa namna alivyoweza kutoa maelezo ya baadhi ya masuala ambayo kwamba yalikuwa yanahitaji maelezo kutoka kwa Wajumbe Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba lile suala ambalo amelieleza hapa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kuhusu habari ya kiwanda cha sukari. Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba, kiwanda kile kimo katika jimbo lake ningemuomba sana afanye ziara kidogo akatembelee hichi kiwanda, vile vile, akatembelee na yale mashamba ya kile kiwanda, hichi kiwanda yule muwekezaji wa kwanza Babuanji aliyekuwepo mwanzo yule ameondoka na kwa sasa kiwanda hiki kipo chini ya kampuni ya *Shanta Sugar Group Company* ambayo ni kampuni kubwa sana iko nchini India na vile vile, imewekeza Tanzania Bara.

Kwa hivyo, hii ni kampuni tofauti na ile kampuni ya kwanza, kampuni hii imefanya kazi kubwa sana katika kiwanda kile, imeshawekeza jumla ya Dola milioni kumi, kiwanda kimetengenezwa, kimekarabatiwa vizuri, kimewekwa mitambo mipya na sasa hivi kimeanza kazi ya majaribio na kimeshazalisha sukari kiasi tani 200 za majaribio sukari nzuri kabisa ambayo kwamba iliuzwa katika masoko ya ndani na watu wote waliridhika kiwango cha sukari iliyozalishwa. Kwa hivyo, kiwanda hichi sasa hivi kinafanya kazi nzuri, mashamba yote ambayo yalikuwa katika milki yao kiasi cha ekari 3,565 ya Mahonda na Upenja yameshalimwa miwa kwa sasa na miwa hii itaweza kuvunwa na kuanza kufanya uzalishaji wa sukari hivi karibuni.

Hata hivyo, kiwanda kinahitaji zaidi ya eka 3,500 za ziada ili iweze kuzalisha sukari kiasi cha tani 250 kwa mwaka, kwa hivyo, kiwanda kipo katika hali nzuri ningemuomba Mhe. Makame Mshimba na wananchi wote wa Jimbo la Kitope kuwapa ushirikiano mzuri sana wenzetu hawa wa kiwanda cha Sukari cha Mahonda na wamefungua hospitali ambayo inahudumia wafanyakazi pamoja na wananchi.

Lakini vile vile imeanza *programmes* zake za kuotesha miwa kwenye mashamba ya watu binafsi, ambapo mpaka sasa hivi watu 25 wameshawapa mafunzo kwa kutumia ekari 75 kwa ajili ya kutoa *outgrowers* au kupewa *contract* kupanda ya kupandisha miwa na baadae kwenda kuwauzia kiwanda. Kwa hivyo, kazi nzuri imefanyika na kwa kweli ipo haja ya Zanzibar sote kuwaunga mkono kiwanda hichi ili kiweze kuendelea kuzalisha sukari ambayo itatusaidia uagiziaji wa sukari kutoka nchi za nje.

Napokea kwa masikitiko makubwa kwamba kuna wafanyakazi 40 ambao wamefukuzwa kazi bila ya kuzingatiwa haki zao, hili sijawahi kulisikia nimelisikia jana, lakini nitalichukua suala hili nitakaa na Waziri husika kwa pamoja mimi na yeye tutalishughulikia suala hili kuona kwamba wafanyakazi hao ambao kwamba hawakutendewa haki ili wapate haki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi yetu.

Nampongeza sana Mhe. Makame Mshimba, kwa jitihada zake za kuvutia kwa wawekezaji mbali mbali kwa kuja kuwekeza mpaka kufika hadi kutaka kufungua kiwanda cha kutengeneza maziwa kwa kutumia kokwa za fenesi. Naamini kwamba ubunifu wake kutaweza kutusaidia sana.

Nikiendelea mbele Mhe. Salim Hamad, ambaye aliongea na suala la mizani, kwa sasa hivi tumeshanunua mizani 14, mizani hizo zinapima mpaka robo kilo na chini ya robo kilo, tunaamini kwamba kwa muda mfupi ujao tutaweza kukamilisha zote mizani zinazohitajika na wauzaji karafuu wote watalipwa haki zao kwa mujibu wa mzigo waliopeleka. Sasa yoyote yule ambae kwamba akienda kituoni ataona robo kilo yake hakulipwa au nusu kilo yake hakulipwa, basi tunamuomba awasiliane na uongozi wa Wizara mara moja kwa ajili ya kumchukulia hatua mfanyakazi yoyote yule ambaye kwamba takiuka agizo hili. Hili ni agizo la Serikali hatutaki kuona mkulima wa karafuu yoyote yule karafuu zake zinachukuliwa bila ya kulipwa haki yake.

Jengine hoteli ya Makonywe tumemaliza kazi ya kujenga ukumbi, tumemaliza kazi ya kujenga uzio na katika bajeti inayofuatia mwaka 2015/16 bodi itakaa pamoja na watendaji wao na kuona gharama gani wataweza kuweka fedha za kuweza kujenga hoteli ya kisasa, hiyo ni moja katika azma ya *ZSTC* na naomba musiwe na wasi wasi, siwezi kutoa muda gani kwa sababu tumewaachia bodi ya *ZSTC* iamue, na hili ni agizo Mhe. Spika, la Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi, kwamba bodi ya *ZSTC* tumeipa kazi basi tuwaachie bodi wenyewe waamue ni lini waanzishe kujenga hoteli na hoteli hii imalize kujengwa lini. Lakini ni imani kwamba kwa muda mfupi ujao bajeti inayofuatia mwakani wataanzisha shughuli za ujenzi wa hoteli hiyo ya Makonywe.

Agizo la Nam. 14 kuhusu Mchukuzi kufariki na mambo mengine, naomba Mhe. Muwakilishi asiwe na wasi wasi. Katika sheria mpya ya karafuu katika Kanuni za karafuu tumeweka uzinduzi wa mfuko wa karafuu, mfuko wa karafuu huo utakuwa na fedha, fedha hizo zimezingatia kuwahudumia wale wote ambao kwamba wanalihudumia hili zao la karafuu, kwa hivyo, naomba Mheshimiwa siwe na wasi wasi wowote, hawa ni wafanyakazi wetu, tunashirikiana nao na tunafanya kazi nao, kwetu sie ni watu muhimu sana, tunawathamini sana na *ZSTC* itawashughulikia kupitia mfuko wake wa maendeleo ya karafuu.

Agizo Na. 16 kuhusu magendo ya karafuu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Muwakilishi Salim Hamad, kwamba hii *Task Force* ni viongozi ambao kwamba tumekaa pamoja tunaandaa mipango tu, lakini utendaji wote wanaotenda ni vikosi vyetu vya ulinzi na vikosi hivi vinafanya kazi sio kwa fedha zote kutoka *ZSTC* hapana. Sisi tunaongezea tu lakini vikosi vyote vinafanya kazi kupitia kazi zao na majukumu yao wamepewa na Serikali kupitia Wizara yao, sasa cha kusaidia ni cha ziada tu cha motisha cha kuwasaidia angalau waweze kufanya kazi hii kwa uzuri zaidi. Lakini utakuta kwamba gharama yoyote inatokana na *Task Force,* asilimia 75 inakwenda katika vikosi vya ulinzi, ni asilimia 25 tu zinatumika kwenye *Task Force.* Kwa hivyo, usiwe na wasi wasi *Task Force* haili pesa za karafuu.

Lakini *operation* ndio inayokula pesa za karafuu, nazo pia ukiangalia katika masuala ya hisabu za kibiashara ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na hasara utakayopata pindipo ulinzi wa karafuu kwa Taifa hili haukuwa mzuri. Kwa hivyo, vikosi maalum tunaviimarisha, viwepo barabarani na msimu ukisha tunaviondosha na wazo lake la kuweka vikosi kazi katika vijiji ni la muhimu sana, tunalizingatia, tunalichukua na itakuwa ni moja katika agenda ya kulizungumza katika vikao vya *Task Force* vitakavyofuatia. Tunamshukuru sana Mhe. Salim Hamad, kwa namna anavyoshughulikia suala hili la zao la karafuu na naamini kwamba katika jimbo lake linatoa karafuu nyingi sana na atashirikiana na Wizara yetu, ili kulinda zao hili lisipotee.

Nikienda kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, suala lake la biashara ya bidhaa za Unguja na Pemba kutokana na suala la bei, hili limesemwa na Waheshimiwa wawili Mhe. Raya Suleiman Hamad na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, kwamba Zanzibar ni Unguja na Pemba na sisi tusingependelea hata kidogo kuona kwamba bidhaa za Pemba zinakuwa ghali zaidi kuliko bidhaa za Unguja. Hii inatokana na kwamba kisiwani Pemba hakuna bandari ambayo kwamba inaweza kuchukua meli ya makontena na bidhaa nyingi huteremshwa hapa zikafikia kwanza Unguja, halfu tena zikapakiwa tena katika meli kutoka Pemba, hiyo husababisha kuwa na ongezeko la gharama za usafirishaji na uchukuzi kutoka Unguja kwenda Pemba.

Hata hivyo, tunapongeza sana wale wafanyabiashara ambao kwamba wanapeleka bidhaa zao kupitia bandari ya Mombasa kwenda Pemba, tunalowasihi ni kwamba walipe kodi za Serikali inavyotakiwa na ikiwa kuna kikwazo chochote kile watufuate na sisi tuko tayari kuwasaidia, tunaamini kwamba kuweza kufikisha mizigo kupitia Mombasa, gharama ya usafiri itapungua na kwa hiyo, bidhaa hizo zitakuwa na bei ndogo kisiwani Pemba. Ni shauri zuri vile vile kuona namna gani Serikali itachukua hatua ya kuona tunachukua hatua gani ya kusaidia wale wanaotaka bidhaa Pemba ili kuwe na tofauti hii ya bei baina ya Unguja na Pemba itasawazishwa. Hii ni changamoto tunaichukua naahidi kwamba tutaifanyia kazi.

Mhe. Raya Suleiman Hamad, naamini kwamba na wewe vile vile utatusaidia katika suala hili kwa sababu wewe ni mdau mkubwa kule Kisiwani Pemba, mara mbili tatu umeshanisikitikia kuhusu bei ya mchele kwamba imepanda na naamini kwamba tunaweza kushajihisha wafanya biashara wapeleke bidhaa zao kupitia Pemba kutoka Mombasa hii itasaidia sana kuondoa suala hilo. Lakini sisi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, haturidhiki hata kidogo kuona kwamba bei ya bidhaa Unguja na Pemba zinapishana. Serikali ya Zanzibar haioni raha kuona suala hilo na tutafanya kila liwezekanalo ili bei ya Unguja na Pemba iwe sawa sawa.

Jengo la *ZSTC* Dar es Salaam ni kweli jengo hili limekodiwa kama alivyosema Mhe. Bikame hapa na sisi tunasema kwamba tumeomba kwa wenzetu jengo hili watuuzie, lakini bahati mbaya mpaka sasa hivi bado hatujapata jawabu la kuuziwa, lakini sisi tunaendelea kuliomba na tumeiomba Serikali ya Tanzania Bara ituuzie jengo hili ili iwe ni mali ya *ZSTC* tuweze kulijenga kwanza iwe ni kitega uchumi cha *ZSTC* Dar es Salaam, lakini vile vile tutaweza kufanya biashara kubwa zaidi kuliko biashara ilivyo sasa hivi.

Mhe. Mohammedraza, tunakushukuru sana kwa namna ulivyotupongeza kwa kazi tunavyozifanya, lakini nataka nikuhakikishie kwamba tunafanyakazi hizi kwa mashirikiano makubwa na wafanya biashara wote wa Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wafanyabiashara wote wa Zanzibar kwa namna tunavyoshirikiana katika masuala yote ya kuleta bidhaa Zanzibar na vile vile kwa kushirikiana katika kuona kwamba bei za bidhaa haziongezeki kiholela holela. Kwa hivyo, wafanyabiashara wote nawapongeza na nakushukuru sana Mhe. Raza, kwa pongezi zako kwa Wizara yetu na naamini kwamba mashirikiano baina ya wafanyabiashara na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko yatazidi kuimarika siku hadi siku.

Mhe. Salma Mohammed Ali, ameeleza habari ya chumvi, chumvi kule Pemba kuna *NGOs* inaitwa *AZASCO,* hii *NGOs* ilipata msaada mwaka 1999 kutoka *UNDP* kupitia mradi wa *NIGP.* Jumuiya hii ina wanachama 56 ambao wote ni wazalishaji wa chunvi Pemba na wanauza kwa matumizi ya binaadam ikiwa na madini joto, kwa kuona idadi ya watu wanaotegemea kipato chao kutoka zao la chumvi kuwa ni wengi. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilitoa kazi kwa Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda yaani *TIRDO* kutoka Dar es Salaam, kufanya utafiti wa njia bora ya kujua usarifu wa chunvi unaofanywa na Jumuiya ya Uendeshaji ya *AZASCO.* Utafiti huo uliigharimu Serikali juma ya shilingi milioni 34. Kwa hivyo, Mhe. Salma, suala hili sisi hatujalipuuza na Serikali imeingiza fedha nyingi kabisa katika masuala ya utafiti.

Utafiti huo umeweza kugundua kasoro zilizokuwepo katika mbinu za ufanyaji wa chunvi na pia katika mzunguko wa mitambo wa kiwanda cha usanifu wa chunvi kilichopo Wawi Pemba, kwa hiyo, basi kufuatia utafiti huo *TIRDO* ilitoa mafunzo kwa wasarifu chunvi 25, vikundi 25 kati ya 56 tayari vilipewa mafunzo ya kuzalisha chunvi, kwa sababu wale walikuwa chunvi wanazalisha, lakini chumvi yao ilikuwa haina viwango, wengine wanavuna chunvi haijaiva, wengine wanavuna chunvi ishakwisha, yaani ishaiva mpaka ishakwisha ni makapi ya chunvi, kwa hivyo, walipewa taaluma ya kuweza kutoa chunvi ambayo kwamba itakuwa na viwango, juhudi hizo zote ni za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Biasahara, Viwanda na Masoko.

Si hayo tu, baada ya kupewa mafunzo yetu hayo, tukatoa tena vijana wetu hapa Zanzibar waendelee na utafiti wa kuangalia namna gani ya kuweza kuzalisha chunvi katika kiwanda kile, tumetumia fedha nyingi sana katika mfuko wa Wizara juu ya tafiti hizi na sasa hivi tunawashauri wafanye kazi kibiashara na sio ki-*NGOs* kwa sababu kile ni kiwanda na kiwanda kikubwa, lakini kiwanda kile bado kinahitaji baadhi ya mashine, mashine hizo gharama yake ni karibu shilingi 258 dola za Kimarekani. Kwa hivyo, wakiweza kujidhatiti barabara wakabadilisha uongozi wao wakafanya uongozi wa kibiashara, wakafanya kazi kibiashara, wakafungua *account* mabenki, wakaweza kupata mkopo na wataweza kununua mashine hizo ambazo kwamba wataweza kuzalisha chunvi ambayo itakuwa na ubora, chunvi itakayoweza kutumika kwa Wazanzibari wote hata kusafirisha katika nchi za jirani.

Kwa hivyo, Wizara yangu haitosita hata siku moja kushughulikia wazalishaji chunvi, haitosita hata siku moja kushughulikia kiwanda cha chunvi kwa sababu hizi ndio kazi zake na kadiri mfuko wa fedha utakavyokuwepo katika Wizara yetu, hiyo keki tunayopata tutagawana lakini tutaona kwamba tunaimarisha viwanda vidogo vidogo na vile vile kuimarisha taaluma kwa wajasiriamali wote Zanzibar ili tuweze kuanzisha viwanda vitakavyoweza kukua na baadae tuwe na viwanda vikubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mawazo yao waliyotupa na kwa changamoto hizo walizotupa, mmetupa kazi tunakwenda kuzifanya. Mashirikiano yenu nimuhimu sana Waheshimiwa.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati wa Fedha, Biashara na Kilimo:** Mhe. Spika, nakushukuru naomba nitoe majumuisho ya ripoti ya Kamati yetu kama ambavyo umeniruhusu na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu ambao tangu juzi walianza kuwasili ofisini kwako na leo Wajumbe wamekamilisha michango kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uwezo wa kusimama mbele yako ili kuweza kufanya majumuisho kuhusu michango mbali mbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe imetokana na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kwa kukushukuru binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kufanya majumuisho ya ripoti yetu.

Mhe. Spika, aidha pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia ripoti hii na wale ambao walibakia kimnya kwa ajili ya kusikiliza michango ya Wajumbe mbali mbali.

Mhe. Spika, Kamati yangu ilibahatika kuchangiwa na Wajumbe 11 na naomba niwataje kwa majina nao ni:

1) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2) Mhe. Muhamedreza Hassanali Muhamedali
3) Mhe. Salum Abdalla Hamad
4) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5) Mhe. Hamza Hassan Juma
6) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7) Mhe. Raya Suleiman Hamad
8) Mhe. Farida Amour Muhammed
9) Mhe. Abdalla Mohammed Ali
10) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11) Mhe. Salma Muhammed Ali

Mhe. Spika, mbali ya Wajumbe hao 11 wa kawaida, pia, tumepata bahati ya kutolewa maoni au majibu ya ufafanuzi kwa Waheshimiwa mbali mbali akiwemo Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Mhe. Waziri wa Fedha kaka angu, Mhe. Waziri wa Kilimo, kaka angu Dokta Mwinyi, Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Nassor Mazurui.

Mhe. Spika, Kamati yangu imepokea salamu za pole kufuatia kifo cha Mwenyekiti wangu Mhe. Salmin Awadh Salmin, Kamati yangu inapokea salamu hizo, lakini naomba kutoa wito kwa maeneo mawili

makubwa. Ili Wajumbe tumuenzi Mhe. Salmin, nashauri kwamba Jumamosi kwenye arubaini yake Wajumbe wote na Wafanyakazi wa Baraza hili waende kuhudhuria kama sehemu ya kumuenzi Mwenyekiti wetu Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Spika, Baraza hili lina historia ya Wajumbe wengi, huwezi kuzungumzia Uwanja wa Ndege bila ya kumtaja Mhe. Hamza Hassan Juma. Huwezi kuzungumzia mambo ya Muungano bila ya kumtaja Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Huwezi kuongelea mambo ya afya bila ya kumtaja Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Na huwezi kuzungumzia mradi wa *ZUSP* bila ya kumtaja Mhe. Salmin Awadh Salmin.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, ili Baraza hili limuenzi Mhe. Salmin Awadh Salmin, niwaombe wajumbe wenzangu kuanzia dakika hii ninayozungumza tupambene kwa nguvu zote ili kuleta ufanisi kwenye mradi wa *ZUSP* ambao Mhe. Salmin Awadh, mpaka siku ya Jumatano kabla ya kifo alisisitiza kwamba atasimamia mradi huu ya *ZUSP* ili tuweze kufanikiwa mafanikio ya wananchi wetu.

Lakini sambamba na hilo Mhe. Salmin Awadh, alikuwa ni muhimili mkubwa wa kusimamia maslahi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wake. Kwa hivyo, Sheria ile ya Utawala wa Baraza ni sehemu ya kumuenzi Mhe. Salmin Awadh Salmin, naomba tupambane.

Mhe. Spika, mbali ya utangulizi wangu huo, sasa naomba nijibu hoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, hoja ya mwanzo ni kukosekana kwa baadhi ya msaada wa *GBS* ambao Mhe. Spika, Kamati yangu imesema wazi kwamba hii itatokana na kashfa ile ya *Account* ya *Tegeta ESCROW,* ambayo Wizara ya Fedha walitwambia wazi kwamba baada ya kashfa ile ya Tanzania Wahisani waliamua kuzuia misaada yao na badala ya bilioni 40 ambazo Wizara ya Fedha walitegemea kuzipata kutokea *GBS* hatimaye fedha iliyopatikana ni chini ya bilioni 40 na si zaidi ya bilioni 25.

Mhe. Spika, kwa hivyo, athari ya wizi ule imetukumba Zanzibar, lazima tukubali kwamba imetukumba Zanzibar. Lakini nakubaliana na hoja ya Mhe. Muhammedraza, kwa nini aibe mtu mwengine hatimaye waadhibiwe Wazanzibari. Nadhani hii ndio athari ya kutia mbwembwe kwa koti la kuazima. Unapoalikwa harusi lakini ukaazima koti na ukaja kutia mbwembwe ndio athari yake hizi.

Mhe. Spika, nadhani tujifunze kwamba masuala ya kuazima hayafanyiwi mbwembwe. Niwajibu wetu sisi na kwa mujibu wa maagizo ya Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tujipange kwa kutafuta vyanzo vya mapato ambavyo vitaweza kuisaidia nchi yetu kwa hali na mali kwa mapato ya ndani na uwendeshaji wa maendeleo yetu.

Mhe. Spika, suala hili linaleta suluhisho ya muda mrefu. Kamati yangu baada ya kuona hivyo na kuamua kwamba lazima tuisaidie Serikali kutafuta vyanzo vya mapato. Kamati yangu imeamua kufanya mkutano mkubwa wa wadau wa mapato wafuatao. Kwanza Kamati yangu imeamua ikutane na *TRA, ZRB,* Bandari, Kamisheni ya Utalii, Baraza la Manispaa, *ZIPA*, *Chamber of Commence* na Wizara ya Biashara. Lengo la Mkutano huu ni kuonyesha Serikali jinsi ambavyo mapato ya Zanzibar yanavuja na vipi tuyadhibiti.

Mhe. Spika, utafiti mdogo ambao Kamati imefanya kila kontena moja bandari limekuwa likipoteza zaidi ya shilingi milioni mbili. Ukiangalia idadi ya biashara ya Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko, makontena ambayo yanaingia Zanzibar, ikiwa kontena moja linapoteza zaidi ya milioni mbili. maana yake Zanzibar inapoteza zaidi milioni 150 kwa mwaka. Sasa kama hivyo ndivyo, basi mapato ya Zanzibar tuyakusanye bila ya mvujo, maana yake mapato ya Wizara ya Fedha yanaongezeka kwa *speed* kubwa.

Lakini pia utafiti umeonyesha kwamba kila hoteli moja ambayo inalaza wageni kwa mwaka inapoteza zaidi ya dola laki moja kwa mwaka. Maana yake kila hoteli moja inapoteza zaidi ya milioni 160 kwa

mwaka. Kwa hivyo, kama itadhibitiwa hiyo mianya ya kupoteza mapoteza mapato, maana yake unaongeza mapato kwenye Serikali na hivyo itakuwa kilio cha Wizara ya Fedha kitakuwa hakipo.

Mhe. Spika, hiyo ndiyo rai yetu na tunaiomba Wizara ya Fedha ituunge mkono mkutano huo wa wadau wa mapato tuweze kushirikiana tukijua kwamba Baraza la Wawakilishi halikutuwezesha, lakini Kamati yangu imeamua kujitolea kwa ajili ya kufanya mkutano huo. Naomba wale wenyeviti wenzangu wa Kamati tukiwaalika mje mtusaidie kazi kwa sababu tunataka angalau kuonyesha Serikali kwamba mapato yanavuja kwa njia hii na kwa njia hii tuweze kuyadhibiti. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo itasaidia Serikali kukusanya mapato.

Mhe. Spika, hoja ya pili ambayo ningependa kuijibu ni hoja ya *TRA* kwamba Naibu Kamishna wa Zanzibar ni mtu wa nne. Ndivyo ulivyo uhalisia wake na ni kweli anawajibika kuwa Kamishna wa Forodha. Sasa hilo ni suala la Kisera na Kiutawala. Nadhani Wizara ya Fedha imesikia, itafanya ufatiliaji wa kina, wataweka mambo sawa na nivyomjua Mhe. Waziri wa Fedha hili jambo litakuwa ni rahisi ili tuweze kurekebisha ili malalamiko haya yasiende kuendelea mbele.

Mhe. Spika, hoja ya tatu ni Shirika la Bima ambalo Wajumbe wengi wamechangia ripoti yetu kwamba, Wafanyakazi wa Shirika la Bima wamekuwa wakipata malipo ambayo hayastahiki na hivyo Bodi yao imepitisha malipo mazuri zaidi ili kwa lengo la kuwadhibiti na kuwahifadhi wafanyakazi hao. Lakini Kamisheni ya Utumishi wa Umma bado haijakubali malipo hayo. Iweje bodi ya Shirika la *PBZ* wao wamekubaliwa kulipa mafao ndani ya uwezo wao lakini bima wanazuiliwa. Taasisi zote zipo chini ya Wizara ya Fedha, lakini Utumishi wa Umma wamewazuia Bima kwa ajili ya kuongeza mapato yao.

Mhe. Spika, wito wangu kwa niaba ya Kamati naomba kwamba Wizara ya Fedha watusaidia ili wafanyakazi wa Shirika la Bima na wao waweze kupata mafao yao mazuri kama ambavyo Bodi yao ya Bima imeamua.

Mhe. Spika, hoja ya *PBZ* kuongeza mtaji sina cha kuongeza, ni hoja ambayo Wizara ya Fedha wametuelimisha vya kutosha chini ya Katibu Mkuu wao na watendaji wake na Waziri leo asubuhi amezungumza. Niombe tu kwamba hoja hizo za kitaalamu wakae vizuri na wazifanyie utafiti mzuri. Ikiwa kuna haja ya kuongeza mapato kwenye benki yetu waongezewe na kama hakuna haja basi wakae wataalamu wakubaliane ili suala letu liende mbele kwa vizuri.

Mhe. Spika, suala jengine ni Kituo cha Usarifu wa Mazao Kizimbani. Mimi nakubaliana na Mhe. Waziri wa Fedha asubuhi. Wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakilaumu kwamba Serikali haitoi fedha kwa mawizara mbali mbali. Lakini ukweli ulivyo wakati mwengine ni masuala ya kujipanga tu kwa vipa umbele. Kamati yangu imethibitisha kwa Wizara ya Kilimo haikuwa na uchache wa fedha kiasi hicho hadi wasiweze kumaliza jengo la usarifu na mazao. Ukiangalia mtitiriko wa fedha inayoingia katika Wizara ya Kilimo, wangeamua kumaliza jengo la usarifu wa mazao Kizimbani wangekuwa na uwezo huo. Lakini ni suala la kujipanga na vipaumbele.

Hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha asubuhi ili kuwa ni hoja halali, haja haipingiki na ni hoja sahihi ambayo Mhe. Waziri ametoa. Kwa msingi huo sasa Mhe. Spika, tumefanya utafiti mdogo hapa na Mhe. Waziri wa Fedha hapa tunakuomba utusimamie. Ipo jumuiya ya *VSO ( Volunteer Services Organization)* ambayo hii ipo Makao Makuu yake Uingereza lakini ina tawi lake hapa Tanzania. Wamekubali kusaidia *euro* 45 na shilingi milioni 200 kwa ajili ya kumaliza jengo la usarifu wa mazao Kizimbani. Fedha hizo ukizi-*calculate euro* 45 na milioni 200 maana yake ni milioni 282.2. Ikiwa haja yetu sisi ni milioni 361, maana yake tuna upungufu wa milioni 73.

Sasa hizi kama Wizara ya Kilimo watashindwa basi bora wakunje watupe nafasi tutafute watu wengine. Ikiwa *NGO* imekubali kuchangia milioni 282 lakini Wizara wenyewe wakashindwa kuchangia milioni 73.

Mimi kwa heshima kubwa niwaombe Wizara ya Kilimo basi watupishe ili Rais atafute mwengine awasaidie.

Mhe. Spika, Kamati yangu itafatilia kwa karibu mno matumizi ya fedha hizi za *NGO* ambazo wamekubali kusaidia Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kumaliza jengo la Usarifu wa Mazao Kizimbani milioni 282. *NGO* hii ni *VSO (Volunteer Services Organization)* ambayo Makao Makuu yake yapo Uingereza tayari wamekubali kutoa milioni 282 kwa ajili yakusaidia jengo lile.

Mhe. Spika, hoja hii ya jengo la Kizimbani tuseme ukweli haikuwa hoja ya upungufu wa fedha za Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa fedha kulingana na uwezo wao, lakini vipaumbele vya watendaji wenyewe walikuwa hawazingatii umuhimu huo.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni mradi wa *ZUSP*. Mhe. Waziri wa Fedha asubuhi amezungumza kwa kina. Nataka niwambie wenzangu wajumbe, Kamati yangu kwa muda wote ya miaka miwili na nusu imekuwa ikipata tabu sana juu ya miradi miwili mikubwa, mradi wa *e-Goverment* na mradi wa *ZUSP*.

Mhe. Spika, nakumbuka mwaka jana ulituagiza chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Salmin, kwamba tufanye kazi maalum ya kuangalia mradi wa *e-Government.* Lakini nimthibitishie kwamba kazi ile ilifanyika kwa kidogo sana, maana yake hatukupata mashirikiano ya kutosha.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha na Waziri wa Fedha yupo, Kamati yangu ilitembelea mradi wa Makao Makuu Mazizini. Kamati ilipofika pale iliona Ofisi imejea vifaa kama compyuta na mambo mengine, sisi Kamati sio wataalamu, kwa hiyo, tukaridhika. Lakini kutoka nje tu, mfanyakazi mmoja akatupigia simu akatwambia niwambie ukweli Waheshimiwa hizo compyuta zimeazimwa leo asubuhi.(*Makofi*)

Wanatwambia wafanyakazi wa Ofisi ile. Mngezifungua mkaangalia hizo kumbukumbu zilizokusanya hakuna kumbukumbu za aina yoyote.

Mhe. Spika, mimi si mtaalamu, Mhe. Hamad yeye ni *Sieving Engineer*, Mhe. Salmin Awadh yeye alikuwa jeshi, kwa hivyo, hatuna uwezo wa kuangalia mambo hayo. Lakini Mhe. Spika, ukweli ulivyo mradi huu tuwe wazi, kwa sababu Mrada wa *e-Government* na Mradi wa *ZUSP*, ufanisi wake ni mdogo. Nakubaliana mia kwa mia na Mhe. Waziri wa Fedha, kwamba sio kuna haja ila kuna ulazima wa kuvunja Bodi ya Zabuni ya Wizara yako ambayo imetia hasara. Ili nikupe ushahidi kwamba kuna haja ya kuvunja Mhe. Spika, mna mradi nyie wa ujenzi wa ukuta wa bahari. Taarifa ambazo tunazo za uhakika zabuni ya mwanzo ambayo mlikubaliana ambayo watu wanaitetea ni bilioni 19. Lakini wengine wakasema mbona hii gharama ni kubwa!

Baada ya kukaa na kujadiliana iliposhuka sasa hivi ni bilioni 8. Watu walikuwa wanafikiria kukunja 11 bilioni. Kwa hivyo, ni lazima sio ridhaa, Bodi yako za zabuni uvunje uchague watu wengine wenye moyo wasaidie nchi hii. Hatuwezi kufuta madeni kwa sababu ya kunufaisha watu wachache, lazima Wizara yako na wizara zote na Serikali kwa ujumla isaidie nchi hii kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, nimalizie kusema kwamba Kamati yangu chini ya Mhe. Hija Hassan, hivi sasa na naambiwa kesho *Inshaallah* nitakuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Nitasaidia kwa nguvu zangu zote ili kuwashawishi wenzengu wa Baraza la Wawakilishi kwamba Wizara ambayo inapoteza fedha kwa makusudi, hiyo wizara lazima ikwamishwe.

Ingekuwa si haki kama Mhe. Waziri wa Fedha leo hakusema, mimi kabla ya hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha leo nilifanya utafiti sehemu mbili; Nilifanya utafiti Wizara ya Fedha yenyewe kwamba nilimwandikia Katibu Mkuu kumtaka anambie kwa mwaka mmoja Wizara ya Afya imeingiza fedha kiasi gani.

Pia, nikamtaka Wizara ya Elimu fedha ni kiasi gani. Akanambia fedha zilizoingizwa na ripoti tunayo kutoka Wizara ya Fedha. Baada ya kuangalia ripoti hizo za utafiti, Wizara zinapoongoza hapa Zanzibar ni Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kwa kuingiziwa fedha na Wizara ya Fedha yenyewe. Lakini ukija hapa ndio wao wa mwanzo wanasema kwamba sisi hatuna fedha, fedha ndogo. Ushahidi ni ule wa asubuhi kwamba wanaingiziwa fedha lakini hakuna ufanisi.

Ripoti hii ya Wizara ya Elimu niliyoifanyia mimi utafiti kabla ya leo, imesema wazi kwamba tatizo la Wizara ya Elimu ni uwezo mdogo wa utendaji. Sio kwamba hawana elimu, lakini jambo halifanywi mpaka afanye Hija, maana yake Omari Yussuf haaminisi, Mohammed Aboud haaminiwi, lazima afanya Hija. Kwa hivyo, uwezo mdogo wa utendaji ndio umesababisha Wizira ya Elimu, kututilisha hasara.

Kwa hivyo, nawashauri wajumbe wenzangu na kama nitakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, hiyo Bajeti Kuu ya Wizara ya Fedha naomba wenzangu basi Wizara ya Elimu wajieleze kabla ya kuja hapa uwanjani. Kwa sababu huko chini wananchi wanalaumu Serikali kwa ujumla kumbe ni makosa ya mtu mmoja. Mimi ni mtu wa CUF, lakini mtu mzuri akifanya vyema lazima apongezwe, aambiwe ukweli na CCM akifanywa vyema ambiwe ukweli. Lakini kumbe CCM wanakula hasara kwa sababu ya watu wachache.

Mhe. Spika, ripoti ya pili ambayo nimeifanyia utafiti ni *BOT*. *BOT* niliwataka wanambie kwamba miaka miwili hii Zanzibar mmetusaidia pesa ngapi za *GBS* na na misaada mengine. Ukiangalia ripoti hizi mbili hakuna tatizo la kifedha. Wizara ya Fedha wanapewa kwa mujibu wa mgao ule *GBS* na wao wanagawa chini kwenda katika mawizara. Lakini mawizara yamekuwa ni vikwazo. Sasa si halali kuja hapa tukawalaumu Wizara ya Fedha kwamba pesa hawatoi, kumbe wanatoa lakini hakuna mpango endelevu.

Mfano mwengine Mhe. Spika, nikupeni ushahidi, fedha ambayo imeingizwa Skuli ya Kengeja Ufundi milioni 200 hadi leo haikufika. Kwa hivyo, walimu wanamwambia Mwakilishi kafatilie fedha. Mimi nakwenda Wizara ya Fedha wananambia fedha imetoka. Iko wapi? Iko Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, matatizo sio Wizara ya Fedha. Na sitetei kwa sababu nataka Uenyekiti wa Kamati hapana, nasema ule ukweli ulivyo. Sio tatizo la Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha wanatoa kulingana na keki ilivyo, lakini upangaji wa vipaumbele ni wizara husika na wizara husika mfano huo wa Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ni mtihani mkubwa. Kamati husika lazima tuwe macho, tupambane ili wananchi wapate maslahi.

Mhe. Spika, baada ya hoja yangu hiyo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo. Waheshimiwa Wajumbe baada ya majumuisho hayo ya Mhe. Makamu Mwenyekiti, sasa nataka niwahoji wale wanaokubaliana na kuzipokea ripoti za utekelezaji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**TAARIFA ZA SERIKALI**

**RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA BARAZA YALIYOTOKANA NA RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI YA MWAKA 2013/2014**

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Ripoti kuhusu Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kabla sijawasilisha nataka kuweka utangulizi mmoja, nataka kusema kwamba kwa upande wa Chama chetu cha CCM tunapoapa kuna kifungu tunasema; *sitotumia cheo changu kwa faida yangu*.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia afya njema na uzima na kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha Ripoti hii ya Utekelezaji wa Maagizo na Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, naomba pia niungane na Waheshimiwa Mawaziri waliopita kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ninayoiongoza kutoa mkono wa pole kwa familia na kwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi marehemu Salmin Awadh Salmin. Tunamuomba Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi.

Mhe. Spika, aidha naomba kutoa shukurani kwa Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako Tukufu kwa utendaji wao wa kazi, maoni, ushauri na mashirikiano makubwa yanayoipa wizara yangu. Hali hiyo imepelekea kuwepo kwa kasi na ufanisi katika utendaji wa kazi na majukumu ya Wizara hii.

Mhe. Spika, katika ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara yangu ilipewa maagizo 13 ambayo yalitakiwa kutekelezwa na taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara kama ifuatavyo:-

Shirika la Umeme lilipewa maagizo matatu (3), Idara ya Nishati ilipewa maagizo manne (4), Mipango Miji na Idara ya Ujenzi ilipewa maagizo mawili (2), Mahkama ya Ardhi ilipewa maagizo mawili (2), Wizara yaani jengo la Kengeja ilipewa agizo moja (1) na Mamlaka ya Mji Mkongwe agizo lilikuwa moja (1).

Mhe. Spika, wizara yangu imeyafanyia kazi maagizo hayo na naomba kuwasilisha kama inavyoonekana katika jadweli.

Kwanza Shirika la Umeme. Agizo la kwanza Mhe. Spika, ni kwamba kamati imeiomba Serikali kuongeza vituo vya kuuzia umeme kwa Pemba mbali na vile vya Wete, Chake na Mkoani. Utekelezaji. Mhe. Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme imo katika juhudi za kuongeza huduma za umeme, ikiwemo kuongeza vituo na kuwa na njia mbadala ya kuuzia umeme kama vile njia ya kununua umeme kwa kutumia simu za mikononi. Shirika tayari limeshatiliana mkataba na Kampuni ya Zantel kwa miaka 2 kuhusiana na huduma za kununua umeme kwa kutumia simu za mikononi, mkataba huo umeanza rasmi Agosti, 2014.

Agizo la pili kwa Shirika la Umeme ni kwamba kamati imeliagiza Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba kila taasisi ya Serikali ambayo hailipi ikatiwe umeme. Sambamba na hilo taasisi hizo zote ziwekewe mita za TUKUZA ili kuwalazimisha kulipia umeme kabla ya matumizi.

Utekelezaji. Mhe. Spika, ni kwamba zoezi la kuzifungia mita za TUKUZA taasisi za Serikali linaendelea sambamba na kuzikatia umeme taasisi ambazo zinaonekana ni sugu katika kulipia madeni yao. Hata hivyo, zoezi la ukataji limekuwa likitekelezwa kwa umakini mkubwa kwa kujali umuhimu wa huduma za msingi za kijamii zinazotolewa na taasisi husika.

Agizo la tatu katika Shirika la Umeme ni kwamba kamati imeliagiza Shirika kuharakisha suala la kuzibadilisha mita za TUKUZA ambazo zinatumia pesa na kuweka zile zinazotumia *unit* ili kusaidia kupata uhakika matumizi ya umeme gharama zake na kuondosha tofauti ya bei kwa wateja.

Utekelezaji. Mhe. Spika, ni kwamba *ZECO* ilifanyika kampeni maalum ya kuzibadilisha mita za TUKUZA zinazotumia pesa ambazo taarifa ilitolewa kupitia vyombo vya habari ya kuwataka wateja wote wenye mita za aina hiyo kujitokeza, ili ziweze kubadilishwa kabla ya mwezi Oktoba mwaka 2014 ambapo Shirika lilipanga kuzima mtambo wa mauzo ya umeme kwa kupitia mita za aina hiyo.

Hata hivyo changamoto ilijitokeza kwa baadhi ya wateja kung'ang'ania kutumia mita hizo, kwa sasa wapo wateja wachache wanaojitokeza kuomba kubadilisha mita hizo baada ya wao wenyewe kukataa hapo awali kubadilishiwa. Shirika linaamini utekelezaji wa kampeni hii umefanikiwa kwa asilimia 98.

Mhe. Spika, Idara ya Nishati ambayo ilikuwa na maagizo 4 ni kwamba agizo la kwanza kamati imeiagiza Idara ya Nishati katika hatua ya uandaaji wa Sera ya Mafuta kuangalia uzoefu wa nchi za wenzetu ambao waliwahi kupitia mambo mbali mbali yanayohusiana na uzoefu wa uchimbaji wa mafuta.

Utekelezaji ni kwamba katika uandaaji wa sera ya mafuta na gesi asilia Serikali imeunda kikosi kazi maalum kinachoshirikisha sekta muhimu zenye uhusiano wa karibu na sekta hiyo ikiwemo Idara ya Nishati. Rasimu ya awali imeshatayarishwa na kuwasilishwa Serikalini kwa hatua zinazofuatia.

Agizo la pili ni kwamba kamati imeishauri Serikali ianze kuwekeza sasa katika kuwasomesha wanafunzi wenye fani zinazohusu masuala ya mafuta na gesi kwa kuwapatia mikopo wanafunzi waliopo vyuoni ambao wanataka kusomea masomo hayo.

Utekelezaji ni kwamba Mhe. Spika, mwanzoni mwaka 2013 Idara ya Nishati ilitekeleza maoni ya kamati kwa utaratibu wa kugawa vipeperushi na kukabidhi kwa watendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa kuvisambaza kwa wanafunzi wanaoomba mikopo hiyo.

Vile vile Idara ilitoa ushauri nasaha kwa wanafunzi hao kwa nyakati tofauti kuhusiana na masomo ambayo wanakusudia kuchukua. Kuanzia mwaka wa masomo 2013/2014 Bodi hiyo ilianza kutoa upendeleo maalum kwa wanafunzi wanaokusudia kuchukua masomo ya mafuta na gesi asilia. Idadi ya wanafunzi wa masomo ya mafuta na gesi wameongezeka katika vyuo mbali mbali vya hapa Tanzania na vile vya nje, ambapo takwimu za hivi karibuni ni vijana 30 waliotambulikana.

Agizo la tatu ni kwamba kamati imeishauri Serikali katika kuimarisha Idara ya Nishati ingeipatia jengo la kisasa, vitendea kazi vinavyoendana na kazi yenyewe, kuwapatia elimu na mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wake na kuwapatia maslahi mazuri wataalamu waliopo sasa ili kuendana na kazi wanayoifanya.

Utekelezaji Mhe. Spika, ni kwamba hatua bado zinaendelea kuzingatiwa katika kutimiza hilo na mipango ya kuongeza maslahi yamezingatiwa. Wizara inalishughulikia hilo na inaomba wakati zaidi kwa vile ni suala linalohitaji nyenzo na mashauriano mbali mbali ndani ya Serikali. Watendaji wa Idara ya Nishati hupatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini China kuhudhuria makongamano na Semina za *East African Commission* kadri nafasi zinapotokezea.

Agizo la nne katika Idara ya Nishati ni kwamba kamati imeishauri Serikali kuanzisha mpango mahsusi wa kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusiana na masuala ya mafuta na gesi, faida na hasara zake.

Utekelezaji ni kwamba Wizara kupitia Idara ya Nishati imeanzisha mikakati miwili ya kuwapatia wananchi elimu ya mafuta na gesi. Mkakati wa kwanza ni kuandaa semina za kuwashirikisha wataalamu wa kimataifa na viongozi wa Serikali, na wa pili ni kwa semina na vyombo vya habari vya nchini na wananchi kwa jumla. Jumla ya semina 16 za kutumia wataalamu wa kimataifa na mbinu za ndani kwa wananchi zimefanyika. Changamoto za upatikanaji wa fedha zinaathiri ukubwa wa zoezi hilo hasa kwa wananchi wa kawaida yaani *public.*

Idara ya Mipango Miji. Mhe. Spika, agizo la kwanza katika Idara hii ni kwamba kamati imezitaka mamlaka husika zikiwemo Idara ya Ardhi na Usajili, Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na kadhalika kusimamia vyema na kwa uadilifu majukumu yao ya kazi kama walivyotakiwa na Serikali.

Utekelezaji ni kwamba Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na kadhalika zinaendelea vyema kusimamia majukumu yao ambapo usimamizi wa ardhi, mipango miji na ujenzi nchini unaendelea vyema kwa kushirikiana na taasisi nyengine nchini.

Aidha bodi zilizo chini ya Idara hizi kama vile Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi, Bodi ya Usajili wa Kandarasi, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo zinaendelea kuzisaidia Idara hizi katika kutekeleza majukumu ya kila siku kwa ufanisi.

Agizo la pili katika Mipango Miji ni kwamba kamati imeiagiza wizara kusimamia upatikanaji wa baadhi ya sehemu za mashine ya kufyatulia matofali iliyowahi kuibiwa ili iweze kurudishwa, kwani hiyo bado ni mali ya Serikali.

Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi ilifanya juhudi kubwa ya kufuatilia vifaa vya mashine ya matofali vilivoibiwa huko Kwarara ili kurejesha mashine iweze kufanya kazi zake. Vifaa vilivyopatikana havijawezesha mashine hizo kufanya kazi.

Mahkama ya ardhi. Agizo katika Mahkama ya Ardhi ni kwamba kamati imeitaka Serikali kuhakikisha kwamba Mahkama za Ardhi zinaimarishwa Unguja na Pemba na kuzipatia majengo yaliyo na nafasi.

Mhe. Spika, Mahkama ya Ardhi imeendelea na ujenzi wa Mahkama ya Koani Mkoa wa Kusini Unguja, hatua iliyobakia katika jengo hilo ni uingizaji wa samani (*furniture)*, kumalizia utiaji wa rangi sehemu ya nje ya jengo, upatikanaji wa maji pamoja na kuweka nondo katika sehemu ya juu ambayo ipo wazi (*open to sky)* kwa ajili ya kuzuia wezi wasiweze kuruka na kuingia ndani.

Agizo la pili katika Mahkama ya Ardhi ni kwamba, kamati imeiagiza wizara kulitembelea jengo la Mahkama ya Unguja na kuipatia vifaa vya kutendea kazi, ili kazi ya utoaji haki iweze kufanikisha.

Kama ilivyoagizwa na kamati Wizara imetembelea jengo hilo na kuona hali halisi ya mazingira ya utendaji wa kazi. Wizara inaendelea kuzipatia taasisi zake fedha kwa kuzingatia mahitaji ya lazima ya taasisi kulingana na mgao tunaopata kutoka Hazina. Hata hivyo bado Mahkama inakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi hususan tatizo la usafiri. Kwa sasa Mahkama zetu zote za Unguja na Pemba hazina gari hata moja, aidha bado inaendelea kukabiliwa na uhaba wa nafasi za kufanyia kazi katika jengo la Mahkama liliopo *Majestic* Unguja.

Mhe. Spika, agizo kwa ajili ya Nyumba ya Kengeja. Kamati iliiagiza Serikali kabla kumalizika kwa mwaka huu wa fedha kuwapatia Wizara pesa zilizoidhinishwa katika bajeti 2013/2014 ambazo ni jumla ya shilingi 200,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa jengo. Wizara iliahidiwa na Wizara ya Fedha kupatiwa milioni 200,000,000 lakini hadi sasa fedha hizo hazijapatikana. Aidha Wizara imeendelea kuziomba pesa hizo kila bajeti ya mwaka ili kufanikisha ujenzi huo.

Mji Mkongwe suala la Kiwanja cha Mhe. Kamal Basha Pandu. Mhe. Spika, kamati baada ya kupata maelezo kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe ambazo kuna sababu za msingi kuzuia utoaji wa kiwanja hicho imeagizwa Wizara kumpatia Mhe. Kamal kiwanja mbadala.

Mhe. Spika, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi cha kupitisha bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2013/2014 Wajumbe walio wengi waliitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kutoa kibali kwa kiwanja hicho kwa Naibu Spika mstaafu, Mhe. Kamal Basha kutokana kuitumikia nchi kama kiongozi.

Mhe. Spika, huyo alikuwa na azimio la kujenga kituo cha petroli, abadilishe matumizi na ajenge nyumba ili kuondoa hatari ya kituo cha petroli kuwa karibu na kituo cha umeme. Matakwa ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Tukufu yalitekelezwa, na kwa sasa kiwanja hicho tayari kishajengwa. Mhe. Spika, naomba kulijulisha Baraza lako Tukufu kwamba bila ya shindikizo la Wajumbe wako kiwanja kile kisingetolewa na kadhia hii isingekuwepo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha ripoti yangu hii naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa mkono wangu wa pole kwa kumpoteza Mwakilishi shujaa, mwana CCM mahiri Mhe. Salmin Awadh Salmin katika Baraza letu.

Mhe. Spika, natoa pole hiyo si kwa sababu tu ndio kawaida kila mmoja anatoa, lakini vizuri wafahamu kwamba Mhe. Salmin nikimjua si kwa sababu kumkuta katika Baraza la Wawakilishi. Familia ya Mhe. Salmin ni familia iliyo karibu sana na mimi, na ni watu tuliokuwa tunafahamiana zamani kiasi cha kwamba hata wewe Mhe. Spika, wengine huamini kwamba mimi nimelelewa Makunduchi.

Mhe. Spika, nilipata masikitiko makubwa na mimi kumkosa Mhe. Salmin kwa sababu ni mmoja katika mtu tuliokuwa tuna mas-hara makubwa humu ndani, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi huko mbele ya haki, yeye ametangulia na sisi hatujui lini, *yarabi husnil khaatima.*

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wa maneno hayo, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kama yalivyowasilishwa wakati wakifanya kazi ya kamati katika wizara yangu. Ushauri na maagizo hayo yana lengo la kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Aidha napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa pamoja na Wajumbe wote wa kamati hiyo kwa ushauri, maelekezo na mashirikiano waliyotupatia muda wote wakati wakifanya kazi zao kwa lengo la kuimarisha kazi zetu za kila siku. Maagizo, ushauri na maelekezo waliyotupatia yamesaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kama ilivyo kawaida kwa wizara nyengine, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea kusimamia utekelezaji wa kazi zake za kawaida na maendeleo kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo yaani *vision 2020,* Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini yaani Mkuza II, Sera ya Usafiri Zanzibar ya 2008, Mpango Mkuu wa Usafiri yaani *Zanzibar Transport Master Plan 2009,* pamoja na sera nyenginezo zinazohusiana . Katika kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi, wizara imejigawa katika Sekta Kuu 4 ambazo ni Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu, Sekta ya Usafiri wa Baharini, Sekta ya Usafiri wa Anga na Sekta ya Mawasiliano.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipata fursa ya kupitia sekta zote nne za wizara Unguja na Pemba, kwa lengo la kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kutoka sekta hizo. Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi naomba uniruhusu kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu utekelezaji wa maagizo, ushauri na maelekezo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 kwa lengo la kujadili, kupata maoni na maelekezo yenu, yenye lengo la kujenga Taifa letu.

Mhe. Spika, wizara yangu ilipewa maagizo 20.

La kwanza, kamati ilitushauri wizara kuhakikisha kwamba mara baada ya mkandarasi kuanza kazi ya ujenzi ni jukumu la wizara kusimamia ili kuhakikisha kwamba mradi huo unamalizika na kuwaondolea wananchi usumbufu waliopata kwa muda mrefu (ujenzi wa barabara za Pemba).

Mhe. Spika, utekelezaji. Wizara inaendelea kusimamia ujenzi wa barabara za Wete/Gando na Wete/Konde kwa kuhakikisha mradi huo unamalizika haraka na kwa muda uliopangwa. Hili limefanyika kwa kuongeza nguvu katika usimamizi ambapo Mhandisi wetu ambaye alikuwa kwenye Mradi wa *MCC* amehamishiwa kwenye mradi huo. Nina furaha kutoa taarifa kuwa ujenzi wa barabara hizo mbili umemalizika na taratibu za makabidhiano zinaandaliwa muda wowote kuanzia sasa.

La pili kamati imeitaka serikali kuzihusisha taasisi husika kwa pamoja wakati wa kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo itapelekea kuwa na mipango ya muda mrefu itayoepusha mradi mmoja kuathiri maendeleo ya mradi mwengine ambayo yote ipo kwa faida ya wananchi.

Utekelezaji. Mheshimiwa Spika, wizara inaendelea kushirikiana na wadau mbali mbali kama vile Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Idara ya Mazingira, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Shirika la Umeme, Mamlaka ya Maji pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wilaya wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo Unguja na Pemba.

Mfano, kuhusiana na uharibifu wa mkonga wa mawasiliano Pemba, wizara imeshirikiana na Kampuni ya Serengeti, ambapo walikubaliana kampuni hiyo ilipe jumla ya milioni 15,000,000/= kugharamia matengenezo ya mkonga katika maeneo mbali mbali huko Pemba ikiwemo Machomane na Wete kufuatia uharibifu waliofanya wakati wa kuweka mabomba ya maji.

Katika Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Wete/Gando na Wete/Konde, wizara imeshirikiana na *ZAWA*, *TTCL* na *ZECO* katika kuondosha miundombinu ya huduma za maji na huduma za jamii. Ushirikiano huu umewezesha mkandarasi kupata eneo la ujenzi na kazi tayari imekamilika.

La tatu, kamati imetaka maelezo ya kina kwa kukosekana kwa fedha za kuendeleza kazi ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege huko Pemba.

Mhe. Spika, maelezo ya utekelezaji. Serikali imeagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuweka taa katika njia ya kutulia na kurukia ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

Katika utekelezaji wa agizo hilo, wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha taratibu za kuipata kampuni ambayo itatengeneza na kuweka taa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Taratibu za kusaini mikataba zimekamilika tangu tarehe 16 Machi, 2015. Kwa mujibu wa ratiba ya kazi ya uwekaji wa taa hizo tunatarajia kazi hiyo kukamilika mwezi wa Juni mwaka huu. .

Agizo la nne, kamati imeitaka serikali kuweka kipaumbele kwa kuiwezesha Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*) hali itakayopelekea kuiwezesha kufanya kazi vizuri na kupunguza majanga yanayojitokeza mara kwa mara.

Utekelezaji. Kutokana na matokeo ya ajali za vyombo vya usafiri wa baharini hapa Zanzibar, serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 5 ya 2006 ya kusajili meli za abiria, ambapo sasa meli zitakazosajiliwa kwa mara ya kwanza zitatakiwa kutozidi umri wa miaka 15. Marekebisho hayo

yamepitishwa na Baraza lako Tukufu na kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Agizo namba tano, kamati iliitaka serikali kuhakikisha kwamba mkonga wa Taifa unalindwa na kuzingatia viwango vya Kimataifa wakati wa uwekaji wa miundombinu kama hii.

Utekelezaji. Kwa kuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikabidhiwa mkonga kutoka Wizara ya Fedha ukiwa tayari umeshalazwa nchi nzima, tulichokubaliana ni kwa kila sehemu itakayotokezea uharibifu tunahakikisha tunafanya marekebisho kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa. Aidha, kutokana na uelewa mdogo wa jamii juu ya umuhimu na uwepo wa mkonga wa Taifa hapa Zanzibar, wizara imetoa elimu kupitia vyombo vya habari, redio na televisheni kwa lengo la kuelimisha jamii ili kuweza kuutunza na kuulinda kwa maendeleo ya Taifa letu.

Agizo namba sita. Mhe. Spika, kamati ilitoa ushauri kwa serikali kuliangalia upya suala la kuzitoza kodi kampuni za simu zinazotoa huduma hapa Zanzibar, ambazo kwa sasa zinalipia kodi Tanzania Bara tu, kinyume na kampuni ya *ZANTEL* ambayo inalipia kodi Tanzania Bara na Zanzibar.

Utekelezaji. Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo Kampuni za Simu zinazotoa huduma hapa Zanzibar ni *ZANTEL*, *Tigo*, *Airtel*, *Vodacom* na *TTCL*. Katika kutoa huduma kampuni hizi zimewekeza kwenye miundombinu kama vile minara, *fibre*, *copper* na kadhalika. Hata hivyo, Mhe. Spika, suala la makampuni haya kulipa kodi hapa Zanzibar halipo chini ya wizara yetu, liko katika Wizara ya Fedha.

Agizo namba saba, kuhusu madeni ya *ZAT*. Kamati imeitaka serikali kuhakikisha kwamba fedha hizo zinalipwa, lakini pia kuhakikisha kwamba kampuni hiyo inasaini mkataba wa kufanya kazi katika Viwanja vya Ndege kama ilivyo sheria.

Utekelezaji. Mheshimiwa Spika Kampuni ya *ZAT* tayari imeshakamilisha kulipa jumla ya milioni 640 ikiwa ni madeni yake yote ambayo ilikuwa inadaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama "*concession fee*" kwa kazi za huduma za ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume.

Kuhusu kusaini mkataba Kampuni ya *ZAT* inapenda kujuulisha Baraza hili kuwa tarehe Februari, 2015 Kampuni ya *ZAT* ilisaini mkataba na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa ajili ya kutoa huduma za ndege katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kama taratibu zinavyoelekeza.

Agizo namba nane, kamati imeitaka serikali kumaliza taratibu za kuipata kampuni nyengine ya kutoa huduma kiwanjani hapo ili kuleta ushindani wa kibiashara.

Mhe. Spika, tayari taratibu zote za kuipata kampuni ya pili ya kutoa huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume zimekamilika. Mkataba na kampuni ya pili ulitiwa saini tarehe 12 Oktoba, 2014. Kwa sasa kampuni hiyo inaendelea na taratibu za kisheria kabla ya kuanza kazi ambapo imeiarifu serikali kuwa inasafirisha vifaa kuja Zanzibar hivi karibuni.

Agizo namba tisa, suala la kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege fedha zinazokusanywa kutokana na huduma inazozitoa mamlaka kwa abiria (*Airport Service Charge*). Kamati imeomba serikali kufikiria upya suala la kuipatia mamlaka japo asilimia fulani ya mapato hayo. Mapato hayo yagaiwe sehemu tatu ambayo theluthi moja iende Mfuko wa Hazina, theluthi ya pili iende katika miradi ya kuendeleza viwanja na theluthi ya tatu ibakie kwa mamlaka ili kufidia gharama za kuendesha kiwanja hicho.

Utekelezaji, jitihada za kuiomba serikali kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege sehemu ya mapato ya tozo la kodi za huduma za Viwanja vya Ndege zinaendelea. Aidha, wizara imeandaa waraka maalum kupeleka serikalini ambapo pamoja na mambo mengine suala la kodi hiyo pia limewasilishwa.

Agizo namba kumi. Mheshimiwa Spika kamati imeitaka serikali kupitia wizara inayohusika na usimamizi wa Vikosi vya Zimamoto kuvipatia huduma zote muhimu ili viweze kufanya kazi ipasavyo.

Utekelezaji, wizara inakiri kuwa hali ya magari ya Zimamoto katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume bado sio nzuri. Hata hivyo, serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa mashirikiano na taasisi husika inachukua juhudi mbali mbali kuondoa tatizo hili. Sambamba na juhudi hizo hivi karibuni wizara imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia waidhinishe ununuzi wa magari ya Zimamoto na vifaa vyake kupitia bakaa ya fedha zilizobaki katika mradi wa ujenzi wa *taxiway* na *apron*.

Agizo namba kumi na moja, kamati imeitaka serikali kupitia wizara inayohusika na usimamizi wa Jeshi la Polisi kuwatafutia utaratibu wa kujengewa Kituo cha Polisi katika maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Pemba ili askari hao waweze kufanya kazi zao mchana na usiku.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tayari imewapatia Jeshi la Polisi chumba katika jengo la Uwanja wa Ndege wa Pemba ambacho wanakitumia katika masuala ya ulinzi. Hivyo kwa sasa hakutakuwa na haja tena ya kujenga kituo maalum kwa shughuli za ulinzi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

Agizo namba kumi na mbili, Mheshimiwa Spika kamati imeitaka serikali kulipatia eneo Shirika la Bandari karibu na bandari hiyo ili iweze kujenga jengo la kisasa litakalokuwa na mnara wa kuongozea meli na kuachana na utaratibu wa sasa wa kuazima majengo.

Mhe. Spika, katika kutekeleza agizo hili kwa vile katika Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, ujenzi wa mnara wa *Signal Station* umezingatiwa. Wizara haioni haja ya Shirika la Bandari kupatiwa eneo jengine la kujenga jengo litakalokuwa na mnara wa kuongozea meli. Aidha, tatizo la kuazima jengo kwa ajili ya kituo cha kuongozea meli kwa sasa halipo tena baada ya kituo hicho kuhamishiwa katika jengo jipya la shirika lilioko bandarini.

Agizo namba kumi na tatu. Kamati imeishauri serikali kuangalia utaratibu wa kuikarabati minara ya kuongozea meli ambayo ni minara inayotambulika Kimataifa hasa kwa kuwa minara mingi imejengwa zamani sana.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari limeanzisha programu maalum ya uimarishaji wa alama za kuongozea vyombo baharini ikiwemo minara na maboya. Katika programu hii shirika linaifanyia ukarabati minara yote ya Unguja na Pemba kwa awamu. Kwa mfano, mwaka huu 2014/2015 shirika limepanga katika bajeti yake kuifanyia matengenezo minara miwili mikubwa, mnara wa Kigomasha na Nungwi. Kazi katika mnara wa Kigomasha imeshakamilika na mnara wa Nungwi imepangwa kuanza katika robo ya nne Aprili/Juni ya mwaka huu wa fedha baada ya kukamilika taratibu za zabuni.

Agizo namba kumi na nne. Kamati imeishauri serikali kulifikiria suala la kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kuipatia vifaa vikiwemo kreni ya kushushia mizigo mikubwa. Kamati imetoa pendekezo la kuitumia gati ya zamani ya Mkoani kutumika kushukia na kupandia meli abiria na gati ya sasa ibakie kuwa ya kushushia na kupakia mizigo ambayo itasaidia ugumu wa kuweka kipaa bandarini.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Shirika limepanga kununua vifaa vipya vya kubebea mizigo bandarini, vifaa hivyo ni pamoja na kreni na *forklift* ambavyo baadhi yake vitapelekwa katika Bandari ya Mkoani.

Kuhusu uwekaji kipaa katika njia ya gati ya Mkoani, shirika limeangalia uwezekano wa kuweka kipaa katika njia hiyo na imeonekana kuwa ni vigumu kutokana na kuwa gati hiyo inatumiwa na magari makubwa ya mizigo kupeleka kwenye meli.

Kuhusu ujenzi wa gati ya zamani ya Mkoani ili iweze kutumika, ujenzi huu utahitaji fedha nyingi kwa vile gati hiyo imebomoka kabisa. Kunahitaji kufanywa utafiti upya, na kwa sasa shirika halina uwezo wa kufanya matengenezo hayo pamoja na kazi *dredging* itakayohitaji kufanywa ili gati hiyo iweze kutumika.

Agizo namba kumi na tano. Kamati imeitaka serikali kuzikarabati bandari ambazo hazipo katika kiwango kizuri hali inayopelekea kutumiwa kinyume na utaratibu na kuikosesha serikali mapato kutokana na kutokuwa na ofisi zinazosimamia harakati za kila siku za bandari hizo. Mfano, bandari ya Mkokotoni.

Mhe. Spika, shirika limepanga mradi wa ujenzi wa gati za Mkokotoni na Tumbatu katika bajeti yake ya mwaka 2014/2015 pamoja na gati ya Wete. Utaratibu wa mradi huo unaendelea ambapo kazi ya kufanya uchunguzi wa kimazingira katika maeneo ya ujenzi, yaani Mkokotoni na Tumbatu imekamilika. Sambamba na kazi hiyo shirika limeanza kukusanya vifaa vya ujenzi huko Tumbatu na tayari shughuli za ujenzi zimeanza.

Agizo namba kumi na sita. Kamati imeishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha bandari ndogo katika maeneo ya Nungwi ambayo itasaidia kupunguza masafa ya safari baina ya visiwa hivi viwili, lakini pia itatumika kurahisisha shughuli za uokozi wakati wa majanga ya meli yanapotokea.

Mhe. Spika, majukumu ya shirika ni pamoja na kuziendesha, kuzitunza na kuziendeleza bandari tano za Zanzibar. Suala la kuanzisha bandari mpya linategemea sera za serikali katika sekta ya usafirishaji. Serikali bado haina mpango wa kuanzisha bandari mpya kwa sasa isipokuwa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ambayo utaratibu wake unaendelea.

Agizo namba kumi na saba. Kamati imependekeza kwa serikali kufikiria kuifanyia marekebisho sheria ya Shirika la Bandari ili iweze kutoa mamlaka kwa shirika hilo, kusimamia masuala yote yanayohusu bandari ikiwemo kubuni au kutoa mapendekezo kwa serikali kuhusiana na uanzishwaji wa bandari mpya katika maeneo tofauti kuliko ilivyo sasa kwamba shirika hilo linapewa mamlaka kusimamia bandari ziliopo tu.

Wizara imepokea ushauri na inaendelea kuufanyia kazi. Shirika kwa kuanzia limekamilisha mageuzi makubwa ambayo yanazingatia maendeleo ya muda mrefu ya shirika hili (*business plan*). Ripoti ya mageuzi hayo imeshawasilishwa serikalini tarehe 12 Februari, 2014 na kukubaliwa. Katika maagizo hayo mabadiliko ya sheria yamezingatiwa.

Agizo namba kumi na nane. Kwa ujumla kamati imeitaka serikali kuhakikisha ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ambayo kwa sasa hakuna taarifa za kuanza kwa harakati za ujenzi wa bandari hiyo.

Mhe. Spika, maelezo ni kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi husika za serikali imekamilisha taratibu zote husika za kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Kwa sasa Benki ya *Exim* ya China inaendelea na taratibu za kupitia maombi (*evaluation*) kabla hawajafanya maamuzi ya kukubali au kukataa.

Agizo namba kumi na tisa. Kamati imeiomba serikali kuja na mpango mahsusi ambao utakuwa na lengo la kutenga fedha maalum kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vifaa vya ujenzi wa barabara.

Mhe. Spika, wizara imewasiliana rasmi na Wizara ya Fedha ambapo idhini imetoka kuanza rasmi zoezi la ununuzi wa vifaa hivyo. Rasimu za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi imeshawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kupata ushauri wa kisheria kuhusu rasimu ya mikataba ya ununuzi iliyopendekezwa.

Mhe. Spika, mwisho kamati iliagiza Idara ya Leseni na Usafiri pamoja na Jeshi la Polisi kusimamia ipasavyo maagizo ya kikao kilichofanyika kwa lengo la kupunguza ajali na kuongeza kiwango cha uheshimu wa sheria za barabarani.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ilifanya kikao na Jeshi la Polisi Zanzibar siku ya tarehe 21 Januari, 2015 kuzungumzia vitendo vya uvunjaji wa sheria vya usafiri barabarani vinavyofanywa na madereva wa vyombo vya moto, kama vile kuendesha vyombo bila ya nambari za usajili hasa wakati wa usiku na mengineyo. Katika kikao hicho ilikubaliwa ifanywe semina itakayozikutanisha sekta zote za usafiri barabarani ili kulijadili suala hili kwa kina. Semina hiyo ilitarajiwa na bado inatarajiwa kufanyika kabla kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kufungwa.

Aidha, wizara tarehe 25 Novemba, 2014 kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, iliitisha mkutano uliowashirikisha wadau wote wa usafiri kwa lengo la kujadili kero za usafiri wa barabarani hapa Mjini. Katika kikao hicho wajumbe walikubaliana itolewe elimu kwa madereva na matingo wao kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya moto barabarani na kurudishwa utaratibu wa magari kufanyiwa uchunguzi wakati wa kuingizwa nchini mara ya kwanza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia, nachukua fursa hii tena kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunivumilia, kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha taarifa hii. Nawaomba Wajumbe wote waipokee na kujadili taarifa hii, na kutushauri ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Tunashukuru sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa kuwasilisha taarifa hiyo ya utekelezaji wa maagizo mbali mbali. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ili naye kuwasilisha ripoti ya mwaka 2014/15.

**Mhe. Marina Joel Thomas (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuwasilisha ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru M/Mungu muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia pumzi za kuweza kukutana tena katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, wakati tukiendelea kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kumbukumbu za Marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin hazitasahaulika na hazitafutika milele kichwani mwangu, kwani alikuwa ni rafiki yangu wa karibu sana na alikuwa mshauri wangu muhimu katika kazi zangu za Kamati na katika kutekeleza majukumu yote ya kuwatumikia wananchi. Kila kukicha naendelea kumuombea kwa Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake na amlaze mahali pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nijielekeze kwenye lengo la kusimama kwangu mbele ya Baraza lako Tukufu ambalo ni kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, hivyo bila ya kupoteza muda wako naomba kuwasilisha ripoti hiyo kwa muhtasari kama kanuni zetu zinavyotutaka.

Mhe.Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa Mujibu wa Kanuni ya 106(d) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012.

Majukumu ya Kamati yameelezwa katika Kanuni ya 111 ya kanuni hizo, ambapo pia kanuni hizo hizo zinatuelekeza kuwa kamati itawasilisha Ripoti yake katika Baraza la Wawakilishi kama inavyosomeka Kanuni ya 108(14) na naomba kuinukuu.

"Itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza, na masharti ya Kanuni ya 122 yatatumika kuhusu utaratibu wa kuwasilisha ripoti hizo".

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inatekeleza majukumu yake kwa kuzisimamia Wizara mbili, nazo ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Ardhi,Makaazi, Maji na Nishati, ambapo kwa kuokoa na kuheshimu muda wako naomba niainishe yale mambo muhimu zaidi ambayo kamati yangu imeyagundua katika kutekeleza kazi zake katika mwaka wa fedha 2014/2015 kama hivi ifuatavyo:-

**WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI**

Mhe. Spika, wizara hii inahusika na usimamizi na utoaji wa huduma katika Sekta ya Ardhi. Sekta ya Makaazi, Sekta ya Maji na Sekta ya Nishati.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imetekeleza malengo yake kwa ufanisi ingawa bado kuna kasoro ambazo kamati imezibaini ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili kufikia ufanisi unaotakiwa wa kuwahudumia wananchi kwa huduma zilizotukuka.

**SEKTA YA MAJI**

**MAMLAKA YA MAJI (*ZAWA*)**

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji *ZAWA* kwa kushirikiana na wahisani wa maendeleo wameendelea kuboresha huduma ya maji Zanzibar katika maeneo ya mijini na vijijini. Juhudi hiyo ni pamoja na uchimbaji wa visima, kujenga matangi pamoja na ufungaji wa pampu katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Juhudi hizi zinazochukuliwa zinastahiki pongezi za pekee kwani kwa kiasi kikubwa matatizo ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini yamepungua, hivyo kuwapunguzia wananchi kero na kujenga imani kwa serikali yao.

Mhe. Spika, licha ya jitihada kubwa inayochukuliwa na Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), Kamati imegundua baadhi ya changamoto ambazo zinarudisha nyuma jitihada za mamlaka na kupelekea kuzorota kwa baadhi ya mipango waliyojipangia. Baadhi ya changamoto hizo ni uchakavu wa miundombinu ya maji hali inayopelekea kupotea kwa rasilimali maji kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na suala la upotevu huo wa maji, kamati yangu imeitaka mamlaka kuchukua hatua za haraka kurekebisha miundombinu ya maji kwa kufunga mabomba mapya yenye ubora, kwa lengo la kupunguza tatizo la upotevu wa maji kwani kama *slogan* ya Mamlaka inavyoeleza kuwa

"*kila tone la maji ni gharama*", hivyo ni vyema maji yakadhibitiwa kwa vile upatikanaji wake ni gharama.

Mhe. Spika, kamati katika kutekeleza majukumu yake katika Mamlaka ya Maji, imebaini kuwa kuna sintofahamu kubwa baina ya *ZECO* na *ZAWA* juu ya uwepo wa deni kubwa ambalo linatokana na ufungwaji wa mita za Tukuza katika visima vya maji, deni ambalo *ZAWA* wanadai hawastahiki kulipia kwani kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Mamlaka yao haijatoa jukumu la kulipa umeme utakaotumika kusukuma maji bali jukumu hilo ni la Serikali.

Mhe.Spika, kamati haikuridhishwa na suala hilo hata kidogo, hivyo inaitaka Serikali kuingilia kati suala la deni la *ZAWA* linalodaiwa na *ZECO* linalotokana na matumizi ya umeme katika visima vya maji, na ikiwezekana kulipwa deni hilo kwani *ZAWA* haina uwezo wa kulilipa kutokana na uchache wa mapato yake. Sambamba na hilo, Kamati imeishauri serikali kuupitia na kuufanyia kazi waraka ulioletwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA),* wenye matakwa ya kuongeza malipo ya maji kwa wananchi kutoka 4,000/= hadi 12,000/= ambayo *ZAWA* inaamini itaweza kulipia gharama zake zote na kuweza kujiendesha kibiashara.

Mhe. Spika, sambamba na juhudi za *ZAWA* za kutafuta vyanzo mbadala vya upatikanaji wa maji, bado vyanzo vya asili vilivyopo vinapotea kwa kasi kubwa, ambapo upoteaji huo unasababishwa na ukataji wa miti katika maeneo ya hifadhi na kupelekea athari ya kupungua kwa mvua, aidha ujenzi holela wa makaazi pia hupelekea uchafuzi katika vyanzo hivyo.

Mhe. Spika, kamati inawaomba wananchi washirikiane na serikali katika juhudi za kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji, kwani athari yake ni kubwa kwa Taifa letu na kwa kizazi cha baadae.

Baadhi ya athari zinazoonekana ni kukauka kwa mito yetu ambayo zamani ilikuwa inajaa maji kama mito ya Zingwe zingwe, Kilimani na kadhalika, pamoja na baadhi ya sehemu kuwa na maji ya chumvi ambayo pia huathirika na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo ulimwengu wote unakabiliana nao.

**SEKTA YA NISHATI**

**SHIRIKA LA UMEME ( *ZECO*)**

Mhe. Spika, Shirika la Umeme Zanzibar lina jukumu la kusambaza umeme katika visiwa vya Unguja na Pemba, ambapo umeme huo *ZECO* inaununua kutoka Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO*, Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la umeme limeendelea na shughuli za usambazaji umeme mijini na vijijini kwa mafanikio licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa miongoni mwa changamoto kubwa inayolikabili Shirika la umeme Zanzibar ni kuwepo kwa deni kubwa wanalodaiwa na *TANESCO* linalotokana na bili za ununuzi wa umeme za muda mrefu, ambapo hadi kufikia Disemba 2014 Shirika lilikuwa linadaiwa bilioni 49.5

Kamati ilielezwa kuwa ukuaji wa deni hilo unasababishwa na *ZECO* kukosa uwezo wa kulipia bili zake za kila mwezi kwa ukamilifu, isipokuwa kwa baadhi ya miezi hali inaporuhusu Shirika huwa inalipa bili yake kwa ukamilifu.

Aidha Kamati ilipewa taarifa kuwa Shirika kwa kawaida huwa linalipa sehemu tu ya bili yake ya kila mwezi kwa mujibu wa uwezo wake wa mapato inayokusanya kutokana na uuzaji wa umeme, na hivyo kupelekea mkusanyiko wa bakaa za madeni katika kila mwezi ambapo shirika hushindwa kulipa.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi za Serikali ndio wateja wenye madeni makubwa kwa Shirika la Umeme, ambapo madeni hayo yanatokana na malimbikizo ya madeni. Kutoka Disemba 2013 hadi Septemba 2014, deni la jumla la taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa kutoka TZS 17.6 bilioni hadi kufikia 21.2 bilioni, na kwa upande wa taasisi za Muungano kutoka Shilingi 0.93 bilioni hadi kufikia 1,12 bilioni.

Mhe. Spika, kuhusiana na deni kubwa wanalodaiwa *ZECO* kwa *TANESCO,* Kamati inaiagiza serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kusimamia ulipwaji wa deni la shilingi bilioni 18 kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya fedha ya SMT kama kila mwezi, ili Shirika liweze kujiendesha kwa faida .

Mhe. Spika, katika kuona kwamba Shirika linaondokana na mrundikano wa deni la ununuzi wa umeme kutoka *TANESCO,* kamati imelishauri Shirika la Umeme (*ZECO)* kulipia ankara yake ya bili ya umeme kila mwezi ili kupunguza mrundikano wa madeni ambayo baadae inakuwa ni vigumu kuyalipa.

## SEKTA YA ARDHI

### AFISI YA MSAJILI WA ARDHI, IDARA YA ARDHI NA USAJILI, IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI, IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Mhe. Spika, taasisi hizi zinashughulika na masuala ya usimamizi wa ardhi ikiwa ni pamoja na usajili wa ardhi, upimaji, uchoraji ramani, pamoja kusimamia matumizi bora ya ardhi hapa Zanzibar.

Taasisi hizi zimekuwa zikifanya kazi kwa karibu sana ili kuhakikisha kunakuwepo na matumzi bora ya ardhi na katika kusajili ardhi kwa mujibu wa sheria za nchi. Kamati ilifanya ziara na kukutana na uongozi wa taasisi zote hizi, na imeridhishwa na utendaji wa kazi wa taasisi hizi licha ya kubaini kasoro ndogo ndogo ambazo zinasababishwa na kuwepo kwa changamoto mbali mbali ikiwemo ufinyu wa bajeti, ukosefu wa usafiri na uelewa mdogo uliomo katika jamii.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza kwa dhati Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa kukamilisha Mpango Mpya wa Mji wa Zanzibar (*Zanzibar Master Plan)* ambao utatoa muongozo bora juu ya kuupanga mji wa Zanzibar kwa kuainisha maeneo ya makaazi, maeneo ya kilimo na maeneo mbali mbali ya biashara, ambayo ni muhimu katika kuuendeleza mji wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati imezishauri taasisi zinazosimamia masuala ya ardhi kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi, kwani wananchi hawajafahamu mambo mengi yanayohusu ardhi, hasa umuhimu wa usajili wa ardhi na matumizi bora ya ardhi kwa kuzingatia mpango wa mji wa Zanzibar.

Aidha, kamati imeitaka Idara ya Mipango Miji na Vijiji, kutoishia katika mji wa Zanzibar pekee, bali pia kuangalia na kuuendeleza mji wa Chake Chake; Pemba, ili nao uwe ni mji wenye kufuata matumizi bora kwa ajili ya maendeleo endelevu.

## WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Mhe.Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara nyengine inayosimamiwa na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambapo inahusika na Sekta ya Usafiri wa nchi kavu, baharini na usafiri wa anga, pamoja na kusimamia masuala yanayohusu mawasiliano Zanzibar.

**SEKTA YA USAFIRI WA NCH KAVU**

**IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI BARABARA (*UUB*)**

Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ndio idara inayosimamia ujenzi na kutunza barabara Zanzibar. Kamati inaipongeza idara hii kwa juhudi zake za kujenga na kutunza barabara za Unguja na Pemba na kwa namna ya pekee kamati inapongeza kukamilika kwa barabara ya Amani – Mtoni, kwa kweli barabara imekamilika vizuri baada ya kusuasua kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na tatizo la barabara zinazojengwa kuchukua muda mrefu bila ya kumalizika, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara tatu Pemba ambalo Kamati imefarijika na kupata tamaa ya kumalizika baada ya makubaliano yaliyafanyika Pandani - Pemba na mbele ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Makubaliano ya Pandani yalikuwa kati ya mkandarasi wa Kampuni ya *MECCO* inayofanya ujenzi wa barabara hizo na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo mkandarasi amekubali kumaliza kazi yote ya ujenzi wa barabara ya Wete hadi Gando, Raha hadi Ukunjwi na Wete hadi Konde ndani ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, Kamati imekuwa na imani kwa mkandarasi huyo mzalendo baada ya kufanya ziara ya ukaguzi na kuona vifaa alivyonavyo kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo ikiwa ni pamoja na lami na mashine mpya kwa ajili ya kuzalisha kokoto aliyoifunga Machomane, Pemba. Kamati inaiomba serikali kumpa ushirikiano mzalendo huyo kwa moyo wake wa dhati aliouonesha kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, kumekuwepo kwa limbikizo kubwa la madeni ya ujenzi wa barabara hasa zile zilizojengwa wakati wa nyuma, na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kulipwa baadhi ya madeni mapya kutoka Wizara ya Fedha bila ya kulipwa fedha kwa ajili ya kulipa madeni yaliyopita kwa mwaka wa fedha husika, hivyo kupelekea kuzaa madeni mengine. Madeni hayo ni yale malimbikizo ya madeni ya fidia za wananchi ambayo bado yanaendelea kudaiwa na kuongezeka kila panapokuwa na ujenzi wa barabara mpya.

Mhe. Spika, kamati inashauri serikali kutenga kifungu maalum kwa ajili ya kulipia madeni ya nyuma au madeni hayo yabebwe na Wizara ya Fedha. Sambamba na hilo Kamati inaiomba Serikali iwe na *account* maalum ambayo itatumika kwa kulipia fidia kwa wananchi kwa miradi ya Serikali na ile ya wafadhili ambayo haina kifungu cha malipo ya fidia, ili kuweza kumaliza miradi hiyo kwa wakati na kumaliza madeni yanayotokana na miradi husika.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali ichukue deni la ujenzi wa barabara tatu na kulipeleka katika taasisi zake za kifedha ili ipunguze kiasi ya riba iliyokuwepo kutoka asilimia 20 hadi asilimia 5, ili kupunguza hasara kwa serikali yetu ambayo inatokana na nguvu za wananchi.

Aidha, kamati inaishauri serikali kupunguza miradi ya ujenzi wa barabara ili kuwezesha fedha zilizopo ziweze kumalizia barabara zilizopo kuliko kuwa na miradi mingi ya barabara ambayo mingi haimaliziki kutokana na ukosefu wa fedha.

**SEKTA YA USAFIRI WA ANGA**

**MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE**

Mhe. Spika, kamati inaipongeza serikali kwa kuendelea na ujenzi wa *Terminal II* baada ya ujenzi huo kusita kwa muda mrefu. Aidha kamati inapenda kuitahadharisha serikali kupitia Wizara ya Miundombinu

na Mawasiliano kuhusiana na uendeshaji wa uwanja huo unaotarajiwa kumalizika hivi karibuni kwa kuhakikisha kuwa inaanza kujipanga juu ya kuajiri wafanyakazi watakaotoa huduma katika jengo hilo ambao hawapungui 400, ambao wengi wao watakuwa na kazi maalum zitakazohitaji mafunzo ya *Aviation Security* na mafunzo mbali mbali kulingana na kazi za viwanja vya ndege ili kukidhi viwango vya kimataifa vya utoaji wa huduma.

Mhe. Spika, kamati imeridhishwa sana na juhudi zinazofanywa na Mamlaka katika kuuendeleza uwanja wa Abeid Amani Karume kwa hatua mbali mbali. Kwa namna ya pekee kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka kwa kujenga jengo jipya la kuondokea abiria wa ndani. Sambamba na pongezi hizo, kamati inaishauri Mamlaka kuweka huduma katika eneo hilo ambazo zitawahudumia wasafiri katika eneo hilo, huduma hizo ni kama vile upatikanaji wa kahawa na vitafunio. Aidha kamati inasisitiza ujenzi na uendelezwaji wa Uwanja wa ndege wa Pemba kwani hali yake siyo ya kuridhisha hata kidogo.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu kamati imeiomba serikali kufikiria upya suala la kuwapatia angalau asilimia ndogo inayotokana na mapato ya huduma za uendeshaji wa uwanja wa ndege Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili ipate kujiendeleza na kuleta ufanisi katika viwanja vyetu vya Unguja na Pemba.

Hivi sasa Mamlaka inapatiwa kiasi cha tozo inayotokana na *safety fee* inayopatikana kwa abiria wa Zanzibar na wageni ambayo bado haikidhi kwa mahitaji ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, katika viwanja vya ndege kuna huduma nyengine ni muhimu kuwepo ili kurahisisha utendaji wa kazi kwa ufanisi na kuvipa sifa viwanja vya ndege kutokana na Sheria za Kimataifa. Kutokana na hilo mamlaka inalazimika kununua baadhi ya vitendea kazi kama *conveyor belts* na mashine za *x-rays* ambazo ndizo zana zinazohitajika. Ununuzi wa vifaa hivyo hufanywa na Mamlaka yenyewe bila ya kupata nguvu kutoka serikalini.

Mhe. Spika, kamati inaiomba serikali kuhakikisha kuwa viwanja vyetu vya ndege vinafuata Sheria za Kimataifa kwa kuvipatia vifaa vinavyotakiwa pamoja na kudumisha masuala ya zimamoto kwa kununua magari maalum. Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutaka kuutengeneza Uwanja wa ndege Pemba kwa hatua ya kutia taa na kurekebisha jengo la abiria, ni matumaini ya Kamati kwamba hatua hiyo itarudisha hadhi na sifa kwa viwanja vyetu vya ndege Zanzibar.

**SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI**

**KUHUSU MAENDELEO YA UJENZI WA MELI MPYA**

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Serikali kuhusiana na Maendeleo yenye kuridhisha ya ujenzi wa Meli mpya ya MV Mapinduzi II inayojengwa nchini Korea na Kampuni *ya STX Marine Service*, kwani hatua iliyofikiwa hadi mwezi Februari ilikuwa ni kuishusha meli hiyo kwenye Maji (*dry docking*) ambapo shughuli hiyo ilifanyika tarehe 12 Februari, 2015 huko *POSCO PLANTEC Yard* nchini Korea na kushuhudiwa na Viongozi mbali mbali wa Serikali akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa niaba ya Kamati.

Kamati iliarifiwa kuwa hatua iliyobakia ni matengenezo madogo madogo ya kukamilisha ujenzi wa meli hiyo, hivyo matarajio ya Kamati ni kwamba meli hiyo itawasili nchini karibuni kwa ajili ya kuanza kazi ya kusafirisha abiria na mizigo ili kuwaondolea tatizo la usafiri wananchi wa Zanzibar.

**MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI**

Mhe. Spika, mamlaka ya usafiri baharini ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya Baharini, sambamba na jukumu hilo la msingi mamlaka inasimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogovidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia pamoja kusimamia shughuli za upakiaji wa abiria kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika.

**KUHUSU KUSITISHWA KWA MKATABA WA *PHILTEX***

Mhe. Spika**,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka wa 2007 ilifunga mkataba na kampuni ya *Philtex Corporation Limited* kwa kazi za kuendesha uwakala wa kusajili Meli za kigeni kwa niaba ya Serikali mkataba ambao ulikuwa ni wa miaka 10. Madhumuni makubwa ya Serikali kuanzisha Wakala huo ni kutoa fursa kwa Zanzibar kushiriki katika biashara ya kimataifa ya usafiri baharini na pia ni njia ya kujiongezea mapato kwa ajili ya uendeshaji kazi za usimamizi wa usalama wa usafiri Baharini.

**UAMUZI WA KUSITISHA MKATABA WA KAMPUNI YA *PHILTEX***

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifikia uamuzi wa kusitisha mkataba na kampuni ya *philtex* mnamo mwezi wa Januari 2013 uamuzi ambao ulitokana na wakala huyo mara kadhaa kukiuka vikwazo vya kimataifa vilivyowekwa dhidi ya nchi ya Iran, pamoja na kuwa wakala huyo alitakiwa kuzifutia usajili meli 36 mnamo mwezi wa Julai 2012 na kutekeleza agizo hilo, lakini bado alibainika kuendelea na kuzipatia usajili meli nyengine za Iran kinyume na agizo la Mamlaka ya usafiri, la kutakiwa kusita kusajili meli hizo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi iliunda kamati ya kusimamia usitishaji wa Mkataba huo ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa na jukumu la kutafuta kampuni nyengine itakayoendesha biashara ya kusajili meli kwa niaba ya Serikali ambapo hatimaye ilipatikana kampuni ya *Al –Khaleej Industries* iliyopo maeneo ya Bandari huru Sharjah, ambayo kwa mujibu wa mkataba wake itakuwa na jukumu la kutafuta Ofisi pamoja na kutafuta soko. Mkataba huo ulifungwa tarehe 11 Oktoba 2014.

Mhe. Spika, Kutokana na kusitishwa kwa Mkataba wa *Philtex* ambao ulikuwa ukiingiza mapato kwa Serikali na Mamlaka ya Usafiri Baharini, ni dhahiri kuwa kwa kusitishwa mkataba huo Mamlaka imeyumba sana kimapato hali inayowalazimu kuomba kuongezewa ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya kumudu kuendesha shughuli zao. Kutokana na hilo Kamati inaiomba Serikali katika Bajeti ya mwaka 2015/2016 kuangalia uwezekano wa kuiongezea ruzuku Mamlaka ili iendelee kusimamia usafiri baharini kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mamlaka imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kukosa jengo la Afisi kwa muda mrefu na kuwalazimu kukodi jengo kwa gharama kubwa, na ukizingatia Mamlaka bado ni taasisi changa, Kamati inaishauri Serikali kutafuta namna ya kuwapatia Ofisi ili waepukane na kukodi jengo, na gharama hizo zitumike kwa ajili ya shughuli nyengine za Mamlaka ukizingatia hata vitendea kazi hasa vya uokozi bado ni kitendawili katika taasisi hii muhimu.

Mhe.Spika**,** kuchelewa kwa Tanzania kuridhia Mkataba wa *'Maritime Labour Convention'* kunasababisha meli za Zanzibar kuzuiwa katika bandari za kigeni, kutokana na mabaharia wa meli hizo kutokuwa na vyeti vya ubora ambavyo mamlaka haiwezi kutoa vyeti hivyo kwa vile mkataba huo haujaridhiwa na nchi yetu. Kutokana na hilo kamati inaishauri Serikali kufuatilia suala hili katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kuhakikisha kuwa Mkataba huu unaridhiwa kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa huu ni Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambao umeeleza kwa ufupi kuhusu mambo ambayo kamati imeyatekeleza katika wizara mbili inazozisimamia, hivyo maelezo ya kina yanapatikana katika Ripoti

kubwa ya Kamati ambayo ni imani yangu kwamba kila Mjumbe ameshapatiwa. Hivyo ni vyema Wajumbe wakaipitia kwa makini ili wapate kuijadili Ripoti na hatimaye kuiboresha na kuikubali.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wa kamati ambao walinipatia mashirikiano makubwa katika kazi zetu za Kamati na hatimaye kuniwezesha leo kuwasilisha Ripoti ya Kamati kwa mwaka 2014/2015 kwa niaba yao. Nawaomba waendelee na mashirikiano yao ili tufanikiwe zaidi katika kuwawakilisha wananchi waliotuchagua.

Mhe. Spika, kwa umuhimu mkubwa naomba niwatambue Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa — Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu — Mjumbe
4. Mhe. Marina Joel Thomas — Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali — Mjumbe
7. Mhe. Mohammed Haji Khalid — Mjumbe
8. Ndg. Maryam Rashid Ali — Katibu
9. Ndg. Saad Othman Saad — Katibu

Mhe. Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo nitamaliza ripoti hii bila ya kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia katika muda wote wa kazi za Kamati ili kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kutoa shukurani za dhati kwako Mheshimiwa Spika kwa msaada mkubwa uliotupatia ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na maelekezo mbali mbali katika kutekeleza majukumu ya kamati yetu, lakini pia nawashukuru watendaji wote wa Afisi ya Baraza la *Wawakilishi* wakiongozwa na Katibu kwa kuiwezesha kamati kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. (*Makofi*)

**Mhe: Spika:** Ahsante sana Mhe. Marina Joel kwa uwasilishaji huo mzuri wa ripoti ya Kamati. Waheshimiwa Wajumbe sasa mjadala uanze na kama ilivyo kawaida naomba nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na muda ukiwepo tumsikilize Mhe. Hamza Hasssan Juma. (*Makofi*).

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, mimi leo sitakuwa na mchango mkubwa sana kwa sababu ripoti zote zimekwenda na yale mahitaji ya Kamati. Isipokuwa lazima kunakuwepo na vionjo vya hapa na pale kwa sababu kamati binadamu na waziri naye huwa binadamu pamoja na watendaji wake. Ndio maana tunaambiwa binadamu imo kusahau, binadamu imo kukumbushwa.

Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze sana na niwapongeze wanakamati kutokana na maamrisho yao hasa katika mawasiliano na uchukuzi waliotoa nimefurahika nao sana, na kwa asilimia kuwa inaonesha ripoti

hii kuna mambo ambayo wameweza kujisaidia kuyatekeleza, hilo ndilo lengo la Waheshimiwa kwa kuionesha serikali nini wanachokitaka kwa kuwasaidia wananchi.

Mhe. Spika, mimi nakwenda katika ukurasa huu wa kumi. Juzi Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa na Vikosi Maalum nilieleza suala moja mimi suala la vituo Mhe. Waziri alilikwepa sana na akalisema kuwa yeye si muhusika. Mhe. Spika, mara nyingi sana mimi nasema kuwa tunapofanya mambo ya mageuzi au tunapotaka kufanya jambo ambalo lilete sura au lilingane na sheria katika nchi za wenzetu, wala tusitake kwenda Marekani, tusiende wapi, tuangalie wenzetu hasa hapo nyumbani Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kituo cha daladala kuondoshwa pale Darajani na hapajulikani walipowekwa ni suala la usumbufu halimo hata kwenye sheria. Kwa sababu haijulikani tumewaweka wapi na wamalizie wapi, leo vituo vinamalizia Makao Makuu pale chini ya mlango wa Chama changu Chama cha Mapinduzi na sehemu nyengine inasambaa Mhe. Spika, huo ni usumbufu.

Nasema kwa upole sana kwa masikitiko Mhe. Spika, ni usumbufu na hasa saa za jioni angalia kimamama Mhe. Spika. Watu haijulikani kuna maandamano, hakujulikani kuna sherehe, hakujulikani kuna mikutano, wao watu masikini ya Mungu wapo tu wanakwenda huku wakirudi huku ni hatari ambayo tumeifanya.

Mhe. Spika, mimi sifahamu hebu naomba ile sheria mliichukua wapi kwa sababu leo ukienda Marekani kuna *Stop* ambayo iko *Washgton DC* utakuta Mhe. Spika, vituo vipo. Sasa mimi nashangaa Marekani wana vituo vya *town* seuze sisi wa Zanzibar ile *Stone town* tunaona tabu kuweka pale. Mhe. Spika, pale ni kitu ambacho cha kuchekesha kweli, twende zetu *Mainland* utakuta Kariakoo ndio mji wenyewe, lakini utakuta vituo viko pale.

Sisi leo tunakwenda mji wapi ina maana Makao Makuu ndio tunasema ndio *town* mimi nashangaa haieleweki Mhe. Spika, hebu tuwape eneo ambalo la kudumu ili mtu ajue, kwa sababu tumeondoa gari tuweke gari. Sasa hapo ndipo vichekesho vikubwa tatizo lipi, hapo mimi nashangaa tunawahangaisha tunawasumbua askari masikini ya Mungu bustani zote zimekufa. Mhe. Spika, nenda kaangalie sasa watu wanajificha kwenye bustani. Hatuoni tabu hizi sheria jamani, ndio mimi nasema *kutembea ni kusoma,* ukiweza kutembea utaona mambo mengi. Twende zetu hapo India tu Mumbai pale nenda kaangalie ndio *Stop,* nasema kitu kwa ukweli sibahatishi nina *memory* ndani ya kichwa kila nchi ninayokwenda mimi na-*note* .

Leo tunakuja kuona mazingira haya ni aibu. Halafu mimi nakaa Zanzibar naona aibu wageni wangu wakija hapa niwaambie wapi *town* ni aibu! Naomba sana Mhe. Spika, hilo tulirekebishe haraka sana, tuwape uhuru wa Mhe. Spika. Pale kama tunasema kuwekeza basi pale mnaekeza kwa sababu wanatia pesa nyingi hawaharibu mazingira hawaharibu chochote, mimi nasema watu wengine hawako *serious* na nchi. Hawako *serious* na nchi hawako *serious* na wananchi wenyewe.

Sasa mimi naomba sana ikiwa Mhe. Waziri kwa kuamini na Naibu wake kama ni kweli mna jukumu nyinyi lile tuwaoneeni huruma Wazanzibari tuwarudishie kituo chao pale kwa sababu wanakwenda masafa marefu mtu anatoka Bandarini hajui aende wapi akaikute gari ya daladala anakuja Kisiwandui na mzigo kutoka Bandarini mpaka kule, mara Baraza la Wawakilishi la zamani haijulikani kama ndio pale kama *official* au kituo chenyewe.

Mhe. Spika, kwa kweli tunawanyanyasa waendesha daladala na wananchi wao. Kwa sababu mwenye daladala hakuna tatizo lakini huyu mwananchi wanasumbuka Mhe. Spika, wanatolewa faini kila leo kila wanaposimama wanatolewa faini. Kwa kweli ninaomba sana Mhe. Waziri atusaidie kwa hili ili tuone mji wetu umekaa vizuri, ikiwa kama mazingira yale sio mazingira mazuri, mimi nashindwa, hata Ulaya hakuna kama ile mimi sijapata kuona, unaweza kuona watu wana- *work* kwenye *street* lakini wanajua

wanakwenda wapi. Lakini leo pale CCM watu hivi kibao heee basi tuwaingize ndani wanachama wetu hamna tatizo lolote. Mimi naomba sana hili tulisaidie sana.

Lakini niende katika asilimia walioiomba Uwanja wa Ndege. Kwanza hapa naomba sana nimpe pole Mkurugenzi *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie amponeshe kwa haraka sana, tuje kuungana naye katika masuala yetu haya ya utekelezaji.

Mhe. Spika, kwa kweli asilimia hii tuwasaidie hawana asilimia na wanafanya kazi vizuri sana. Mhe. Spika, wanajitahidi sana, sasa hivi Uwanja wa Ndege *alhamdulillah* Uwanja wa ndege ni mzuri sana, hiyo haki yao tuseme kila usiku ukicha mambo yanageuka ilikuwa zamani njia unazunguka ndani kwa kwenda kule kutoa mizigo lakini leo kuna *special road* imetiwa lami vizuri.

Mhe. Spika kwa kweli Mkurugenzi nimpe hii hongera sana, na hiyo asilimia iliyokuwepo tuweze kumpa, lakini hapa nilipata suala, nimeona vizuri tu kuwa hata huyo mwekezaji mwengine baada ya mshirika mwenzake *ZAT* tushaambiwa kuwa karibuni atakuja kuanzisha hizi shughuli na vitu anaanza kuleta. Naomba Mhe. Spika, aje haraka sana ili kuweza kumaliziana naye ili tuone maendeleo zaidi yanavyokwenda katika mawasiliano hayo.

Mhe. Spika, nawashukuru sana mashirika mengine hayo Shirika la Meli, Shirika la Bandari, kutokana na jitihada zao na kazi zao wanazotuonesha humu zimekwenda kwa ufanisi mkubwa sana, kama nilivyosema makoseo madogo madogo hayaachi kuwepo, lakini kwa hatua hii waliyofikia niwapongeze na niwashukuru sana.

Naingia Ardhi. Mhe. Spika, niwapongeze sana watu wa ardhi, lakini nianze na Nishati. Mhe, Spika, tulitunga sheria sijui niite ilikuwa azura au uzuru au vipi kidogo imenitoka ZURA. Mhe. Spika, ZURA jamani naomba radhi mdomo kuteleza imo, sasa naomba nieke sawa niseme vipi? Zura, Mhe. Spika, wenzetu kule tuna sijui *EWURA* kuna kule Dar es Salaam, wenzetu hawa wanakuwa waadilifu sana kwa sababu sasa hivi mafuta yameshuka bei.
Mhe. Spika, Idara hii tulileta hapa tukaipanga hapa Mhe. Waziri usione tabu kuwatia watu kufuli, wanatusumbua mafuta hawataki kushusha bei halafu isitoshe wanayazuia kwa makusudi. Mhe. Spika, naomba sana mchezo huo wasituchezee tumechoka nao, wanatusumbua wanatupeleka kwenye mafuta ya magendo ambayo yanachanganywa na maji tunaua vyombo vyetu kwa makusudi Mheshimiwa. Katibu watieni kamba, kwani tatizo liko wapi, nyang'anyeni mtu leseni, wanazoea, wanatutania. Serikali ikachezewe ndevu, heee! Ni kitu kinanishangaza, mimi inanisikitisha sana serikali mtu anaichezea, serikali kwa sheria hatari huyo mtu tumuogope. Kama kweli tunamwachia huyo mtu serikali anaichezea tumuogope sheria, sheria, Mhe. Waziri ondoka kamata watu nyang'anya watu leseni!

Hili Mhe. Spika, suala ambalo linaumiza sana na linasikitisha sana. Ninaomba sana liweze kuchukuliwa amri mara moja. Na mafuta wenzetu Bara wanazidi kushusha na wao kama wezi basi na wakae nyumbani watizamwe nani anaweza *wallahi* Bakhressa anaweza kabisa na wamwachie *Bakhressa* mara moja tu. Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa wamenielewa na kunipigia makofi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, niende katika Shirika la Umeme. Nawashukuru sana kwa jitihada zao na hasa katika masuala haya ya kuweka vituo karibu kwa wananchi katika ulipaji, hilo mimi nakubaliana nalo sina tatizo na naomba sana *speed* hiyo ya kuekeza kwa wananchi mradi huo uendelee.

Mhe. Spika, naomba kwa sababu sasa hivi wananchi wengi wanatumia umeme Zanzibar, na tena umepanda kwa asilimia kubwa, vijiji sasa hivi vinang'ara. Vijiji vimekuwa mji siyo tena vijiji kutokana na kupata umeme kwa wakati.

Lakini tatizo sasa hivi ninasikia watu wanapiga kelele mita, sijui kama zimeshakuja kama zipo tunaomba sana. Nimuombe Meneja na watu wake wajipange ili kufikisha hizo mita kwa wakati unaotakiwa.

Mhe. Spika, vile vile nilitaka kutoa tahadhari. Kuna suala la wafanyakazi wanalalamika kuhusu suala hili la upungufu wa miaka. Mhe. Spika, kwa kuwa hili suala lipo, naomba sana lifuatilie na ninamshukuru sana Meneja amelifanyia kazi vizuri lakini aliyemkabidhi bado hajataka kulitekeleza, wanalia sana wafanyakazi.

Mhe. Spika, shirika hili linafanya kazi ngumu sana, unapofika pahali anaona haki yake unamnyima kwa makusudi, kwa kweli halitii sura nzuri kwa sababu ni hali ya hatari. Meneja amejitahidi na kulishusha lakini huyo aliyeshushiwa bado analiviza, sijui sababu gani. Hapa mimi nashangaa, wewe ni mtendaji kwa mujibu wa sheria lifuatilie kwa sheria, mrudishie Meneja kama umemaliza au hujamaliza lakini unawasumbua watu. Jamani hii ni hatari, kusumbuana kwa kweli inaleta sura mbaya. Mhe. Spika, hilo suala siyo vizuri.

Mhe. Spika, ninawashukuru *ZAWA* kwa kutuletea maji kwenye vijiji na wajitahidi katika misingi ambayo ili tufikishe pale. Mhe. Spika, nina masikitiko. Mhe. Spika, humu sijaona migogoro na ninashukuru sana kwa kuwa migogoro haipo lakini binadamu inakuwa tukusaidie sisi.

Mhe. Spika, nina hati hapa naomba niisome ili nimalizie na hati nyengine mbili tatu hizi ninamalizia, kama nilivyokwambia leo sina mchango mkubwa, nina utetezi wa wananchi tu.

Mhe. Spika, inasema Ushirika wa *Tutafaidika* kuhusu upandaji miti. Kuhusu kupatiwa utambulisho cha umiliki wa ardhi. Kutokana na ofisi iliyoomba uliopitishwa kwenye vyombo vinavyohusika hatimaye kupatikana ushauri wa Kamati ya Wilaya na Mkoa za ushauri na ardhi, mazingira na barua ya mwaka 1999.

Mhe. Spika, hao ni wananchi ambao wapo katika Jimbo la Kitope, hii ni *double location*. Hawa ni mwanzo wamepewa mwezi Disemba, 1998 lakini kuna watu wengine wamepewa hati dhidi ya hawa walioomba tena ni wana ushirika, yeye ni *one person*, hawa ni watu wengi. Kwa hivyo, hii Mhe. Spika, kosa tayari linajionesha wazi warejeshewe hawa walioomba mwanzo. Ninaomba sana Mhe. Spika, ili suala lako kusaidia.

Mhe. Spika, lakini nina barua nyengine ambayo huyu mama muliuzia nyumba kule Pemba. Afisa Mdhamini Afisi ya Nyaraka kupatiwa waraka wa nyumba ya kijiji nambari saba iliopo Makombeni ni Bibi Miza Khamis Haji.

Mhe. Spika, amelipa shilingi laki nne na hamsini(450,000) lakini kuna kijana mmoja wa KMKM hataki kutoka, nyumba si yake. Mhe. Spika, naomba huyu mama tusimsumbue ambaye amesaini mwalimu wangu Mwalimu Hemed Salim Hemed, huyu mama apewe nyumba yake ameshalipa. Tulitoa sheria hapa nyumba za zamani ziuzwe, kwa hivyo yeye hakuwahi kununua, hakuwahi kuitaka aliyetaka apewe haki yake. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana hili agizo, sisemi kwa mdomo, ninasema kwa waraka huu hapa ambao mumetoa nyinyi Serikali. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, asaidiwe huyu mama.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana viongozi wangu, lakini ninachotaka kusema ni moja tu. Mhe. Spika, sisi Wawakilishi kazi yetu kuielekeza Serikali. Kuna watu Mhe. Spika, hawafahamu kazi yetu ni nini. Kazi yao ni kutuandika kwenye mabango tu, hiyo sifa ya mabango. Mimi ninashukuru sana Mhe. Spika, aangalie mtandao nimeandikwa kwenye bango.

Ninashukuru, wao hawajui wanaona labda mimi nitakonda, hawajui kwangu mimi vile ni mbolea, hawajui kwangu mimi kunitangaza, kwa sababu unajua unapomuweka katika mtandao na

ninayozungumza hapa ni ya kusikitisha, kwa sababu hapa nimemtetea mwananchi, sikutetea kitu chengine. Sasa angalieni kwenye mtandao nimeingizwa mule, lakini ninamuona jamaa kapitwa na wakati. Mimi ndiyo sheria ninamwambia tena, hapa ninachotetea ni wananchi walionituma kuielekeza Serikali iweze kufanikisha.

Mhe. Spika, unataka kunipa dakika 5 za kumalizia, simalizi dakika 5. Mhe. Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu wake, Mkurugenzi wake, nimshukuru Mheshimiwa babu yangu Waziri na Naibu Waziri wake Mwenyezi Mungu akubarikini kwa leo kutuonesha ripoti yenu ndiyo kwanza *the first time*, ripoti ilivyokuwa nzuri sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa hayo machache sana. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana ninakushukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa mchango huo. Nimkaribishe basi Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumza kutilia nyalio katika ripoti hizi za kamati pamoja na majibu ya Mawaziri.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze na kitendawili. Kitandawili changu kinauliza, kuna mji mkuu gani duniani uliokuwa hauna kituo kikubwa cha daladala? Zanzibar eeh! Umepata, zawadi yako nje. *(Makofi).*

Mhe. Spika, suala alilozungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ni suala sahihi kabisa. Kama kutembea Mhe. Spika, umeshatutembeza sana duniani na tunayokwenda kujifunza tuje kuielekeza Serikali yetu. Serikali watafute pesa wanunue nyumba wavunje waweke kituo cha daladala. Kwa mujibu wa sheria pale Ofisi Kuu ya CCM huwezi ukasimamisha gari, gari pale zote zinazosimama anatakiwa *traffic* azikamate kwa sababu zipo barabarani, zime-*park* barabarani. Leo ndiyo kituo cha daladala. *It's a shame! (Makofi).*

Mhe. Spika, kitendawili cha pili. Ninakuulizeni kuna nchi gani duniani taa za kuongoza magari, taa inakuongoza uilekee kushoto kumbe unatakiwa uende kulia. Leo mambo haya yanafanywa na sisi ndiyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tunatakiwa tuisimamie Serikali, tunaangalia tu.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wewe unaendeshewa gari, hebu siku moja endesha mwenyewe, nenda zako Ofisi Kuu ya CCM ukitoka fanya kama unaelekea Skuli ya Haile Selassie halafu iangalie taa, halafu wewe utake kwenda zako Mnazi Mmoja, uangalie taa inakwambia uende wapi? Uende Darajani. Manispaa wapo, kuna wakurugenzi wana *PhD* na kila kitu, leo makandarasi wanapewa sijui watie taa za barabarani aibu tupu. Taa ile ikang'olewe au izimwe*! (Makofi).*

Leo Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mshimba munatusafirisha sisi, tunakuja na watu wenye akili zao, anakwambia si tunaelekea huku mbona unakwenda huko. Ninamwambia aah! Ile taa haielekezi huku, ile unatakiwa uende huku, anasema ile inaelekeza huku, munakamata kwenye sukani. Kwa hivyo vitendawili hivyo viwili, hiyo ndiyo taswira ya mji wetu wa Zanzibar. Hatutaki kuonekana kama hao. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya hapo ninataka nianze na mchango wangu. Mhe. Spika, ninawashukuru sana Mawaziri kwa taarifa zenu, lakini mimi nilikuwa nianze na miundombinu. Naanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, taarifa ya Waziri tumeisikia kuhusu suala la *ground handling* na munasema kuna kampuni mushatia nayo mkataba kwa tarehe uliyotaja hapa kutokana na muda sitaki kuirejea, vifaa vipo njiani. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa taarifa nilizokuwa nazo, hiyo kampuni muliyotiliana saini sijui kama imefuata sheria. Naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri ukija hapa usinifiche kitu, wewe mtu wa Mkwajuni mwenzangu, Chaani na Mkwajuni baba mmoja mama mmoja, utwambie wewe umeridhika na yaliyofanyika.

Haiwezekani kazi imetolewa *tender*, sheria za *tender* tumezipitisha hapa. *Tender* inapopitishwa katika Bodi, maamuzi ya Bodi ndiyo yaheshimiwe. Leo tuangalie hiyo kampuni Mhe. Spika, Mhe. Waziri aliyotutajia ndiyo iliyoshinda kwenye huu mradi, musituletee kampuni za mikobani. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kampuni hiyo na ninataka Mhe. Waziri aje atupe taarifa kabla ya Mwenyekiti, atwambie imefanya kazi nchi gani, ina uzoefu gani, ina wataalamu wa aina gani. Ina maana kama kampuni haijawahi kufanya kazi, haina *experience*, ina maana huo mkataba ni feki, arudishe vitu vyake. Kampuni iliyoshinda ipewe kazi au *tender* iitishwe tena. *(Makofi).*

Mhe. Spika, Uwanja wa Ndege leo ule tunategemea Mwenyezi Mungu akitujaalia, sijui Mhe. Waziri wa Fedha pale ulinikatisha nilikuwa sijamaliza maneno yangu, nilikuwa nataka atwambie Uwanja wa Ndege utamaliza lini, lakini ndiyo ukaniambia ooh!

Sasa Mhe. Spika kupitia hapa ninataka niambiwe Uwanja wa Ndege utamaliza lini. Uwanja wa Ndege ule Mhe. Spika, kile ni chanzo cha mapato cha nchi. Serikali tunajua imeshaumia sana, tumeshakula hasara lakini hatuna jinsi lazima uwanja tuumalize, hatuwezi kuliacha gofu tu pale na kampuni inayotakiwa katika masuala ya *handling*, ile kampuni yenyewe inatakiwa iwe na *experience*, imeshafanya kazi duniani tayari ina ndege. Ina maana uwanja ukifungua kuna ndege zitaletwa na hiyo ya Kampuni ya *ground handling*. Je, hii muliyokuwa nayo nyinyi, ime-*handle* mashirika mangapi ya ndege.

Mhe. Spika, ukileta kampuni kuja kujifundishia kazi pale, sisi Zanzibar tusigeuzwe kichwa cha mwendawazimu watu kuja kujifundishia kunyoa. Leo pale tunataka kampuni ikija tu madege siku ya pili yamejaa pale Uwanja wa Ndege, kila mmoja anasema nipishe mimi. Munatuletea kampuni ije kujifundishia kazi pale.

Mhe. Spika, naomba sana kwa Mhe. Waziri inawezekana pengine taarifa ulizozipata siyo sahihi, lakini taarifa za kwako ndizo zitakazokuwa sahihi, na nikizifuatilia ukiniambia siyo sahihi, nitakusubiri kwenye bajeti, ijapokuwa itakuwa ndiyo ya mwisho, lakini itakuwa ndiyo wakati mzuri wa kuagana huku tunakamatana tai. *(Makofi).*

Mhe. Spika, pamoja na maboresho ya Uwanja wa Ndege lakini hebu ufanye ukaguzi wa miradi yenu muliyofanya, maduka yale sijui kama yenu au ndiyo ya Mamlaka au vipi. Kuna msikiti pale mumefanya jambo zuri, lakini msikiti kwa mila zetu haukai karibu na baa. Sasa sijui ile baa ni ya mkubwa au ya nani. Naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri aifanyie kazi. Mhe. Spika, kama kweli ipo basi aidha uifunge baa au ufunge msikiti. Sasa sijui utafanya lipi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kutokana na muda na ninaona unaniangalia sana, nina mambo mengi ya kutaka kuyazungumza nilikuwa ninakuja katika eneo la pendekezo la 56 (b) kuhusu suala la *Bakhressa*, kamati imependekeza anatakiwa kufanya maboresho au kuendeleza Bandari ya Wete.

Hizi taarifa tumezipata, na kwa kuwa kamati imeeleza itabidi ukweli upo vipi. Na taarifa nilizokuwa nazo mimi kwamba inataka kujengwa bandari kwa kutumia meli za *Bakhressa* tu. Kama hiyo ni kweli Mhe. Spika, hilo suala siyo sahihi na hata ikiwa vipi. Kwa sababu ina maana hapa juzi tumepitisha sheria ya *PPP* na tulipendekeza katika kamati yangu, sijajua Wajumbe wangu sijakaa nao kwa utulivu kwamba yale mapendekezo ambayo tuliyopendekeza yaingizwe.

Tulipendekeza katika sheria basi Rais awe na mamlaka awe na uwezo, kwa sababu wenyewe walitaka kuwe na ma-*senior officers* tu ambao watumishi wa Serikali ambao wameshafanya kazi muda mrefu ndiyo waweze kushika taasisi mbali mbali. Sisi tukapendekeza basi hata na watu binafsi ambapo Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete amefanya uzoefu mkubwa sana, kuna watu wengi ambao sasa hivi amewachagua walikuwa hawamo Serikalini wanafanya kazi vizuri.

Sasa sijajua mradi wa ujenzi wa sehemu ya abiria Malindi. Nimeuliza sana Bandari ya Malindi ilivyojengwa na *Bakhressa* tunamshukuru ameboresha vizuri, lakini mikataba mpaka leo hajaambiwa inasemaje. Hivi ni ya kwake, ni ya Serikali, *PPP* au katoa sadaka. Sasa na hii ya Bandari ya Wete vile vile tunataka maelezo na kama maelezo yatakuwa vyenginevyo, kama itakuwa kwa kutumia vyombo vyake tu, basi tusubiri Serikali yetu na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu karibu tutapata mkefu hapa mafuta yapo, gesi ipo, Serikali itajenga wenyewe Bandari, lakini kama anataka kujenga basi tunampongeza lakini vitumike vyombo vyote ili wananchi waweze kuitumia bandari hiyo. *(Makofi).*

Jengine Kampuni ya *Philtex*. Tunaishukuru sana Serikali baada ya kilio chetu cha muda mrefu, upotevu wa fedha na ubadhirifu ulivyokuwa unafanywa, kukiuka sheria za kimataifa, kampuni ile sasa hivi Serikali imetusikiliza tayari mumeshaifungia imeshafunga virago, lakini hatujui kwamba katika kufungashana virago. Je, kuna madeni au kuna nini, hilo hakutwambia lakini sasa hilo mutaangalia wenyewe baadae, lakini muhimu kwamba sasa hivi tumepata kampuni nyengine ambayo inaitwa *Al-Khaleej* iko Sharja kule.

Tena kwa bahati nzuri juzi nilipita pale, kama ningelijua kwamba hii ipo ningelipitapita nikaangalia pale, kampuni ipo vipi, lakini tunataka tujue. Hii kampuni utaratibu wake upo vipi, hii ofisi wameambiwa watafute wao kwa gharama za nani. Na mpaka sasa hivi Serikali au mamlaka inakula gharama gani kwa ajili ya hii shughuli mpya. Nilikuwa nataka kidogo maelezo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, na vile vile hizi kamati zako uzitoe. Kama hii Kampuni ya *Philtex,* kama Kamati ya Miundombinu na Ujenzi ingelipata nafasi ikaenda kule ikaangalia pengine isifike pahala mukaifungia. Pengine kamati ingelikwenda ukashauri, ukaja ukashauri na Serikali wakafanya vizuri lakini tunaanzisha vitengo nje ya nchi, halafu kamati mwisho Pemba na Unguja, Bara, Dodoma tumemaliza kazi. Mhe. Spika, tutaibiwa, tutanyang'anywa, sheria zitavunjwa, hatuna uwezo wa kuweza kushauri. *(Makofi).*

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mimi ninataka niwapongeze sana. Kuna wenzangu walipitikiwa kidogo, wakasema kwamba Mji Mkongwe sasa hivi yale majengo yameshapitwa na wakati kuendelea kuhifadhi.

Mhe. Spika, nimekwenda mimi *Ireland*, Uingereza, Ufaransa, kuna majengo tokeo miaka ya 1700. Mhe. Spika, na wewe ninajua wewe umeshakwenda mpaka yale masanamu yaliyokuwa kule yanavyowekwa, wewe mwenyewe umeshaona, mengine hata kuyatizama huwezi vile yalivyo. Nikisema hivyo nafikiri wengine waliowahi kusafiri watajua yalivyo yale masanamu ya kule.

Miaka ya 1700 leo majengo yetu ya Mji Mkongwe ni historia na ni sehemu ya watalii wanaokuja Tanzania, wakaja Zanzibar wanakuja historia ya majengo ya Mji Mkongwe. Sasa suala la kusema kwamba kila mtu afanye anavyotaka haiwezekani bwana. Mji Mkongwe lazima ulindwe na zile nyumba Serikali tukijaaliwa hivyo hivyo tutafute pesa tuyaboreshe yale majengo yasianguke, na hata yale maboresho yenyewe yazingatie yale masharti. *(Makofi).*

Mhe. Spika, tukijenga kisasa, wazungu huko kwao wanapokwenda duniani, leo ukienda Dubai pale hayo majengo yanayojengwa wala hayana maelezo, watakwenda huko. Sasa huku wanakuja kuangalia vitu vya historia, na ndivyo vijana wetu watakapopata kazi, kaja mtalii kampeleka huku, kampeleka katika chochoro hii, ndiyo ajira zenyewe zinavyopatikana. *(Makofi).*

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa nataka nizungumzie suala la ujenzi wa... *(Makofi).*

Mhe. Spika, naomba kwa makofi haya ya Waheshimiwa Wajumbe ninaambiwa dakika zako uje umalizie kesho, kwa hivyo ninaamini Mhe. Spika, utaruhusu dakika zangu nije nimalizie kesho, ili tusikiuke yale masaa yaliyowekwa kwa utaratibu.

Mhe. Spika, ninakushukuru. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Hamza ninakushukuru sana kwa mchango ulioutoa huo na muda umemalizika. Kwa hivyo, Wajumbe ninarudia tena kwamba ratiba tuliyokuwa tumejiwekea tupo nyuma, lakini hata hivyo ninawashukuru tunakwenda vizuri tunaweza tukamaliza bila ya kuongeza muda mkubwa.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe ninaahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 26/03/2015, saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:43 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/03/2015 saa 3:00 asubuhi)*